SILSILA ZA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI 3



# Nguzo Za Imani

## KUTOKA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI

UTUNZI WA

DKT. ABDUL-MUHSIN IBNU MUHAMMAD AL-QAASIM

IMAMU NA HATIBU WA AL-MASJID AN-NABAWI SH-SHARIIF

مترجم بالسواحيلية

# NGUZO ZA IMANI

## Katika Hotuba za Al-Masjid An-Nabawi

**TEREMSHA KITABU HIKI KWA KUPANGUSA KODI**

a-alqasim.com

# NGUZO ZA IMANI

## Katika Hotuba za Al-Masjid An-Nabawi

**UTUNZI WA**

**DKT. ABDUL-MUHSIN IBN MUHAMMAD AL-QAASIM**

IMAMU NA HATIBU WA MSIKITI MTUKUFU WA MTUME

بسم الله الرحمن الرحيم

NAANZA KWA KUTAKA USAIDIZI NA BARAKA KWA JINA LA ALLAH, MWINGI WA REHMA, MWENYE KUREHEMU.

## UTANGULIZI

Sifa njema zote anastahiki Allah Mola mlezi wa viumbe wote, na swala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad, watu wake na masahaba wake kwa jumla.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi Imani ina misingi sita inayojengeka nayo, mtu hawi Mwislamu ila kwa kuiamini yote, na mojawapo ukiondoka; mtu atatoka katika mila [ya Uislamu].

Hakika ya Imani ni: Kukiri kwa moyo, kutamka kwa ulimi na kutenda kwa viungo, nayo inazidi kwa utiifu na inapungua kwa maasi.

Pia inaingia katika Imani: kufanya yalioamrishwa - ya wajibu na yanayo pendekezwa -, na kuacha yaliokatazwa - yaliochukizwa na yalioharamishwa-.

Na kwa ajili ya umuhimu wa nguzo za Imani; nilitoa hotuba kuhusi kila nguzo mingoni mwazo katika Msikiti wa Mtume, kisha nikazikusanya na kizipangilia katika kitabu hiki, zikafika hotuba kumi na saba, na nikakiita: «NGUZO ZA IMANI; Katika Hotuba Za Al-Masjid An-Nabawi».

Namuomba Allah anufaishe [watu] nacho, na akijaaliye ni kilichotakasiwa Uso wake mkarimu.

Swala na salamu za Allah zimshukie Nabii wetu Muhammad, jamaa zake na masahaba wake wote.

ABDUL-MUHSIN IBNU MUHAMMAD AL-QAASIM
IMAMU NA HATIBU WA MSIKITI MTUKUFU WA MTUME

# KUMWAMINI ALLAH

## MJA KUMTAMBUA MOLA MLEZI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani neema zinakuwa katika kufuata uongofu, na uovu unakuwa katika kufuata matamanio [ya nafsi].

**Enyi Waislamu:**

Allah ameumba viumbe ili utiifu uwe ni wake na kujidhalilisha ni kwake, na ukamilifu wa saada ni katika kumtambua Allah na kumwamini. Mja kumjua Mola wake Mlezi ndio msingi wa kwanza ambao ni wajibu juu ya binadamu kuujua, nao ndio jambo la kwanza atakaloulizwa mja ndani ya kaburi lake. Allah amewaleta viumbe baada ya kutokuweko, na akawapa neema kwa wingi, na akawadhaminia riziki:

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٖ فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزۡقُهَا﴾

{Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Allah} [Huud:6].

Amewaleta walimwengu baada ya kuwa hawakuwa ni kitu:

﴿هَلۡ أَتَىٰ عَلَى ٱلۡإِنسَٰنِ حِينٞ مِّنَ ٱلدَّهۡرِ لَمۡ يَكُن شَيۡـٔٗا مَّذۡكُورًا﴾

{Hakika kilimpitia binadamu kipindi katika zama ambacho kwamba hakuwa kitu kinacho tajwa} [Al-Insaan:1].

Ni Mola Mlezi aliyepwekeka na jambo la kuumba, kuruzuku, na kuendesha:

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na tano, mwezi wa Safar, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na sita hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

﴿أَلَا لَهُ ٱلۡخَلۡقُ وَٱلۡأَمۡرُۗ تَبَارَكَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾

{Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote} [Al-a`raaf:54].

Amepwekeka na Tawhidi, amesifika na utukufu na kahari, hatamu za mambo yote ziko Mikononi mwake, ni mwenye nguvu sana, mwenye kukahiri aliye juu ya waja wake, haridhii kuabudiwa mwengine ila Yeye:

﴿إِن تَكۡفُرُواْ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنكُمۡۖ وَلَا يَرۡضَىٰ لِعِبَادِهِ ٱلۡكُفۡرَۖ وَإِن تَشۡكُرُواْ يَرۡضَهُ لَكُمۡ﴾

{Mkikufuru basi Allah si mwenye haja nanyi, wala haridhii kufuru kwa waja wake. Na mkishukuru, basi Yeye huridhia hilo kwenu} [Az-Zumar: 7].

Amesimamisha katika kila kiumbe alama ya kujulisha kupwekeka kwake; ili moyo uzidi kushikamana Mola wake Mlezi. Alama mbili zinaandamana juu yetu, ambazo zinatukumbusha kupwekeka kwa Allah, nao ni usiku unaofunika na mchana unaodhihiri, kila moja ya alama hizo inamfukuza mwenzake kwa kasi:

﴿يُغۡشِي ٱلَّيۡلَ ٱلنَّهَارَ يَطۡلُبُهُۥ حَثِيثٗا﴾

{Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi} [Al-a`raaf: 54],

Jua na mwezi zinatembea katika njia ilio pangika, yenye kushangaza wenye busara, hili linachomoza na ule unaondoka, mwendo uliopangika, hautangulii mbele wala hauchelewi:

﴿لَا ٱلشَّمۡسُ يَنۢبَغِي لَهَآ أَن تُدۡرِكَ ٱلۡقَمَرَ وَلَا ٱلَّيۡلُ سَابِقُ ٱلنَّهَارِۚ وَكُلّٞ فِي فَلَكٖ يَسۡبَحُونَ﴾

{Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao} [Yaasin: 40].

Ardhi inatubeba, na mbingu zinatufunika, wala hatuachi kuvihitajia. Uumbaji wa kina, na uendeshaji wa Muumbaji mzuri:

﴿هَٰذَا خَلۡقُ ٱللَّهِ فَأَرُونِي مَاذَا خَلَقَ ٱلَّذِينَ مِن دُونِهِۦ﴾

{Huu ni uumbaji wa Allah. Basi nionyesheni wameumba nini hao wasio kuwa Yeye!} [Luqman:11],

Na Mwislamu anajivunia kuwa mja wa [Allah] mwenye kuendesha ulimwengu huu mkubwa:

﴿قُلۡ إِنَّنِي هَدَىٰنِي رَبِّيٓ إِلَىٰ صِرَٰطٖ مُّسۡتَقِيمٖ﴾

{Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi ameniongoza kwenye njia iliyonyooka} [Al-an`aam:161],

Hamwabudu ila Mola Mlezi wa huu ulimwengu aliyetukuka na aliye juu, wala hapeleki chochote katika aina za ibada kwa asiye kuwa Yeye, anakimbilia kwake katika mambo mazito, na anamuogopa Yeye peke yake hadharani na mafichoni:

﴿وَإِن يَمۡسَسۡكَ ٱللَّهُ بِضُرّٖ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَۖ﴾

{Na Allah akikufikishia madhara, basi hapana wa kukuondolea [madhara hayo] ila Yeye} [Al-An`aam:17],

Basi hamuogopi maiti asije kumdhuru na uovu, au akatarajia ihsani kutoka kwake.

Na kukimbilia kwake peke yake ni [dalili ya] wingi wa akili, na ni amani ya moyo, na utulivu wa roho, na aliyemuogopa Mola wake Mlezi basi hataogopeshwa na yeyote; bali huwa na moyo imara na utulivu wa viungo, na ni neema ya ajabu ya nafsi isiyopata pumbao ila pamoja na Allah:

﴿فَلَا تَخَافُوهُمۡ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ﴾

{ basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini} [Aalu Imraan: 175]

Abu Suleiman Ad-Daaraani Allah amrehemu anasema: "Hofu [ya Allah] haiepuki moyo wowote ila [moyo huo] unaharibika".

Mja aliye karibu zaidi na Allah ni yule anaye muogopa zaidi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema:

«**Hakika mimi ndio mjuzi wao zaidi wa kumjua Allah, na mchamngu wao zaidi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, nayo ni miongoni mwa yanayo lazimu Imani na yanayo wajibishwa nayo, na atakayemuogopa Mola wake Mlezi peke yake atafunguliwa milango ya Pepo; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَلِمَنۡ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِۦ جَنَّتَانِ﴾

{Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi [akawa ni mwenye kufanya mema na kuepuka maovu] atapata Pepo mbili} [Ar-Rahmaan: 46]

Wenye elimu [ya sheria] walisema: "Allah hamkusanyii mja wake hofu mbili; basi atakayemuogopa duniani atampa amani siku ya Kiyama, na atakaye jichukulia amani duniani, na asimuogope Mola wake Mlezi, basi

atamuogopesha akhera"; basi mchunge Mola wako [katika maamrisho yake na makatazo yake] na muogope aliyekuumba, utakuwa mja mwenye saada zaidi mbele ya Allah.

Wala usitaraji kutimia matakwa au kusalimika na yanayohofiwa kutoka kwa asiyekuwa Allah, - miongoni mwa: kuondokewa ugonjwa na kasoro, au kupoa kwa ugonjwa, au kutaka riziki, au kuleta afya -, na yatekeleze [yafunge] matarajio yako kwa Allah pasi na wengine; kwani viumbe wamepewa umbile la udhaifu, hawana uwezo wa kuziletea nafsi zao manufaa, na kuzikinga na madhara, nao sio waweza wa kuwafanyia hayo wengine, wala hajawahi yeyote kumtarajia kiumbe ila dhana yake kwake huenda patupu, basi usifunge tamaa na matarajio yako kwa asiyekuwa Allah, kwani hautavuna ila majuto na udhalilifu wa kuomba, na tarajia ukarimu wa Allah, vipawa vyake, na neema zake nyingi, kwani kutarajia yalio kwa Allah ni ibada, na mnao katika kudhalilika moyo kwa Allah nguvu na ushindi wa nafsi, kunyanyuka daraja, na kupata matarajio.

Na raha [mapumziko] ya nafsi yamo ndani ya kutegemeza amri yake kwa Muumba wake, na mashikamano yake na Mola wake yanazidi inapokumbuka ya kuwa Mola wake ni Mjuzi wa hali yake, ni mwenye rehema na jambo lake, ni muweza wa kumwondolea madhara yake, na kwanini [moyo] kushikamana na kiumbe asiye weza kuondoa madhara, mgumu katika kutoa?! Na hali Mola wako anakutosheleza mambo yako yote; naye ni mwenye kuyasimamia endapo utampelekea haja zako, na ukamkabi hatamu za mambo yako.

﴿وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُۥٓ﴾

{Na anayemtegemea Allah Yeye humtosha}[At-Twalaaq: 3].

Na mwenye saada ni yule mwenye shauku na rehema za Allah, na mwenye kuogopa adhabu yake, aliye dhalili katika kumwabudu Mola wake, na hizo ni sifa za hali ya juu zilizosifika nazo nyumba za Manabi; [Allah] aliyetakasika alisema kuhusu Zakariya [salamu zimshukie] na jamaa zake:

﴿إِنَّهُمْ كَانُوا۟ يُسَٰرِعُونَ فِى ٱلْخَيْرَٰتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ۖ وَكَانُوا۟ لَنَا خَٰشِعِينَ﴾

{Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea}[Al-Anbiyaa: 90],

Na Mitume ni wenye kutangulia mno katika kuwa na shauku ya yaliyo kwa Allah; [Allah] aliyetakasika alisema kumwambia Nabii wake Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie:

﴿وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَٱرۡغَب﴾

{Na Mola wako Mlezi ndio mshughulikie}[Ash-Sharh:8].

Nayo shauku ya yaliyo kwa Allah inapungua kwa mja kwa kadri ya madhambi, na inazidi kwa kuzidi imani, Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Allah anapomtakia mja heri, humuafikia katika kutumia uwezo na kufanya bidii katika kumshughulikia Yeye na kumuogopa Yeye; kwani hayo mawili ndio vyanzo viwili vya kuafikiwa, kwa kadri itakavyo simama shauku na hofu ndani ya moyo ndio itapatikana taufiki".

Na kuogopa kiumbe ni udhalilifu na utwevu, na atakayemuogopa Muumba wake ataishi akiwa azizi, na atakuwa ni mwenye saada katika maisha yake, na hilo litang'arisha fahamu yake awe mwenye kukumbuka [kumkumbuka Allah], [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿سَيَذَّكَّرُ مَن يَخۡشَىٰ﴾

{Atakumbuka mwenye kuogopa}[Al-a`laa:10],

Na atafaidika na mawaidha na mazingatio; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبۡرَةٗ لِّمَن يَخۡشَىٰٓ﴾

{Kwa hakika katika hayo kuna mazingatio kwa wanaoogopa} [An-Nazi`aat:26],

Na Kitabu cha Allah kitakuwa kwake ni Saada na ukumbusho:

﴿مَآ أَنزَلۡنَا عَلَيۡكَ ٱلۡقُرۡءَانَ لِتَشۡقَىٰٓ * إِلَّا تَذۡكِرَةٗ لِّمَن يَخۡشَىٰ﴾

{Hatukukuteremshia Qur-ani ili upate mashaka * bali ni mawaidha kwa wenye kuogopa} [Twaaha: 2-3],

Nalo [jambo la kumuogopa Allah] ni lenye kuwajibisha msamaha wa Allah na vipawa vyake vingi:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يَخۡشَوۡنَ رَبَّهُم بِٱلۡغَيۡبِ لَهُم مَّغۡفِرَةٞ وَأَجۡرٞ كَبِيرٞ﴾

{Hakika wanaomuogopa Mola wao Mlezi kwa ghaibu watapata msamaha na ujira mkubwa} [Al-Mulk:12],

Basi mjaaliye Mola wako Mlezi mbele ya macho yako, wala usijiaminie makri yake [mipango yake] na kushuka kwa adhabu yake, wala usimuogope

asiyekuwa Allah katika kukatika kwa riziki, au kuchelewa kwa ponyo, au kushuka kwa mashaka, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَٱخْشَوْنِي وَلِأُتِمَّ نِعْمَتِي عَلَيْكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ﴾

{Basi msiwaogope wao, lakini niogopeni mimi – na ili nikutimizieni neema yangu, na ili mpate kuongoka} [Al-Baqarah: 150].

Mja ni dhaifu akitegemea nafsi yake, anahitajia msaada wa Mola wake Mlezi mwenye nguvu, na kwa kutaka msaada kwake Allah aliye mtukufu na aliye juu kunatosheleza kutokana na kutaka msaada kwa viumbe, na atakayefanya bidii kutekeleza analolitaka, kisha asiwe ni mwenye kutaka msaada kwa Allah na asiwe mwenye kumuhitajia Yeye katika kulipata analolihitaji; basi milango itafungwa mbele ya uso wake, na mapato yatakuwa na uzito mbele yake, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumwambia ibnu Abbaas Allah amridhie yeye na babake:

**«Ewe kijana! Mimi nakufundisha maneno, mhifadhi Allah Naye atakuhifadhi, mhifadhi Allah utamkuta mbele yako, unapoomba basi muombe Allah, na unapotaka msaada basi taka kutoka kwa Allah»**, imepokewa na Tirmidhi.

Na mzungukio wa dini uko juu ya kutaka msaada kwa Allah:

﴿إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ﴾

{Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada} [Al-Fatiha:4],

Na Mitume waliwaamrisha kaumu zao jambo hili:

﴿قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ ٱسْتَعِينُوا۟ بِٱللَّهِ وَٱصْبِرُوٓا۟﴾

{Musa akawaambia watu wake: Ombeni msaada kwa Allah, na subirini} [Al-A`raaf: 128],

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Dini ni asiabudiwe ila Allah, na kusitakwe msaada ila kwake".

Na kukamilika ukwasi wa mja ni katika kufungamana kwake na Mola wake Mlezi, na ni katika fadhila za Allah juu ya waja wake kuwa humsaidia anayefungamana Naye, na riziki huwa nyepesi kwa kumtii na kutaka msaada kwake, na huzidi kwa kumtegemea yeye na kunyenyekea kwake, [Allah] aliye takasika amesema:

﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجۡعَل لَّهُۥ مَخۡرَجٗا * وَيَرۡزُقۡهُ مِنۡ حَيۡثُ لَا يَحۡتَسِبُ﴾

{Na anaye mcha Allah humtengezea njia ya kutokea * Na humruzuku kwa jiha asiyotazamia} [At-Twalaaq: 2-3],

Maisha yamejaa maafa na machukivu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِي كَبَدٍ﴾

{Hakika tumemuumba mtu katika taabu} [Al-Balad:4],

Na kila kiumbe kina maadui katika majini na binadamu, na kiongozi wao akiwa ni ibilisi - laana za Allah zimshukie -; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّ ٱلشَّيۡطَٰنَ لَكُمۡ عَدُوّٞ فَٱتَّخِذُوهُ عَدُوًّا﴾

{Hakika shetani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui} [Faatwir:6],

Basi mja haachi kuwa muhitaji wa kutaka kinga kwa Allah, na kutaka kulindwa Naye, na kushikamana na himaya yake kutokana na shari.

Na Mola Mlezi amesifika na Ujabari na Ushindi; na atakaye shikamana naye basi hakuna mtu atamsibu na madhara, na madhara hayatamfika hata lau sababu zake zikiwepo; [Mtume] swala na salamu zimshukie amesema:

«**Atakayeshukia sehemu akasema: *'audhu bi kalimaati llaahi ttaammaati min sharri maa khalaq'*; hatadhuriwa na kitu hadi aondoke sehemu yake ile**», imepokewa na Muslim, Al-Qurtubi Allah amrehemu amesema: "Tangu nilipoisikia habari [hadithi] hii nimekuwa nikiifanyia kazi; basi sikudhuriwa na kitu hadi nilipoiacha, basi nikaumwa na nge siku moja nilipokuwa mji wa Al-Mahdiyyah, nakafikiria katika nafsi yangu, nikajipata kumbe nilisahau kujilinda na maneno hayo [aliyoyafundisha Mtume katika hadithi iliyotangulia]".

Na kiumbe huwa ni mwenye kupata maudhi, wala maisha yake hayawi mazuri ila kwa kushikamana na Allah na kujikinga naye, kwani madhara na manufaa yote yamo Mkononi mwake, na atakayefanya bidii kukudhuru basi halitatimia lengo lake iwapo Allah hajalitaka hilo; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**na jua ya kwamba lau umma mzima utakusanyika ili wakudhuru na kitu, hawatakudhuru na chochote ila kile alichokuandikia Allah**», imepokewa na Tirmidhi, na Allah alimwamrisha Nabii wake swala na salamu za Allah zimshukie ajilinde na Muumba wa asubuhi kutokana na shari za

viumbe vyote, na shari ya giza la usiku, na ya hasidi, na aliye mweza wa kuliondoa hili giza katika ulimwengu; ni mueza wa kumwondolea aliyejilinda naye anayoyaogopa, na mwenye kushikamana na Allah, mwenye kujilinda naye katika kila hali, huyo yumo ndani ya ngome imara [ya kumkinga] kutokana na wenye shari na vitimbi.

Hatuna pa kukimbilia katika mazito ila kwake Mola wetu Mlezi, wala hatuna pa kuelekea ili kujikinga naye ila kwake Yeye, na anayetaka uokozi kwa Allah na hifadhi yake huwa ametekeleza aina ya juu ya maombi, na kutaka uokozi kwa Mola Mlezi ndio jambo wanalolikimbilia Manabii na watu wema katika hali nzito na vitimbi, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِذۡ تَسۡتَغِيثُونَ رَبَّكُمۡ فَٱسۡتَجَابَ لَكُمۡ أَنِّي مُمِدُّكُم بِأَلۡفٖ مِّنَ ٱلۡمَلَٰٓئِكَةِ مُرۡدِفِينَ﴾

{Mulipokuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, naye akakujibuni kuwa: Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu wanao fuatana mfululizo} [Al-Anfaal:9].

Na [Allah] aliyetakasika amesema tena:

﴿أَمَّن يُجِيبُ ٱلۡمُضۡطَرَّ إِذَا دَعَاهُ﴾

{Au nani yule anayemjibu mwenye shida pale anapomwomba} [An-Naml: 62]

Atakayewaomba maiti basi maombi yake hayasikiwi, na mahitaji yake hayatanyanyuliwa; [Allah] aliyetakasika amesema tena:

﴿وَٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِهِۦ مَا يَمۡلِكُونَ مِن قِطۡمِيرٍ * 
إِن تَدۡعُوهُمۡ لَا يَسۡمَعُواْ دُعَآءَكُمۡ وَلَوۡ سَمِعُواْ مَا ٱسۡتَجَابُواْ لَكُمۡ﴾

{Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende * Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni} [Faatwir: 13-14],

Basi yanapokushukia mazito, na yakakulemea majanga, basi taka uokozi kwa Mjuzi wa ghaibu [Allah]:

﴿إِنَّمَآ أَمۡرُهُۥٓ إِذَآ أَرَادَ شَيۡـًٔا أَن يَقُولَ لَهُۥ كُن فَيَكُونُ﴾

{Hakika amri yake anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa} [Yaasin: 82].

Na kumpwekesha Allah kwa matendo ya waja ni usafi katika itikadi, na

ni saada yenye kuenea jamii, na ni utulivu ndani ya nafsi.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمُ ٱلَّذِى خَلَقَكُمۡ وَٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ۞

ٱلَّذِى جَعَلَ لَكُمُ ٱلۡأَرۡضَ فِرَٰشٗا وَٱلسَّمَآءَ بِنَآءٗ وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءٗ

فَأَخۡرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزۡقٗا لَّكُمۡۖ فَلَا تَجۡعَلُواْ لِلَّهِ أَندَادٗا وَأَنتُمۡ تَعۡلَمُونَ﴾

{Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu Mlezi aliyewaumba nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka * [Mola] ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyie Allah washirika, na hali nyinyi mnajua} [Al-Baqarah: 21-22].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Milango ya saada na heri inafunguliwa kwa kufungamana kwa moyo na Allah, na milango ya shari inafungwa kwa toba na istighfari, na afueni ya moyo iko katika kuacha maovu, na neema ya dunia imo katika kuvutika moyo kwa Allah kwa kumpenda, kumuogopa, na kutarajia fadhila zake, kwani hofu inakuepusha na kumuasi Allah, na matarajio yanakusukuma katika kumtii, na kumpenda kunakuvuta kwake, basi zifanye amali zako zote ni zenye kutakasiwa Allah, zenye kusimama kwa njia iliyo kamili zaidi kidhahiri na batini, pamoja na kuwa na yakini kuwa Allah anaona ya siri na niya, ni mwenye kuona na ni Mjuzi wa yaliyofichana.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## KUWA NA HOFU YA ALLAH[1].

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na kamateni Uislamu katika kishikio madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Matamanio yanapelekea katika kasoro na maasi, na shetani anamsukuma binadamu na kumhimiza kufanya makosa na kushiriki masanamu, na nafsi inapenda uzembe na penye utamu, wala hakuna wa kuzuia hatamu zake bila hofu ya Allah Mwenye ushindi na utukufu, na kuogopa adhabu yake.

Kuwa na hofu yake [Allah] aliyetakasika ndio nguzo kubwa ya ibada ambayo kwamba kuitakasa dini kwa Allah hakuwi barabara ila kwayo, nayo ni faradhi juu ya kila '*Mukallaf*' [mwenye akili aliyebalighi], na ni katika ibada za kimoyo kubwa zaidi; Allah amesema kumwambia Nabii wake Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie:

﴿قُلۡ إِنِّيٓ أَخَافُ إِنۡ عَصَيۡتُ رَبِّي عَذَابَ يَوۡمٍ عَظِيمٖ﴾

{Sema: Hakika mimi ninaogopa adhabu ya Siku Kubwa nikimuasi Mola wangu Mlezi} [Az-Zumar: 13], na Malaika wanamuogopa Mola wao Mlezi:

﴿وَلِلَّهِ يَسۡجُدُۤ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلۡأَرۡضِ مِن دَآبَّةٖ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَهُمۡ لَا يَسۡتَكۡبِرُونَ ۞ يَخَافُونَ رَبَّهُم مِّن فَوۡقِهِمۡ وَيَفۡعَلُونَ مَا يُؤۡمَرُونَ﴾

{Na vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi, tangu wanyama

1) [Hotuba hii] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na moja, mwezi wa Rabiul Akhir, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na saba, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

mpaka Malaika, vinamsujuidia Allah, na wala havitakabari * Vinamkhofu Mola wao Mlezi aliye juu yao, na vinafanya vinavyoamrishwa} [An-Nahl: 49-50].

Manabii waliwaogopea kaumu zao adhabu ya Allah; Nuuh [salamu zimshukie] alisema:

﴿إِنِّيٓ أَخَافُ عَلَيۡكُمۡ عَذَابَ يَوۡمٍ أَلِيمٖ﴾

{Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu} [Al-A'raaf: 59], na Shueib [salamu zimshukie] alisema:

﴿إِنِّيٓ أَرَىٰكُم بِخَيۡرٖ وَإِنِّيٓ أَخَافُ عَلَيۡكُمۡ عَذَابَ يَوۡمٖ مُّحِيطٖ﴾

{Mimi nakuoneni mmo katika hali njema, nami nakukhofieni adhabu ya Siku kubwa hiyo itakayo kuzungukeni} [Huud: 84], na Huud [salamu zimshukie] alisema:

﴿إِنِّيٓ أَخَافُ عَلَيۡكُمۡ عَذَابَ يَوۡمٍ أَلِيمٖ﴾

{Hakika mimi ninakukhofieni adhabu ya Siku iliyo kuu} [Ash-Shu'araa: 135], na Ibrahim [salamu zimshukie] alisema:

﴿يَٰٓأَبَتِ إِنِّيٓ أَخَافُ أَن يَمَسَّكَ عَذَابٞ مِّنَ ٱلرَّحۡمَٰنِ فَتَكُونَ لِلشَّيۡطَٰنِ وَلِيّٗا﴾

{Ewe baba yangu! Hakika mimi naogopa isikupate adhabu inayotoka kwa Mwingi wa Rehema ukaja kuwa mwenziwe shetani} [Maryam: 45], na watu wema wanawaogopea kaumu zao kushukiwa na adhabu duniani:

﴿وَقَالَ ٱلَّذِيٓ ءَامَنَ يَٰقَوۡمِ إِنِّيٓ أَخَافُ عَلَيۡكُم مِّثۡلَ يَوۡمِ ٱلۡأَحۡزَابِ﴾

{Na akasema yule aliyeamini: Enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni mfano wa siku za makundi} [Ghaafir: 30], na wanawaogopea adhabu ya Akhera:

﴿وَيَٰقَوۡمِ إِنِّيٓ أَخَافُ عَلَيۡكُمۡ يَوۡمَ ٱلتَّنَادِ﴾

{Na enyi watu wangu! Hakika mimi nakukhofieni Siku ya kuitana [Kiyama, watu wa Peponi na wa Motoni watakapoitana]} [Ghaafir: 32], wala hazingatii maonyo ila yule aliyehuishwa moyo wake na Allah kwa kuwa na hofu naye:

﴿وَتَرَكۡنَا فِيهَآ ءَايَةٗ لِّلَّذِينَ يَخَافُونَ ٱلۡعَذَابَ ٱلۡأَلِيمَ﴾

{Na tukaacha humo aya kwa ajili ya wanaoiogopa adhabu chungu} [Adh-Dhaariyaat: 37].

Mwenye kumuogopa Mola wake Mlezi hupewa utambuzi katika aya na mazingatio:

﴿إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَءَايَةٗ لِّمَنۡ خَافَ عَذَابَ ٱلۡأٓخِرَةِۚ﴾

{Hakika katika haya ipo aya kwa yule anayeogopa adhabu ya Akhera} [Huud: 103], na hunufaika na mawaidha ya Qur-ani na ukumbusho wake:

﴿فَذَكِّرۡ بِٱلۡقُرۡءَانِ مَن يَخَافُ وَعِيدِ﴾

{Basi mkumbushe kwa Qur-ani anayeliogopa onyo} [Qaaf: 45].

Allah huleta maonyo na alama ili nyoyo ziwe na hofu na zikimbilie kwake:

﴿وَمَا نُرۡسِلُ بِٱلۡأٓيَٰتِ إِلَّا تَخۡوِيفٗا﴾

{Nasi hatupeleki alama ila kwa ajili ya kuhofisha} [Al-Israa: 59], na mitihani yalio katika maagizo [maamrisho na makaazo] ni kwa ajili ya kudhihirisha cheo cha hofu ya Allah

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَيَبۡلُوَنَّكُمُ ٱللَّهُ بِشَيۡءٖ مِّنَ ٱلصَّيۡدِ تَنَالُهُۥٓ أَيۡدِيكُمۡ وَرِمَاحُكُمۡ لِيَعۡلَمَ ٱللَّهُ مَن يَخَافُهُۥ بِٱلۡغَيۡبِۚ﴾

{Enyi mulioamini! Allah atakujaribuni kidogo kwa wanyama wa kuwinda inayo wafikia mikono yenu na mikuki yenu, ili Allah amjue [amdhihirishe] nani anayemkhofu kwa ghaibu} [Al-Maidah: 94].

Nayo [hofu ya Allah] ni katika sifa tukufu zaidi za waja, na ni katika sababu za kupata mafanikio katika kauli na amali.

﴿قَالَ رَجُلَانِ مِنَ ٱلَّذِينَ يَخَافُونَ أَنۡعَمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِمَا ٱدۡخُلُواْ عَلَيۡهِمُ ٱلۡبَابَ فَإِذَا دَخَلۡتُمُوهُ فَإِنَّكُمۡ غَٰلِبُونَۚ﴾

{Watu wawili miongoni mwa wanaomhofu Allah ambao Allah amewaneemesha, walisema: Waingilieni kwa mlangoni. Mtakapo waingilia basi kwa yakini nyinyi mtashinda} Al-Maidah: 23], na [Allah] aliwakejeli makafiri kwa kukosa sifa hii,

﴿كَلَّاۖ بَل لَّا يَخَافُونَ ٱلۡأٓخِرَةَ﴾

{Hasha! Kwani wao hawaiogopi Akhera?} [Al-Muddaththir: 53].

Atakaye muogopa mola wake atapata amani wakati wa kifo

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسْتَقَٰمُواْ تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُواْ وَلَا تَحْزَنُواْ﴾

{Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Allah! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike} [Fusswilat: 30], na atakingwa na janga la siku ya kukusanywa [Kiyama].

﴿إِنَّا نَخَافُ مِن رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا * فَوَقَىٰهُمُ ٱللَّهُ شَرَّ ذَٰلِكَ ٱلْيَوْمِ وَلَقَّىٰهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا﴾

{Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu Mlezi hiyo siku yenye shida na taabu * Basi Allah atawalinda na shari ya siku hiyo, na atawakutanisha na raha na furaha} [Al-Insaan: 10-11], na Pepo itakuwa ni mashukio yake

﴿وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِۦ جَنَّتَانِ﴾

{Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi atapata Pepo mbili} [Ar-Rahmaan: 46].

Kwa kadri ya elimu ya kumjua Allah ndio inakuwa hofu ya kumuogopa Yeye, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Hakika mimi ni mjuzi wao zaidi kumjua Allah na ni mwenye hofu yake zaidi**» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na [Mtume] swala na salamu zimshukie alikuwa anapoona wingu au upepo rangi yake hubadilika, hutoka na kuingia, na huja akirudi; anaogopa isije kuwa ni adhabu.

Na pindi hofu inapojaa moyoni huizuia na maasi,

﴿لَئِنۢ بَسَطتَ إِلَيَّ يَدَكَ لِتَقْتُلَنِى مَآ أَنَا۠ بِبَاسِطٍ يَدِىَ إِلَيْكَ لِأَقْتُلَكَ ۖ إِنِّىٓ أَخَافُ ٱللَّهَ رَبَّ ٱلْعَٰلَمِينَ﴾

{Ukininyooshea mkono wako kuniuwa, mimi sitakunyooshea mkono wangu kukuuwa. Hakika mimi namwogopa Allah, Mola wa walimwengu wote} [Al-Maidah: 28].

Hofu [ya Allah] ni daraja ya juu, nayo ni miongoni mwa misingi ya dini madhubuti, inamfanya muumini kuwa ni mwenye kukita kimisingi, matamanio ya nafsi hayamgeuzigeuzi wala tamaa hazimbadilishi, anatembea juu ya njia ya Allah akiiga amri ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Mche Allah popote ulipo**», imepokewa na Tirmidhi, na wamo kati ya watu waliokosa cheo hicho, basi wakanyimwa ladha ya ibada na mfumo wao wa kimaisha ukatingisika, [Allah] aliyetakasika amesema kuwahusu:

﴿مُّذَبْذَبِينَ بَيْنَ ذَٰلِكَ لَآ إِلَىٰ هَٰٓؤُلَآءِ وَلَآ إِلَىٰ هَٰٓؤُلَآءِ﴾

{Wanayumbayumba baina ya huku na huko. Huku hawako na huko hawako} [An-Nisa: 143].

Kuondoka hofu ya Allah ni kufisidi kwa hali [ya mtu], ni uovu katika maisha, na ni giza la moyo; shubuha na matamanio yanauzunguka, Abu Suleiman Ad-Daaraani Allah amrehemu amesema: "Hofu haijawahi kuepuka moyo ila moyo huo huharibika", na haikuwa kugeuka kwa watu wa kufuru ila ni kwa sababu ya kutolewa hofu ya Allah katika vifua vyao, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿كَلَّاۖ بَل لَّا يَخَافُونَ ٱلۡأٓخِرَةَ﴾

{Hasha! Kwani wao hawaiogopi Akhera} [Al-Muddaththir: 53], na istizai ya wanafiki kuifanyia dini ya Allah, na shere zao katika hukumu zake [Allah] ni kutokana na nyoyo zao kukosa kumchunga Allah [kunako patikana kwa ajili ya hofu yake]:

﴿وَإِذَا لَقُواْ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قَالُوٓاْ ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوۡاْ إِلَىٰ شَيَٰطِينِهِمۡ قَالُوٓاْ إِنَّا مَعَكُمۡ إِنَّمَا نَحۡنُ مُسۡتَهۡزِءُونَ﴾

{Na wanapokutana na walioamini husema: Tumeamini. Na wanapokuwa peke yao na mashetani wao husema: Hakika sisi tu pamoja nanyi. Hakika sisi tunawadhihaki [waumini] tu} [Al-Baqara: 14].

Hajawahi kupotoka aliyepotoka miongoni mwa watu wa maasi ila kwa ajili ya upungufu wao katika cheo hiki [cha hofu ya Allah], na watu wema hawakukanya nafsi zao kutokana na matamanio ya haramu ila kwa ajili ya hofu kuzunguka nyoyo zao:

﴿ٱلَّذِي يَرَىٰكَ حِينَ تَقُومُ ۝ وَتَقَلُّبَكَ فِي ٱلسَّٰجِدِينَ﴾

{Ambaye anakuona unapo simama [katika swala ya usiku] * Na mageuko yako kati ya wanao sujudu} [Ash-Shu'araa: 218-219], na atakayemhofu Allah katika faragha Allah atamlipa kivuli cha chini ya Arshi yake [siku ya Kiyama]; «**Na mtu aliyeitwa na mwanamke mwenye cheo na urembo [ili afanye jimai naye]; basi akasema: Hakika mimi namuogopa Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Mtu aliye mwingi wa ibada na hofu akiwa faraghani, mwenye kutiririkwa na machozi kwa ukweli; ameahidiwa mfano wa hilo [kivuli chini Arshi], na mwenye bidii [ya ibada] katika giza la usiku, aliyeamshwa na hofu ya Allah; basi Allah akampa badala ya anayoyataka:

﴿تَتَجَافَىٰ جُنُوبُهُمۡ عَنِ ٱلۡمَضَاجِعِ يَدۡعُونَ رَبَّهُمۡ خَوۡفٗا وَطَمَعٗا وَمِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ يُنفِقُونَ ۝

فَلَا تَعۡلَمُ نَفۡسٞ مَّآ أُخۡفِيَ لَهُم مِّن قُرَّةِ أَعۡيُنٖ جَزَآءَۢ بِمَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ﴾

{Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku * wala nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho - ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda} [As-Sajda: 16], na muumini hukusanya ihsani na hofu, na mnafiki hukusanya uovu na kujiaminia.

**Enyi Waislamu**:

Kushambulia kwa Allah ni kukali, na ahadi yake ni hakika, na kuaminia kutokana na adhabu ya Allah na kutomchunga ni sababu ya uovu ya miji na watu. Kaumu za watu zilikeuka hofu ya Allah na zikafululiza katika maasi; basi Allah akawateremshia adhabu yake, na aliiangamiza kaumu ya Nuuh kwa kuwazamisha, na Thamuud kwa ukelele, na 'Aad kwa upepo mkali, na kaumu ya Shu'ayb kwa mtetemeko, ukelele na wingu liliojaa adhabu [badala ya maji], na akanyanyua kijiji cha kaumu Luut kwa ncha ya mbawa ya Malaika kisha akawatupa ardhini, na alinyanyua jabali kubwa juu ya vichwa vya wana wa Israili, akawaadhibu na mafuriko, akawatumia panzi, damu na chawa, na akawageuza baadhi yao nyani na nguruwe kwa ajili ya madhambi yao, na akalichoma bustani kubwa na matunda yake - kama ilivyobainishwa katika sura ya Al-Qalam - kwa ajili ya madhambi ya wamiliki wake,

﴿وَكَذَٰلِكَ أَخۡذُ رَبِّكَ إِذَآ أَخَذَ ٱلۡقُرَىٰ وَهِيَ ظَٰلِمَةٌۚ إِنَّ أَخۡذَهُۥٓ أَلِيمٞ شَدِيدٌ﴾

{Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola wako Mlezi anapoiadhibu miji inapokuwa imedhulumu. Hakika adhabu yake ni chungu na kali} [Huud: 102].

[Allah] aliyetakasika amemkemea na adhabu ya kudunisha mwenye kuaminia hofu katika zama zote na miji yote,

﴿أَفَأَمِنَ أَهۡلُ ٱلۡقُرَىٰٓ أَن يَأۡتِيَهُم بَأۡسُنَا بَيَٰتٗا وَهُمۡ نَآئِمُونَ ۝ أَوَأَمِنَ أَهۡلُ ٱلۡقُرَىٰٓ أَن يَأۡتِيَهُم بَأۡسُنَا ضُحٗى وَهُمۡ يَلۡعَبُونَ﴾

{Je, watu wa mijini wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafika usiku, nao wamelala? * Au watu wa mijini wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafika mchana, nao wanacheza?} [Al-A'raf: 97-98], na aliteremsha adhabu yake kwa watu ambao hawakumhofu; akamfanya dhalimu mwenye kiburi - Firauni - ni mfu usiotaharaki ukiwa baina ya mawimbi, na akamdidimiza [ardhini] Karuni - aliyekuwa na mali mingi na dhalimu - mwili wake na nyumba yake, na alimdidimiza mtu aliyekuwa akigogota nguo yake kwa kiburi, na Amr ibnu Luhay anagogota tumbo zake Motoni.

Allah anamkunjulia muda muasi wala hapuuzi, ndio hata akimchukua hatamponyoka:

﴿وَيُحَذِّرُكُمُ ٱللَّهُ نَفۡسَهُۥۗ﴾

{Na Allah anakuhadharisheni naye} [Aalu Imraan: 28].

[Allah] aliwaita watu kumwabudu na akawatahadharisha kumuasi na adhabu yake: kwani Yeye ni mkali wa kuadhibu, hawaridhii waja wake kufuru:

﴿إِن تَكۡفُرُواْ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنكُمۡۖ وَلَا يَرۡضَىٰ لِعِبَادِهِ ٱلۡكُفۡرَ﴾

{Mkikufuru basi Allah si mwenye haja nanyi, lakini hafurahii kufuru kwa waja wake} [Az-Zumar: 7], na amemkemea atakayeacha swala Jahanamu:

﴿مَا سَلَكَكُمۡ فِي سَقَرَ * قَالُواْ لَمۡ نَكُ مِنَ ٱلۡمُصَلِّينَ﴾

{Ni nini kilicho kupelekeni Motoni? * Waseme: Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakisali} [Al-Muddaththir: 42-43], na amemzunguka na uzito na taabu yule aliyewatendea wazazi wake wawili uovu:

﴿وَبَرَّۢا بِوَٰلِدَتِي وَلَمۡ يَجۡعَلۡنِي جَبَّارٗا شَقِيّٗا﴾

{Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu} [Maryam: 32], na imekurubia adhabu kuwaenea watu wote pindi watakapoacha kuamrisha mema na kukataza maovu, Naye Allah aliyetakasika ana ghera juu ya kuvunja mipaka ya haramu na heshima, «**Hakuna yeyote atakuwa na ghera zaidi kuliko Allah juu ya mja wake wa kiume au wa kike kuzini**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Amali hurudishwa kwa kula mali ya haramu; «**Hakika Allah ni Mzuri, hakubali ila kilicho kizuri**», na mja anaadhibiwa kwa kupokonywa utakatifu na utwahara wa nafsi yake kwa ajili ya kuliachilia jicho katika ya haramu:

﴿قُل لِّلۡمُؤۡمِنِينَ يَغُضُّواْ مِنۡ أَبۡصَٰرِهِمۡ وَيَحۡفَظُواْ فُرُوجَهُمۡۚ ذَٰلِكَ أَزۡكَىٰ لَهُمۡ﴾

{Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao} [An-Nuur: 30], na [Mtume] alitahadharisha kutokana na madhambi madogo; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Ewe Aisha! Chunga madhambi ya kudharaulika; kwani hakika yanayo mwenye kuyadai kutoka kwa Allah**», imepokewa na Ahmad.

Katika alama za ukweli wa mja kumhofu Allah: ni iwe faragha yake na dhahiri yake ni sawasawa, asiwe pindi amefichika na macho [ya watu] ni

mwenye maovu faraghani:

﴿وَهُوَ مَعَكُمۡ أَيۡنَ مَا كُنتُمۡۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعۡمَلُونَ بَصِيرٞ﴾

{Naye [Allah] yu pamoja nanyi popote mulipo. Na Allah ni Mwenye kuyaona mnayoyatenda} [Al-Hadiid: 4], na chunga makosa mafichoni kwani hayo ni yenye kuangamiza; Anas Allah amridhie amesema: "Hakika nyinyi mnafanya amali ambazo ni nyembamba katika macho yenu kuliko nywele, ingawa tulikuwa tukizizingatia katika zama za Mtume kuwa ni katika madhambi yenye kuangamiza", imepokewa na Bukhari.

Anayejiaminia kutokana na adhabu ya Allah ndiye aliyehasirika:

﴿أَفَأَمِنُواْ مَكۡرَ ٱللَّهِۚ فَلَا يَأۡمَنُ مَكۡرَ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡقَوۡمُ ٱلۡخَٰسِرُونَ﴾

{Je, wamejiaminisha na makri ya Allah? Kwani hawajiaminishi na makri ya Allah ila watu waliokhasirika} [Al-A'araaf: 99], na hakika kufuatana kwa neema juu ya mja pamoja na kufululiza kwake juu ya makosa ni kuvutwa kwake polepole; basi mja aogope adhabu yake [Allah].

Asiyeacha madhambi hazingatiwi ni mwenye kumhofu Allah, na kila mwenye kumuasi Allah huyo ana ujinga upande wa kumjua Allah, na kila anayemhofu Allah huyo ni mjuzi wa kumjua Allah, na kila mja akiwa ni mjuzi zaidi wa kumjua Allah atakuwa ni mwenye hofu yake zaidi; Ibnu Mas'uud Allah amridhie amesema: "Inatosha hofu ya Allah kuwa ni elimu, na inatosha kughurika na Allah kuwa ni ujinga", na upungufu wa hofu ya Allah unakuwa kwa sababu ya upungufu wa maarifa ya mja kumjua Mola wake, na kukumbuka yanayohofiwa kunazidi kwa kuugopa mwisho [wa matendo; yaani: malipo yake].

Ni miongoni mwa rehema za Allah kuwa Yeye hamkusanyii mja wake hofu mbili; basi atakayemhofu duniani atapata amani akhera, na aliyejiaminia makri yake duniani basi [Allah] atamtia hofu Akhera, na atakayemhofu Mola wake Mlezi ataisha baina ya waja akiwa adhimu, na katika maisha yake atakuwa azizi, na kumhofu kiumbe ni udhalilifu na unyonge Allah aliyetukuka amesema;

﴿إِنَّمَا ذَٰلِكُمُ ٱلشَّيۡطَٰنُ يُخَوِّفُ أَوۡلِيَآءَهُۥ فَلَا تَخَافُوهُمۡ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ﴾

{Hakika huyo ni shetani anawatia hofu marafiki zake, basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini} [Aalu Imraan: 175].

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿وَأَنِيبُوٓاْ إِلَىٰ رَبِّكُمۡ وَأَسۡلِمُواْ لَهُۥ مِن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَكُمُ ٱلۡعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ ۝ وَٱتَّبِعُوٓاْ أَحۡسَنَ مَآ أُنزِلَ إِلَيۡكُم مِّن رَّبِّكُم مِّن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَكُمُ ٱلۡعَذَابُ بَغۡتَةً وَأَنتُمۡ لَا تَشۡعُرُونَ﴾

{Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi, na silimuni kwake, kabla ya kukujieni adhabu, kisha hapo hamtanusuriwa * Na fuateni yaliyobora kabisa katika yale yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu Mlezi, kabla haijakujieni adhabu kwa ghafla, na hali hamtambui} [Az-Zumar: 54].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika, na nashuhudia ya kwamba Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, jamaa zake na masahaba wake.

Enyi Waislamu:

Hayajahifadhiwa mipaka ya Allah na aliyoyaharamisha, wala hawajafika kwake waliofika, na jambo mfano wa kumhofu Yeye, kumtarajia na kumpenda, na pindi moyo utakapokosa haya matatu; utafisidika, na pindi moja ya haya litadhuufika; itadhuufika imani yake kwa kiwango chake [cha kudhuufika hilo], na moyo ni mfano wa ndege katika kuenda kwake kwa Allah- basi mapenzi ndio kichwa chake, na hofu na matarajio ndio mbawa zake mbili-.

Na hofu inalazimu 'khashya' [haiba], na 'khashya' inalazimu utiifu, na matarajio yanamchunga mja katika mwendo wake kwa Allah, inamfanyia mwendo kuwa mzuri, inamuhimiza, na inampendekezea kudumu katika njia hiyo, na atakaye mwadhimisha Allah moyoni mwake, basi Allah humpa kuadhimishwa katika nyoyo za waja wala hawatomdhalilisha, Al-Fudhwail Allah amrehemu amesema: "Atakayemhofu Allah hatadhuriwa na yeyote, na atakayemhofu asiyekuwa Allah hatanufaishwa na yeyote".

Kujisalimisha kwa Allah na kutegemeza mambo kwake kutoa hofu ya watu moyoni, na atakayemhofu Mola wake Mlezi hatotishwa na yeyote; bali yeye ni mwenye moyo mtulivu na viumgo vilivotulia, basi jilazimisheni kumhofu Allah na mpeni Mola wenu Mlezi cheo apasacho; mtapata Saada duniani na Akhera.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# KUAMINI MALAIKA

## KUAMINI MALAIKA[1]

Sifa njema zote anastahiki Allah Muumba wa viumbe, Mjuzi wa yaliofichana, Mwenye kuona dhamiri na nia, namhimidi Yeye aliyetukuka kwa neema zake zenye kuandamana.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah pekee, hana mshirika naye, Mola mlezi wa ardhi na mbingu.

Na nashuhudia ya kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume wake, mwenye kuongoza katika njia iliyonyooka, na mwenye kulingania katika dini madhubuti.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani uchamngu ndio msingi wa kila kheri na kichwa cha kila bora, basi shikamaneni nayo katika dhahiri na mafichoni; mtafaulu siku ya maonyesho na malipo [Kiyama].

**Enyi Waislamu:**

Kuamini Malaika ni msingi kati ya misingi ya itikadi, haitimii Imani ila kwayo, nao [Malaika] ni katika ulimwengu ya ghaibu ambao ni wajibu kuiamini, na kuwasadikisha inawajibisha kuwaamini kwa ujumla sehemu ya ujumla, na kwa uchambuzi sehemu ya uchambuzi, na kuainisha sehemu ya kuainisha, kama ilivyokuja katika Kitabu kilicho azizi na Sunnah iliotwahirishwa.

[Allah] Mwenye ushindi na utukufu amewaumba kutokana na nuru, katika umbile zuri karimu na ukubwa katika umbo na uwezo wa kujibadilisha katika sura tofauti, hawali wala hawanywi, tabia zao na matendo yao ni twahara na ya ukamilifu, Allah amewapa maumbile ya kuwa na haya; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Hivi nisimwonee haya mtu ambaye Malaika wanamwonea haya?** -yaani: Uthmaan Allah amridhie-», imepokewa na Muslim.

Safu zao mbele ya Mola wao Mlezi ziko kwa nidhamu, hakika wao ni viumbe wakubwa miongoni mwa viumbe vya Allah; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Nimeidhinishwa niwahadithie kuhusu Malaika kati ya Malaika wa Allah aliyetukuka miongoni mwa**

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na tatu, mwezi wa Swafar, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na nne hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

**wanaobeba Arshi, hakika masafa yaliyo baina ya ndewe za masikio yake hadi begani kwake ni mwendo wa kutembea miaka mia saba**», imepokewa na Abu Daaud.

Mbora wao zaidi ni Jibrili [salamu zimshukie], ana mbawa mia sita, baina ya kila mbawa mbili ni kama baina ya mashariki na magharibi, kila mbawa miongoni mwazo imefunika upeo wa macho, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Nilimwona Jibrili katika *'Sidratul Muntahaa'*, anao mbawa mia sita, katika mabele yake mna tungo za nakshi za lulu na yakuti**», imepokewa na Ahmad. Allah alisema kumhusu:

﴿شَدِيدُ ٱلۡقُوَىٰ﴾

{Aliye mwingi wa nguvu} [An-Najm: 5], mwenye umbile zuri na kung'ara, ana nguvu na ukali sana, na ana cheo cha juu mbele ya Allah, anateremka kwa Mitume na habari za ukweli na sheria za uadilifu, alipigana vita pamoja na Nabii swala na salamu zimshukie katika vita vya Badr na Khandaq, na alisuhubiana naye katika [tukio la] Israa, na Allah anapompenda mja humnadi Jibrili: «**Hakika Mimi nampenda fulani; nawe mpende, basi na Jibrili naye ampende, kisha [Jibrili] anadi mbinguni: Hakika Allah anampenda fulani; nanyi mpendeni, basi watu wa mbinguni nao wampende, kisha awekewa kabuli katika ardhi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nao [Malaika] wamo ndani ya aina tofauti za ibada; wamo miongoni mwao wale wanaosimama milele kwa ajili ya Allah, wanaorukuu milele, na wanaosujudu milele, na miongoni mwao ni wale walio ndani ya aina tofauti za ibada nyinginezo, Mola wako ni Mjuzi wazo:

﴿وَمَا مِنَّآ إِلَّا لَهُۥ مَقَامٞ مَّعۡلُومٞ﴾

{Na hapana katika sisi [Malaika] ila anapo mahali pake maalumu} [As-Swaaffaat: 164], [Mtume] swala na salamu zimshukie anasema: «**Mbingu imepiga kitunu, na ni hakika kwake ipige kitunu, hamna ndani sehemu ya kuweka vidole vinne ila juu yake yupo Malaika amesujudu**», imepokewa na Ahmad.

**Enyi Waislamu:**

Hakika Allah amemlinda binadamu, akamtukuza na akamkinga, na akalitegemeza hilo [la kumlinda] kwa viumbe vyake bora; Malaika wanaoshikiana zamu juu yake, walinzi wake wa usiku na walinzi wa mchana, wanamuhifadhi kutokana na amri ya Allah kwa amri ya Allah, na washikiana zamu juu yake Malaika wengine ili kuhifadhi amali zake, hatamki neno lolote

ila kuna mwenye kulichunga, ameandaliwa kwa kazi hiyo - analiandika -, haachi neno wala haraka ila anaiandika, basi yeye [binadamu] yupo baina ya Malaika wanne mchana, na wanne wengine usiku, na yupo Malaika aliyeakilishwa tone la manii, na [Malaika] mwenye kuandamana naye kwa ajili ya kumwongoa na kumuelekeza, na Malaika wa mauti atakayeitoa roho yake, nao katika majukumu yao hayo wapo karibu zaidi naye [binadamu] kuliko hata mshipa wake wa moyo, kwa kupatiwa uwezo wa hilo na Allah.

Idadi yao: Ni viumbe wingi, hawezi kuwahesabu ila aliyewaumba; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَمَا يَعۡلَمُ جُنُودَ رَبِّكَ إِلَّا هُوَ﴾

{Na hapana yeyote anayejua majeshi ya Mola wako Mlezi ila Yeye tu} [Al-Muddaththir: 31], na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema kuhusiana na Nyumba iliyoimarishwa [Al-Baytul Ma'muur] iliyo katika mbingu ya saba: «**Waingia ndani yake kila siku Malaika elfu sabiini, si wenye kuirudia tena kabisa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, Allah ameteua miongoni mwao wenye kuibeba Arshi, na miongoni mwao ni Malaika waliokurubishwa kwake [Allah], na miongoni mwao ni walio katika mbingu ya saba, wanaiamirisha kwa ibada ya kudumu, wabora wao ni wale walioshuhudia vita vya Badr.

**Enyi Waislamu:**

Malaika wanawapenda watu wema na matendo ya watu wema; wanamuombea mwenye kufundisha watu kheri, na walio katika safu ya kwanza [katika swala], wanawahimiza waja juu ya kufanya kheri; basi «**Hakuna siku ambayo waja hupambauka ila kuna Malaika wawili hushuka. Mmoja wao husema: 'Ewe Allah, mpe badala yule anayetoa [katika njia yako],' na mwingine husema: 'Ewe Allah, mpe uharibifu yule anayezuilia [kutoa].'**», wanawaombea na kuwatakia msamaha Waumini, bali wanaobeba Arshi na walio kingizoni mwa Arshi wanamtakia msamaha muumini aliyetubu hususan, na wanamuombea kusalimika na Moto, kuingia Peponi na kuhifadhiwa kutokana na madhambi, na wanaitikia amiin Dua ya muumini anapomuombea nduguye kwa ghaibu, na wanamwambia: «**Nawe upate mfano wake**».

Wanashuka pamoja na kushukapo baraka na rehema, wanashuka katika usiku wa cheo [Laylatul qadr], na wanashuka pindi Qur-ani inaposomwa, wanazunguka vikao vya dhikri [vya elimu ya sheria], na wanawazunguka [walio katika vikao vya dhikri] kwa mbawa zao hadi kufika mbingu ya karibu, na wanaweka mbawa zao chini kwa unyenyekevu kwa ajili ya mwanafunzi wa elimu [ya sheria] ili kuonyesha kuridhia anayoyafanya.

Mnao katika kutukurubia kwao kheri na utukufu, hakika Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa mtoaji sana katika watu, na alikuwa mtoaji zaidi pindi anapokutana naye Jibrili. Na watu wema wanaposimamiwa na mauti [Malaika] wanawathibitisha na wanawabashiria Pepo, na wanawatoa roho zao kiwepesi, na Malaika wanawaingilia kupitia milango yote wakiwapa bishara ya kuingia Peponi, na Malaika wanawajia kimakundi wakiwasalimia na kuwabashiria kwa waliopata kutoka kwa Allah miongoni mwa kukurubishwa, kuneemeshwa na kuishi katika nyumba ya salama jirani na Manabii na Mitume wakarimu.

Pamoja na mapenzi yao ya watu wema wao wanamchukia muasi na wasusia maasia; basi hawaingii nyumba ambayo ndani yake mna picha wala jibwa wala sanamu, na wanaudhika na yale wanayoudhika nayo binadamu - miongoni mwa harufu ya kuchukiza -, wanawalani makafiri; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَمَاتُواْ وَهُمۡ كُفَّارٌ أُوْلَٰٓئِكَ عَلَيۡهِمۡ لَعۡنَةُ ٱللَّهِ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلنَّاسِ أَجۡمَعِينَ﴾

{Hakika walio kufuru na wakafa hali ni makafiri, hao iko juu yao laana ya Allah na ya Malaika na ya watu wote} [Al-Baqarah: 161], na pindi ajali yao [Makafiri] itakapokurubia wanawabashiria adhabu, maangamivu, Jahimu na kinywaji kimoto, basi roho zao zienee ndani ya miili yao na zikatae kutoka, basi Malaika wawapige katika nyuso zao na nyuma kwao na wawaambie:

﴿أَخۡرِجُوٓاْ أَنفُسَكُمُۖ ٱلۡيَوۡمَ تُجۡزَوۡنَ عَذَابَ ٱلۡهُونِ بِمَا كُنتُمۡ تَقُولُونَ عَلَى ٱللَّهِ غَيۡرَ ٱلۡحَقِّ
وَكُنتُمۡ عَنۡ ءَايَٰتِهِۦ تَسۡتَكۡبِرُونَ﴾

{Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya muliyokuwa mkiyasema juu ya Allah yasiyo ya haki, na mulivyokuwa mkizifanyia kiburi aya zake} [Al-An'aam: 93].

**Enyi Waislamu:**

Malaika ni waja waliokirimiwa [na Allah], wako katika daraja za juu na vyeo vitukufu, nao wako katika upeo wa utiifu kwa Mola wao Mlezi kikauli na kimatendo:

﴿لَا يَسۡبِقُونَهُۥ بِٱلۡقَوۡلِ وَهُم بِأَمۡرِهِۦ يَعۡمَلُونَ﴾

{Hawamtangulii [Mola wao Mlezi] kwa neno, nao wanafanya amri zake} [Al-Anbiyaa: 27], hawatangulii mbele ya amri yake, wala hawamhalifu katika aliyoamrisha, wala hawafanyi kiburi kuacha kumwabudu wala hawachoki:

﴿يُسَبِّحُونَ ٱلَّيۡلَ وَٱلنَّهَارَ لَا يَفۡتُرُونَ﴾

{Wanamtakasa usiku na mchana, wala hawanyong'onyei} [Al-Anbiyaa: 20], ni wenye kudumu katika amali usiku na mchana, wenye kutii kimakusudio na kimatendo, na «**pindi Allah atapitisha jambo mbinguni, Malaika wanapiga mbawa zao kunyenyekea kauli yake, kana kwamba ni sauti ya silisila ilipigwa juu ya jiwe manga, inawapita hiyo [sauti]**», na «pindi Allah anapotaka kufunua amri huzungumza kwa wahyi, basi mbingu hufikwa na mtetemeko mkali, kwa hofu ya Allah, basi watu wa mbinguni wanaposikia hilo wanazimia, na wanaanguka kumsujudia Allah, basi Jibrili awe wa kwanza atakayenyanyua kichwa chake, na Allah amsemeshe kwa ufunuo wake yale anayoyataka», Allah amesema kuwahusu:

﴿وَمَا مِنَّآ إِلَّا لَهُۥ مَقَامٞ مَّعۡلُومٞ ❋ وَإِنَّا لَنَحۡنُ ٱلصَّآفُّونَ ❋ وَإِنَّا لَنَحۡنُ ٱلۡمُسَبِّحُونَ﴾

{Na hapana katika sisi ila anapo mahali pake maalumu * Na hakika bila ya shaka sisi ndio wajipangao safu * Na hakika sisi ndio wenye kusabihi kutakasa} [As-Swaaffaat: 164-167].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Ama baada ya haya, enyi Waislamu:**

Hakika pamoja na viumbe hawa wakubwa katika viumbe vya Allah cheo chao hakivuki ya kuwa wao ni waja wadhalilifu mbele ya Allah, si washirika katika ufalme, wala hawana kuendesha katika ulimwengu, na Allah alimuahidi Jahanamu yule atakayedai miongoni mwao haki ya kuabudiwa pasi na Yeye; [Allah] aliyetukuka na aliye juu amesema:

﴿وَمَن يَقُلْ مِنْهُمْ إِنِّيٓ إِلَٰهٌ مِّن دُونِهِۦ فَذَٰلِكَ نَجْزِيهِ جَهَنَّمَۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

{Na yeyote kati yao atakayesema: Mimi ni Mwabudiwa, badala yake, basi huyo tutamlipa malipo yake Jahanamu. Hivyo ndivyo tuwalipavyo wenye kudhulumu} [Al-Anbiyaa: 29].

Wakiwa Malaika - na wanao nguvu hizo [zilizotajwa hapo awali] - watetemeka na kuzimia wanaposikia maneno ya Allah kwa hofu yake na utishio, basi vipi aombwe mmoja wao kinyume na Allah?! Bali wasiokuwa wao miongoni mwa wasioweza chochote katika maiti na masanamu ni aula wasiombwe na wasiabudiwe, basi mambo yote yako mikononi mwa aliye Mmoja Mwenye kukahiri, na kila asiyekuwa Yeye ni kiumbe aliyeumbwa; hamiliki manufaa wala madhara.

Haya yaliotangulia, kwa hakika wako baadhi ya watu hawakutambua hekima ambayo kwa minajili yake wameumbwa, na hawakujikisi nafsi zao kiasi wanavyostahiki, na hawakutambua kukirimiwa na kutukuzwa kwao na Allah kwa kule kuchagua viumbe vyake bora ili wamlinde [binadamu], wamuhifadhi na wamsaidie, basi akaikabili [neema] hiyo kwa ukafiri, ufasiki na kuikanusha, na atakaye fanya kiburi katika kumwabudu Mola wake Mlezi na akakataa ila kushirikisha na kuasi, basi walio kwa Mola wako wanamsabihi usiku na mchanana wao hawachoki, na Allah ni mkwasi hawahitaji, hanufaishwi na utiifu wa mwenye kutii, wala hadhuriki na maasi ya mwenye kuasi.

Basi jitahidini - enyi waja wa Allah - katika kumtii Mola wenu Mlezi,

na waaminini Malaika wake, na kumbukeni kuwa wamo kati yao waja wenye kuwahifadhi nyinyi, wanawahifadhia matendo yenu na kauli zenu, na wanawaandikia katika nyaraka za matendo yenu [nyaraka] ambazo mtakabidhiwa siku ya Kiyama, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿فَأَمَّا مَنۡ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ بِيَمِينِهِۦ ❁ فَسَوۡفَ يُحَاسَبُ حِسَابٗا يَسِيرٗا ❁ وَيَنقَلِبُ إِلَىٰٓ أَهۡلِهِۦ مَسۡرُورٗا ❁
وَأَمَّا مَنۡ أُوتِيَ كِتَٰبَهُۥ وَرَآءَ ظَهۡرِهِۦ ❁ فَسَوۡفَ يَدۡعُواْ ثُبُورٗا ❁ وَيَصۡلَىٰ سَعِيرًا﴾

{Ama atakayepewa daftari lake kwa mkono wa kulia * Basi huyo atahesabiwa hesabu nyepesi * Na arudi kwa ahali zake na furaha * Na ama atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake * Basi huyo ataomba kuteketea * Na ataingia Motoni} [Al-Inshiqaaq: 7-12]

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake..

# KUAMINI VITABU

## QUR-ANI TUKUFU[1]

Sifa njema zote anastahiki Allah Mwenye kuwapa ushindi atakayemtii na kumcha Yeye, na Mwenye kumdhalilisha atakayepoteza amri yake na kumuasi, namhimidi Yeye himdi nyingi nzuri zenye baraka kama anavyopenda Mola wetu Mlezi na anavyoridhia.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah pekee, hana mshirika naye, hatuna Mola ila Yeye, wala hatumwabudu ila Yeye.

Na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, mlinganizi kwa Allah aliye mkweli zaidi, na ni kiumbe wa Allah mwenye nasaha zaidi kwa waja wa Allah. Ewe Allah mswalie na msalimie Yeye, jamaa zake, masahaba wake, na atakayefuata njia yake na akaandama uongofu wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na mtakasieni siri yenu na dhahiri yenu, na kimbilieni kwenye kumridhisha Mola wenu Mlezi, na patilizeni fadhila za mwezi wenu [huu mlio nao].

**Enyi Waislamu:**

Allah amemtumiliza Nabii wake Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie na Qur-ani iliyo kwa kiarabu yenye kubainisha, ikashangaza akili za mafasihi wa kiarabu, na ikawasimamishia hoja; wakakiri ubora wa ubainifu wake na uzuri wa maneno yake, Al-Waliid ibn Al-Mughiira: "Naapa kwa Allah, hakika [Qur-ani] iko na utamu, na inayo juu yake uzuri, iliyojaa maji kijani chini yake, na hawezi kusema [maneno] haya binadamu."

Allah amejalia katika giza la usiku kuna nuru yenye kung'ara, aya baada ya yengine:

﴿يَهۡدِي بِهِ ٱللَّهُ مَنِ ٱتَّبَعَ رِضۡوَٰنَهُۥ سُبُلَ ٱلسَّلَٰمِ﴾

{Allah huwaongoa nacho [kitabu hiki] wenye kufuata radhi yake katika njia za salama} [Al-Maidah: 16]. Imekusanya na kuhifadhi [ndani yake] katika kutibu nafsi, kutengeneza hali, na kuamsha nyoyo, hakika hiki [Kitabu] ni kamba ya Allah yenye nguvu, na nuru yenye kubainisha, ni kinga kwa atakayeshikamana nacho, na kusalimika kwa mwenye kukifuata, atakayesema kwacho atasema kweli, na atakayehukumu nacho atafanya

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na sita ya mwezi wa Ramadhani, mwaka elfu moja mia nne na ishirini hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

uadilifu, na atakaye kitendea kazi atapewa ujira. Majini walishangaa kutokana na maajabu yake:

﴿قُلۡ أُوحِيَ إِلَيَّ أَنَّهُ ٱسۡتَمَعَ نَفَرٞ مِّنَ ٱلۡجِنِّ فَقَالُوٓاْ إِنَّا سَمِعۡنَا قُرۡءَانًا عَجَبٗا ❁
يَهۡدِيٓ إِلَى ٱلرُّشۡدِ فَـَٔامَنَّا بِهِۦۖ وَلَن نُّشۡرِكَ بِرَبِّنَآ أَحَدٗا﴾

{Sema: Imefunuliwa kwangu ya kuwa kundi moja la majini lilisikiliza, na likasema: Hakika sisi tumeisikia Qur-ani ya ajabu! * Inaongoza kwenye uongofu, kwa hivyo tumeiamini, wala hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu Mlezi} [Al-Jinn: 1-2].

**Enyi Waislamu:**

Kwa kuisoma Qur-ani na kuitendea kazi daraja inanyanyuka na cheo kinakuwa, Abu Dharr Allah amridhie anasema: «Nilisema: Ewe Mtume wa Allah! Nipe wasia, [Mtume] akasema: **Shikamana na kusoma Qur-ani na kumdhukuru Allah; kwani hayo ni nuru yako ardhini, na ni akiba yako mbinguni**», imepokewa na ibnu Hibbaan, na mtu bora zaidi ni atakayejifunza [Qur-ani] na akaifundisha, Abu Abdulrahman As-Sulami Allah amrehemu alikaa miaka arubaini akisomesha Kitabu cha Allah ili kutaka kheri.

Kwa ajili ya [kikao cha] kujifunza Qur-ani na kuisoma utulivu unashuka, rehema zinatanda, na malaika wanawazunguka, na mjuzi wa kuisoma yuko pamoja na Malaika watukufu waliowema, kuisoma ni katika ibada bora zaidi, kila herufi moja yake ni jema linalolipwa maradufu, na cheo cha mwenye kuisoma Akhera kitakuwa katika aya ya mwisho aliyoisoma duniani, kujifunza [kitabu hiki] ni bora kuliko kukusanya mali na mapato; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Ni nani kati yenu anapenda kuenda [bonde la] 'But-haan' - au 'Al-Aqiiq' - kila siku ili arudi na ngamia wawili wenye nundu kubwa bila ya kupata dhambi, wala kukata kizazi? Tukasema: Ewe Mtume wa Allah! Tunapenda hilo, akasema: "Basi si aende mmoja wenu msikitini ili ajue au asome aya mbili katika Kitabu cha Allah Mwenye ushindi na utukufu, hilo ni bora kwake kuliko ngamia wawili, na [aya] tatu ni bora kwake kuliko [ngamia] watatu, na nne kwake ni bora kuliko wanne, na [aya ni bora] kuliko idadi zake katika ngamia**», imepokewa na Muslim

**Enyi Waislamu:**

Hakika Qur-ani imefikia upeo katika balagha na ufasaha, wanastaajabu nao mabingwa wa balagha, na pia wanaifahamu jumla ya watu wa kawaida. Basi ni kitabu gani [hiki] kinachoweza kukusanya fahamu za binadamu katika zama zenye kuandamana, pamoja na tofauti zilizoko katika fahamu zao,

sehemu zao, lugha zao, na tofauti za maarifa yao?! Pindi Uqbah ibnu Rabi'a alipoisikia [Qur-ani kwa mara ya kwanza] alisema: "Naapa kwa Allah, katu sijasikia mfano wake, naapa kwa Allah hiyo [Qur-ani] si mashairi wala ukuhani», na pindi washirikina walipotaka miujiza ya kihisi kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie - miongoni mwa kupasua mito ardhini na kuangusha mbingu -; ikawajia habari:

﴿أَوَلَمۡ يَكۡفِهِمۡ أَنَّآ أَنزَلۡنَا عَلَيۡكَ ٱلۡكِتَٰبَ يُتۡلَىٰ عَلَيۡهِمۡ﴾

{Je! Kwani hayakuwatosha ya kwamba tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa?} [Al-Ankabuut: 51].

Hakika hicho ni Kitabu kilichofanywa chepesi:

﴿وَلَقَدۡ يَسَّرۡنَا ٱلۡقُرۡءَانَ لِلذِّكۡرِ فَهَلۡ مِن مُّدَّكِرٖ﴾

{Na bila ya shaka Sisi tumeifanya Qur-ani iwe nyepesi kufahamika. Lakini yupo anayekumbuka?} [Al-Qamar: 17].

Pamoja na hilo, lau ingeteremka juu ya majabali ingeyapasua, au juu ya ardhi ingeikata vipande vipande.

Kuisoma ni ponyo ya nafsi kutokana na ladha [za haramu], na ni dawa ya nyoyo kutokana na matamanio na shubuha, na ni tiba ya miili kutokana na maradhi na maafa:

﴿وَنُنَزِّلُ مِنَ ٱلۡقُرۡءَانِ مَا هُوَ شِفَآءٞ وَرَحۡمَةٞ لِّلۡمُؤۡمِنِينَ﴾

{Na tunateremsha katika Qur-ani yaliyo na matibabu na rehema kwa waumini} [Al-Israa: 82].

**Enyi Waislamu**:

Hakika maneno mazuri zaidi ni Kitabu cha Allah, na hakika amefaulu yule ambaye Allah amekipamba [Kitabu hiki] ndani ya moyo wake, Al-Fudhwail ibnu Iyaadh Allah amrehemu anasema: "Aliyebeba Qur-ani amebeba bendera ya Uislamu, haimpasi kucheza na wanaocheza, wala kufanya upuuzi na wanaofanya upuuzi, wala haghafiliki na wenye kughafilika", na yamlazimu mwenye kukisoma [Kitabu hiki] ajipambe na ukweli, ikhlasi, na swala ya usiku, kwa kutekeleza dini na amana ya zile [neema] zilizoko mbavuni mwake.

Hutapata utamu wa saada hadi uwe juu ya kumtii Mola wako Mlezi, uwe mwenye kudumu kukisoma Kitabu cha Mola wako Mlezi, basi yatibu maradhi ya kuhalifu kwa toba, na [maradhi ya] mghafala kwa kurudi kwake, na shikamana na kamba ya Qur-ani katika hali ngumu; kwani kila kamba

isiokuwa hiyo ni mbovu, na jaalia ndani ya nyumba yako sehemu katika Qur-ani, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Mfano wa nyumba ambayo anadhukuriwa Allah ndani yake na nyumba ambayo hadhukuriwi Allah ndani yake; ni mfano wa aliyehai na aliyekufa**», imepokewa na Muslim.

Basi utie manukato ulimi wako kwa kukisoma na kuzingatia maana yake, na shikamana na uongofu wake na hukumu zake; utajishindia bishara ya duniani na akhera.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿كِتَٰبٌ أَنزَلۡنَٰهُ إِلَيۡكَ مُبَٰرَكٞ لِّيَدَّبَّرُوٓاْ ءَايَٰتِهِۦ وَلِيَتَذَكَّرَ أُوْلُواْ ٱلۡأَلۡبَٰبِ﴾

{Hiki Kitabu, tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie aya zake, na wawaidhike wenye akili} [Swaad: 29].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu**:

Hakika Kitabu cha Allah kinaleta pamoja kaumu tofauti, na raia mbali mbali chini ya bendera ya Uislamu na itikadi sahihi, kinaunganisha baina yao kwa kiungo cha imani na mashiko ya dini, na kinawafanya kuwa umma mmoja ulioshikana kinguvu, uliyo na kingo zilizojumuika, na safu zilizokaa pamoja:

﴿إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ﴾

{Hakika Waumini ni ndugu} [Al-Hujuraat: 10].

Pindi Waislamu watafanya kasoro katika kukitendea kazi Kitabu cha Mola wao Mlezi; udhaifu utawashukia, watanyenyekea udhalilifu, fitina zitawazunguka, wataenda katika udanganyifu wa maadui zao, watatia dosari upande wa *'al-Walaa'* na *'al-Baraa*' [nusra na uadui], watasadikisha mazingaombwe na makuhani, watamsikiliza anayedai kujua elimu ya ghaibu, na kujua kushuka kwa majanga na misiba namna karne zinavyosonga, wataambatana na sababu, na waghafilike na imani ya kuwa Allah ndiye mwenye hukumu, hakuwi kitu katika ufalme wake ila anayoyataka, basi ni haki kwa Mwislamu kuwa azizi na dini yake, na ashikamane na Kitabu cha Mola wake Mlezi, wala asifanye ulaini katika dini ya Allah, wala asigeukie sherehe za makafiri na misimu yao; kwani wao ni watu wa dini ya batili, na wamo ndani ya upotevu wa wazi kabisa, na wanazozizingatia kuwa idi basi ni wajibu kwa Mwislamu kuzikanusha kwa moyo wake na ulimi wake.

Tahadhari kuridhia au kuangalia matendo ya idi zao, kwani mnao katika kuona maovu ya mila zao: upungufu wa itikadi, upotevu wa nyoyo, na kuingia shubuha ndani ya nyoyo, na Allah anasema:

﴿وَدَّ كَثِيرٌ مِّنْ أَهْلِ ٱلْكِتَٰبِ لَوْ يَرُدُّونَكُم مِّنۢ بَعْدِ إِيمَٰنِكُمْ كُفَّارًا حَسَدًا مِّنْ عِندِ أَنفُسِهِم مِّنۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ ٱلْحَقُّ﴾

{Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau

wangewarudisha nyinyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa ajili ya uhasidi uliomo ndani ya nafsi zao, baada ya kwisha wapambanukia Haki} [Al-Baqarah: 109].

Basi ewe Mwislamu mhimidi Allah juu ya neema ya Uislamu; kwani hiyo ndio neema yenye cheo kikubwa zaidi, na ni yenye athari zaidi, na ifanye imani yako safi iliyotakaswa ikuangazie njia ya maisha yako, wala usifanye upungufu katika dini yako, wala usimuige adui yako; Mtume swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Nimeacha kati yenu mambo mawili ambayo hamtapotea mtaposhikamana nayo: Kitabu cha Allah na Sunnah ya Nabii wake**», imepokewa na Malik.

Waislamu wanao Kitabu cha Mola wao Mlezi, kilichohifadhiwa kutokana na kila mageuzo, kilichokusanya kheri ya duniani na Akhera, mnao ndani yake nuru na uongofu, nacho ndicho kinachomtoa mtu katika misiba na fitina; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿أَوَلَمْ يَكْفِهِمْ أَنَّآ أَنزَلْنَا عَلَيْكَ ٱلْكِتَٰبَ يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَرَحْمَةً وَذِكْرَىٰ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ﴾

{Je! Kwani hayakuwatosha ya kwamba tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa? Hakika katika hayo zipo rehema na mawaidha kwa watu wanaoamini} [Al-Ankabuut: 51].

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia aliyekuwa reheme iliyozawadiwa, na neema iliotolewa [kwa waja], Muhammad mwana wa Abdallah...

## UTUKUFU WA QUR-ANI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu**:

Mola wetu Mlezi aliyetakasika ni Mkamilifu katika dhati yake na sifa zake, hana mfano wake, sifa zake ndio zilizokamilika zaidi na nzuri zaidi, na ni katika sifa zake aliyetakasika: Kuzungumza; anazungumza wakati anaotaka, pindi anapotaka, kwa [maneno] anayoyataka, wala maneno yake hayana mwisho:

﴿قُل لَّوۡ كَانَ ٱلۡبَحۡرُ مِدَادٗا لِّكَلِمَٰتِ رَبِّي لَنَفِدَ ٱلۡبَحۡرُ قَبۡلَ أَن تَنفَدَ كَلِمَٰتُ رَبِّي وَلَوۡ جِئۡنَا بِمِثۡلِهِۦ مَدَدٗا﴾

{Sema: Lau kuwa bahari ndio wino wa [kuandikwa] maneno ya Mola wangu Mlezi, basi bahari ingeli malizika kabla ya kumalizika maneno ya Mola wangu Mlezi, hata tungeli ileta mfano wa hiyo kuongezea} [Al-Kahf: 109].

Mazungumzo yake ni mazuri zaidi, na ubora wa maneno yake juu ya maneno ya viumbe ni kama ubora wa Muumba juu ya viumbe, na neema zake aliyetakasika juu ya waja hazihesabiki.

Ni katika hekima ya Allah na rehema yake kwao: kuwa amewatumia Mitume wake, na akawateremshia vitabu vyake, akateremsha Taurati, Injili, Zaburi, Suhuf za Ibrahim na Musa, na akavihitimisha na Qur-ani Tukufu, yenye fadhila kubwa zaidi, na cheo kitukufu zaidi, [Allah] aliyetakasika

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na nne ya mwezi wa Rabiul Awwal, mwaka elfu moja mia nne na thelathini na saba hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

amejihimidi nafsi yake kwa kukiteremsha; akasema:

﴿ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ ٱلَّذِيٓ أَنزَلَ عَلَىٰ عَبۡدِهِ ٱلۡكِتَٰبَ وَلَمۡ يَجۡعَل لَّهُۥ عِوَجَاۜ﴾

{Himdi zote ni za Allah, ambaye amemteremshia mja wake Kitabu, wala hakukifanya kina upogo} [Al-Kahf: 1].

Na akaitukuza dhati yake ya juu kwa kukuteremsha; akasema:

﴿تَبَارَكَ ٱلَّذِي نَزَّلَ ٱلۡفُرۡقَانَ عَلَىٰ عَبۡدِهِۦ لِيَكُونَ لِلۡعَٰلَمِينَ نَذِيرًا﴾

{Ametukuka aliyeteremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote} [Al-Furqaan: 1].

Na akaapa nayo; akasema:

﴿يسٓ * وَٱلۡقُرۡءَانِ ٱلۡحَكِيمِ﴾

{Yaa - Siin * Kwa Haki ya Qur-ani yenye hekima!} [Yaa-Siin: 1-2],

Nayo ni miongoni mwa [vitu] alivyoviapia

﴿فَلَآ أُقۡسِمُ بِمَوَٰقِعِ ٱلنُّجُومِ * وَإِنَّهُۥ لَقَسَمٞ لَّوۡ تَعۡلَمُونَ عَظِيمٌ * إِنَّهُۥ لَقُرۡءَانٞ كَرِيمٞ﴾

{Basi naapa kwa mashukio ya nyota * Na hakika bila ya shaka hiki ni kiapo kikubwa, laiti mngelijua! * Hakika hii bila ya shaka ni Qur-ani Tukufu} [Al-Waaqi'a: 75-77].

Ni yenye kusadikisha vitabu vilivyo kabla yake, na ni yenye kuvihukumu, na yenye kufuta utendakazi wake, na ni yenye kuaminiwa juu ya yaliomo ndani yake.

Manabii walibashiria kuja kwake kabla hata kuteremka kwake

﴿وَإِنَّهُۥ لَفِي زُبُرِ ٱلۡأَوَّلِينَ﴾

{Na hakika bila ya shaka haya [utajo wa hii Qur-ani] yamo katika vitabu vya kale} [Ash-Shu'araa: 196].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "utajo wa hii Qur-ani na kuiadhimisha yamo ndani ya vitabu vya waliotangulia, vilivyopatikana kutoka kwa Manabii wao".

Na Ibrahim na Ismail waliomba Allah atumilize Nabii ili aisome [Qur-ani] na aifundishe; wakasema:

﴿رَبَّنَا وَٱبۡعَثۡ فِيهِمۡ رَسُولٗا مِّنۡهُمۡ يَتۡلُواْ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ﴾

{Ewe Mola wetu Mlezi! Waletee Mtume anayetokana na wao, awasomee aya zako, na awafundishe Kitabu na hikima na awatakase. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima} [Al-Baqarah: 129].

Qur-ani ni maneno ya Mola Mlezi wa walimwengu, amezungumza kwayo kiuhakika kwa herufi na sauti za kusikika, imeanza kutoka kwake na kwake itarudi mwisho wa zama, ameisikia kutoka kwa Allah Jibrili [salamu zimshukie] ambaye ndiye Malaika bora zaidi, na akateremka nayo kwa Mtume bora zaidi [akaifikisha] kwa kiungo bora zaidi cha mwilini - nacho ni moyo-; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿نَزَلَ بِهِ ٱلرُّوحُ ٱلۡأَمِينُ * عَلَىٰ قَلۡبِكَ لِتَكُونَ مِنَ ٱلۡمُنذِرِينَ﴾

{Amekiteremsha [Kitabu hiki] Roho mwaminifu * Juu ya moyo wako, ili uwe katika waonyaji} [Ash-Shu'araa: 193-194], katika sehemu ya ardhi bora zaidi, ndani ya mwezi bora zaidi, na ndani ya usiku mtukufu zaidi - Laylatul qadr -, kwa ummah bora zaidi, kwa lugha bora zaidi na yenye kukusanya zaidi.

Hiki ni Kitabu kisicholingana nacho kitabu chochote [kingine]:

﴿أَوَلَمۡ يَكۡفِهِمۡ أَنَّآ أَنزَلۡنَا عَلَيۡكَ ٱلۡكِتَٰبَ يُتۡلَىٰ عَلَيۡهِمۡ﴾

{Je! Kwani hayakuwatosha ya kwamba tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa?} [Al-Ankabuut: 51].

[Allah] aliyetakasika amejisifu na neema ya Kitabu hiki juu ya umma huu; akasema:

﴿لَقَدۡ مَنَّ ٱللَّهُ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ إِذۡ بَعَثَ فِيهِمۡ رَسُولٗا مِّنۡ أَنفُسِهِمۡ يَتۡلُواْ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمۡ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ﴾

{Hakika Allah amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyowaletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, anayewasomea aya zake, na anawatakasa, na anawafunza Kitabu na hikima} [Al-Imraan: 164], Kitabu hiki ni utukufu kwa Nabii huyu na kwa umma wake

﴿وَإِنَّهُۥ لَذِكۡرٞ لَّكَ وَلِقَوۡمِكَ﴾

{Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako} [Az-Zukhruf: 44], nacho ndio roho yake [umma huu], kule kuwa maisha ya hakika

yanakitegemea, na pindi mtu atakiepuka atakuwa hai bila uhai, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَكَذَٰلِكَ أَوۡحَيۡنَآ إِلَيۡكَ رُوحٗا مِّنۡ أَمۡرِنَا﴾

{Na namna hivi tumekufunulia roho [Qur-ani] kwa amri yetu} [Az-Zukhruf: 51].

Lau Allah angeiteremsha juu ya jabali basi lingemhofu na likapasuka kwa udhalilifu kwa Allah na utiifu.

Haisihi Imani ya mja hadi aiamini [Qur-ani] kwa ujumla na kwa uchambuzi, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ ءَامِنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَٱلۡكِتَٰبِ ٱلَّذِي نَزَّلَ عَلَىٰ رَسُولِهِۦ﴾

{Enyi mulioamini! Mwaminini Allah, na Mtume wake, na Kitabu alichokiteremsha juu ya Mtume wake} [An-Nisaa: 136].

Nacho kiko huko mbinguni:

﴿فِي صُحُفٖ مُّكَرَّمَةٖ * مَّرۡفُوعَةٖ مُّطَهَّرَةِۭ * بِأَيۡدِي سَفَرَةٖ﴾

{kimo katika kurasa zilizo hishimiwa * Zilizoinuliwa, zilizotakaswa * Zimo mikononi mwa Malaika waandishi} [Abasa: 13-15]. Nao ni malaika

﴿كِرَامِۭ بَرَرَةٖ﴾

{Watukufu, wema} [Abasa: 16].

Allah amekihifadhi kabla hata kukiteremsha; akasema:

﴿بَلۡ هُوَ قُرۡءَانٞ مَّجِيدٞ * فِي لَوۡحٖ مَّحۡفُوظِۭ﴾

{Bali hii ni Qur-ani tukufu * Katika Ubao Ulio Hifadhiwa} [Al-Buruuj: 21-22].

Na akaihifadhi kutokana na mashetani wakati wa kuiteremsha

﴿وَمَا تَنَزَّلَتۡ بِهِ ٱلشَّيَٰطِينُ * وَمَا يَنۢبَغِي لَهُمۡ وَمَا يَسۡتَطِيعُونَ﴾

{Wala Mashetani hawakuteremka nayo * Wala haitakiwi kwao, na wala hawawezi} [Ash-Shu'araa: 210-211], na akadhamini kuihifadhi baada ya kuteremka kwake:

﴿إِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا ٱلذِّكۡرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ﴾

{Hakika Sisi ndio tulioteremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio

tutaulinda} [Al-Hijr: 9].

Allah alitanguliza kuitaja mbele ya neema zake nyingi; akasema:

﴿ٱلرَّحۡمَٰنُ * عَلَّمَ ٱلۡقُرۡءَانَ﴾

{Ar-Rahmaan, Mwingi wa Rehema * Amefundisha Qur-ani} [Ar-Rahmaan: 1-2], Allah amewafundisha waja wake Qur-ani, na akaisahilisha kwao kuisoma, kuitekeleza na kuihifadhi, anaihifadhi muarabu na asiyekuwa muarabu, mkubwa na mdogo, mume na mke, na mkwasi na fakiri.

Yamekithiri majina yake na sifa zake. Allah ameijaalia kuwa uongofu na ukumbusho kwa walimwengu, ni yenye kuwaenea binadamu wote kama unavyoenea utume wa Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie, basi si mahususi kwa umma pasi na wengine. Inafanana baadhi yake kwa baadhi nyingine, na aya zake zinasadikisha aya zake nyingine:

﴿كِتَٰبٗا مُّتَشَٰبِهٗا مَّثَانِيَ﴾

{Kitabu chenye kufanana na kukaririwa} [Az-Zumar: 23].

Imesimama wima wala Allah hakuijaalia na jongo, hamna hitilafu ndani yake wala mgongano:

﴿وَلَوۡ كَانَ مِنۡ عِندِ غَيۡرِ ٱللَّهِ لَوَجَدُواْ فِيهِ ٱخۡتِلَٰفٗا كَثِيرٗا﴾

{Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Allah bila ya shaka wangeli kuta ndani yake hitilafu nyingi} [An-Nisaa: 82].

Nayo ndio maneno mazuri zaidi na bora zaidi:

﴿ٱللَّهُ نَزَّلَ أَحۡسَنَ ٱلۡحَدِيثِ﴾

{Allah ameteremsha maneno mazuri kabisa} [Az-Zumar: 23], An-Nawawi Allah amrehemu amesema: "ikajulisha ya kuwa hii [Qur-ani] ni maneno mazuri zaidi kuliko maneno yote yalioteremshwa [kutoka kwa Allah] na ambayo hayajateremshwa [yaani: maneno ya viumbe]."

Allah ameisifu na utukufu; akasema:

﴿وَلَقَدۡ ءَاتَيۡنَٰكَ سَبۡعٗا مِّنَ ٱلۡمَثَانِي وَٱلۡقُرۡءَانَ ٱلۡعَظِيمَ﴾

{Na tumekupa aya saba zinazosomwa mara kwa mara, na Qur-ani tukufu} [Al-Hijr: 87].

Allah ameiandikia utukufu katika dhati yake na cheo chake; akasema:

﴿وَإِنَّهُۥ فِيٓ أُمِّ ٱلۡكِتَٰبِ لَدَيۡنَا لَعَلِيٌّ حَكِيمٌ﴾

{Na hakika hiyo [Qur-ani] imo katika asili ya maandiko yalioko kwetu, ni tukufu na yenye hekima} [Az-Zukhruf: 4].

Iko wazi katika matamshi yake na maana yake, na ina ubainifu wa mambo juu ya uwazi wake, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿هَٰذَا بَيَانٌ لِّلنَّاسِ وَهُدًى وَمَوْعِظَةٌ لِّلْمُتَّقِينَ﴾

{Hii ni bayana kwa watu wote, na ni uongofu, na mawaidha kwa wachamngu} [Aalu Imraan: 138].

Ibnu Mas'uud Allah amridhie amesema: "[Allah] ametubainishia ndani ya Qur-ani hii kila elimu na kila kitu".

Ni chenye hekima, mnao ndani yake hekima:

﴿تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ﴾

{Hizo ni aya za Kitabu chenye Hekima} [Luqmaan: 2].

Ni kikarimu mbele ya Allah, mnao ndani yake mambo makarimu ya hali ya juu, na kwacho mja hukirimiwa na huadhimishwa mbele ya Allah na mbele ya viumbe wake, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ﴾

{Hakika hii bila ya shaka ni Qur-ani Tukufu} [Al-Waaqi'a: 77].

Mnao ndani yake uongofu wa waja, na pamoja na uongofu mnao ndani yake rehema:

﴿هُدًى وَرَحْمَةً لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ﴾

{Uongofu na rehema kwa watu wenye kuamini} [Al-A'raf: 52].

Ni kinga kutokamana na upotevu kwa aliyeshikamana nacho; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Nimeacha kwenu ambayo endapo mtashikamana nayo hamtapotea: Kitabu cha Allah...**», imepokewa na Muslim.

Ni kitukufu, kimefikia daraja ya juu zaidi ya utukufu, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿ق ۚ وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ﴾

{Qaaf. Naapa kwa Qur-ani tukufu!} [Qaaf: 1].

Ni chenye ushindi, hakuna chochote chenye kukikurubia katika hilo, na

atakayekukikurubia atapata ushindi:

﴿وَإِنَّهُۥ لَكِتَٰبٌ عَزِيزٌ﴾

{Na hiki bila ya shaka ni Kitabu chenye ushindi [juu ya kila anayetaka kukibadili au kukikusudia na uovu]} [Fusswilat: 41].

Kitabu kilicho juu kisicho kurubiwa, chenye heri na manufaa mengi, na njia za baraka ndani yake ni nyingi, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَهَٰذَا كِتَٰبٌ أَنزَلۡنَٰهُ مُبَارَكٌ﴾

{Na hiki ni Kitabu tulichokiteremsha, kilichobarikiwa} [Al-An'aam: 92].

Atakayekisoma, akakifanyia kazi na akakinushuru katika sehemu mbalimbali atapata ushindi, na atapata amani na ukunjufu wa maisha, Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Ilipokuwa khilafa ya Uthmaan Allah amridhie, ufalme wa Uislamu ulikunjuka hadi mashariki na magharibi za ardhi za mbali, na hilo ni baraka za kusoma kwake, na kuidurusu [Qur-ani], na kuukusanya kwake umma juu ya kuihifadhi Qur-ani".

Kitabu cha Allah ni nuru katika maisha yenye kutambuza nuru ya duniani na Akhera; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قَدۡ جَآءَكُم مِّنَ ٱللَّهِ نُورٌ وَكِتَٰبٌ مُّبِينٌ﴾

{Bila shaka imekujieni kutoka kwa Allah nuru na Kitabu kinachobainisha} [Al-Maidah: 15].

Na kwacho roho zinapata uhai, kwani [Kitabu] hicho ni uhai kwa aliyekiitikia:

﴿ٱسۡتَجِيبُواْ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمۡ لِمَا يُحۡيِيكُمۡ﴾

{Muitikieni Allah na Mtume anapokuitieni jambo la kukuhuisheni} [Al-Anfaal: 24].

Pamoja na kupatikana kwacho uhai wa roho, pia ni ponyo ya maradhi ya viwiliwili, «Katika zama za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie nge alimuuma mtu, basi akasomewa Suratul Faatiha; akapona», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nacho ni mawaidha na chenye kupatia moyo imara wakati wa fitina, misiba na mazito:

﴿كَذَٰلِكَ لِنُثَبِّتَ بِهِۦ فُؤَادَكَ﴾

{Hivyo [kuteremsha Qur-ani sehemu sehemu] ni ili tuupe imara moyo wako} [Al-Furqaan: 32].

Neno la umma linajumuika kwa Qur-ani, na hitilafu zaondoka:

﴿وَٱعۡتَصِمُواْ بِحَبۡلِ ٱللَّهِ جَمِيعٗا وَلَا تَفَرَّقُواْ﴾

{Na shikamaneni na kamba ya Allah nyote pamoja, wala msifarikiane} [Aalu-Imraan: 103].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "nayo Qur-ani ni kamili kisura na kimaana", aya zake ni imara katika matamshi yake, na zenye ufafanuzi katika maana yake:

﴿كِتَٰبٌ أُحۡكِمَتۡ ءَايَٰتُهُۥ ثُمَّ فُصِّلَتۡ مِن لَّدُنۡ حَكِيمٍ خَبِيرٍ﴾

{Hiki ni Kitabu ambacho aya zake zimetiwa imara, kisha zikapambanuliwa, kilichotoka kwa Mwenye Hekima na Mjuzi} [Huud: 1].

Aliwapa changamoto nayo waliotangulia na watakaokuja, binadamu na majini miongoni mwao; akasema:

﴿قُل لَّئِنِ ٱجۡتَمَعَتِ ٱلۡإِنسُ وَٱلۡجِنُّ عَلَىٰٓ أَن يَأۡتُواْ بِمِثۡلِ هَٰذَا ٱلۡقُرۡءَانِ لَا يَأۡتُونَ بِمِثۡلِهِۦ
وَلَوۡ كَانَ بَعۡضُهُمۡ لِبَعۡضٖ ظَهِيرٗا﴾

{Sema: Wangelikusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur-ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao} [Al-Israa: 88].

Hajawahi kuisikia mwenye akili ila hushuhudia kuwa ni haki, majini waliisikia wakaambiana baadhi yao kwa baadhi: "Nyamazeni", na wakarudi kwa jamaa zao wakisema:

﴿إِنَّا سَمِعۡنَا قُرۡءَانًا عَجَبٗا﴾

{Hakika sisi tumeisikia Qur-ani ya ajabu!} [Al-Jinn: 1].

Ni dhikri iliyobora zaidi, kuisoma kunazidisha Imani:

﴿إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتۡ قُلُوبُهُمۡ وَإِذَا تُلِيَتۡ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتُهُۥ زَادَتۡهُمۡ إِيمَٰنٗا﴾

{Hakika Waumini ni wale ambao anapotajwa Allah nyoyo zao hujaa

hofu, na wanaposomewa aya zake huwazidisha Imani} [Al-Anfaal: 2].

Aya zake ziliwaliza watukufu; «Ibnu Mas'uud Allah amridhie alimsomea Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie 'Suratu An-Nisaa', alipofikia kauli yake [Allah]:

﴿فَكَيۡفَ إِذَا جِئۡنَا مِن كُلِّ أُمَّةِۭ بِشَهِيدٖ وَجِئۡنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰٓؤُلَآءِ شَهِيدٗا﴾

{Basi itakuwaje pindi tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?} [An-Nisaa: 41], Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akamwambia: "**Yatosha**", asema [Ibnu Mas'uud]: Nikageuka, nikakuta macho yake yanabubujika machozi», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na «Abu Bakar Allah amridhie alikuwa anaposoma Qur-ani [anaposwalisha] inakurubia kwa aliyekuwa nyuma yake kutomsikia kwa ajili ya kulia».

Na «Ja'afar At-Twayyaar Allah amridhie alimsomea An-Najjaashi mwanzo wa suratu Maryam; akalia hadi ndevu zake zikatota [kwa machozi], na maaskofu wake [An-Najjaashi] wakalia hadi misahafu yao ikatota».

Na Allah aliamrisha kumpa hifadhi aliyetaka hifadhi katika makafiri ili apate kusikia Qur-ani; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَإِنۡ أَحَدٞ مِّنَ ٱلۡمُشۡرِكِينَ ٱسۡتَجَارَكَ فَأَجِرۡهُ حَتَّىٰ يَسۡمَعَ كَلَٰمَ ٱللَّهِ﴾

{Na ikiwa mmojawapo katika washirikina akikuomba ulinzi, basi mpe ulinzi apate kusikia maneno ya Allah} [At-Tawbah: 6].

[Qur-ani] imebeba miongoni mwa elimu zilizokusanya zaidi, na maarifa yalio na manufaa zaidi, watu wake wajuzi wa maana yake ndio wanazuoni wa hakika; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿بَلۡ هُوَ ءَايَٰتُۢ بَيِّنَٰتٞ فِي صُدُورِ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡعِلۡمَ﴾

{Bali hii [Qur-ani] ni aya zilizo wazi [zenye kubainisha] katika vifua vya waliopewa elimu} [Al-Ankabuut: 49].

Na mwalimu wa Qur-ani na mwanafunzi wake wao ndio watu bora zaidi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Mbora wenu ni yule anayejifunza Qur-ani na akaifundisha**», imepokewa na Bukhari.

Mnao ndani yake habari za ukweli zaidi, hoja na dalili zilizowazi zaidi, visa bora zaidi, hekima nzuri zaidi, balagha na ufasaha mzuri Zaidi. Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Mtungo wenyewe wa Qur-ani na mtindo

wake ni wa ajabu ulio mzuri mno, si katika jinsi ya mitindo ya maneno yanayojulikana, na hakuna yeyote aliyekuja na mfano wa mtindo huu, kwani hakika hiyo [Qur-ani] si jinsi ya ushairi, wala 'rajaz' [bahari ya ushairi ilionyepesi zaidi], wala hotuba, wala barua, wala utunzi wake si katika utunzi wa watu -waarabu wao na wasio waarabu-, na uwezo wake [unaokeuka uwezo wa kibinadamu] katika maana yake unashinda ule wa katika matamshi yake".

Ni Kitabu cha Allah kilichokusanya [kila kitu] katika hukumu zake, chenye uadilifu katika uamuzi wake, chenye hekima katika maamrisho yake na makatazo yake, kinacho utishio na utukufu, na kinacho nguvu, uwezo wakuathiri na uzuri, ni muujiza kwa maneno yake hata yakiwa machache, chenye kuongoza kwa hoja zake hata zikiwa chache, ni aya adhimu, na muujiza uliowazi, atakaye itendea kazi atalipwa thawabu, atakaye hukumu kwayo atafanya uadilifu, atakaye shikamana nayo atalindwa, na atakaye ifuata atarehemewa,

﴿فَٱتَّبِعُوهُ وَٱتَّقُواْ لَعَلَّكُمۡ تُرۡحَمُونَ﴾

{Basi kifuateni, na mchenimngu, ili mrehemewe} [Al-An'aam: 155].

Nayo ndio dhikri yenye manufaa zaidi na iliyokusanya zaidi, Allah aliwasifu wenye kuisoma na wenye kuitendea kazi, na akawaahidi malipo kamili na ziada; akasema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يَتۡلُونَ كِتَٰبَ ٱللَّهِ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنفَقُواْ مِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ سِرّٗا وَعَلَانِيَةٗ
يَرۡجُونَ تِجَٰرَةٗ لَّن تَبُورَ * لِيُوَفِّيَهُمۡ أُجُورَهُمۡ وَيَزِيدَهُم مِّن فَضۡلِهِۦٓۚ إِنَّهُۥ غَفُورٞ شَكُورٞ﴾

{Hakika wale wanaosoma Kitabu cha Allah, na wakashika swala, na wakatoa kwa siri na kwa dhahiri katika tulivyowaruzuku, hao watarajia biashara isiyobwaga * Ili Yeye awalipe ujira wao kwa ukamilifu, na awazidishie kutokana na fadhila zake} [Faatwir: 29-30].

Nayo ni biashara yenye faida yenye malipo maradufu, atakayesoma herufi yake moja itakuwa kwake ni jema, na jema [malipo yake] ni mara kumi yake, na kujifunza [Qur-ani] ni heri kuliko mali ya duniani; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Kwa nini asiende mmoja wenu msikitini ili ajue - yaani: ajifunze - au asome aya mbili katika Kitabu cha Allah hilo ni bora kuliko ngamia wawili, na [aya] tatu ni bora kwake kuliko [ngamia] watatu, na nne ni bora kwake kuliko wanne, na kuliko idadi yake katika ngamia**», imepokewa na Muslim.

Na «**Aliye mahiri wa kusoma Qur-ani yupamoja na Malaika wajumbe waliopewa heri na baraka nyingi, walio wema wa nyoyo na**

**matendo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Vikao vya Qur-ani na sehemu za kujifunza ni sehemu za kushuka utulivu na rehemu juu ya wenye kuifunza na wenye kujifunza; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Hawatokusanyika watu ndani ya nyumba kati ya nyumba za Allah, wakawa wanasoma Kitabu cha Allah, na wanafunzana baina yao, ila utulivu utawashukia, rehema zitawafunika, Malaika watawazunguka na Allah atawataja mbele ya walio kwake**», imepokewa na Muslim.

Na rehema zinapatikana kwa kuisikiliza; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَإِذَا قُرِئَ ٱلۡقُرۡءَانُ فَٱسۡتَمِعُواْ لَهُۥ وَأَنصِتُواْ لَعَلَّكُمۡ تُرۡحَمُونَ﴾

{Na isomwapo Qur-ani isikilizeni na mnyamaze ili mpate kurehemewa} [Al-A'raf: 204].

Kushikamana nayo na kuisoma ni wasia wa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kwa umma wake; Abdallah ibnu Abii Awfaa Allah amridhie aliulizwa kuhusiana na wasia wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, akasema: «Ameusia Kitabu cha Allah», wameafikiana Bukhari na Muslim, ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: "Makusidio ya kuusia Kitabu cha Allah ni: Kukihifadhi kihisia na kimaana; basi kikirimiwe, kilindwe, yafuatwe yaliomo ndani yake, kisomewe kwa daima, kujifunza na kukifundisha.

Aliyeibeba Qur-ani ni mkirimiwa maishani na baada ya kufariki; basi maishani: «**awaongoze watu katika swala yule aliyemjuzi zaidi wa kukisoma Kitabu cha Allah**», imepokewa na Muslim. Na baada ya kufa kwake: «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akikusanya wawili kati ya waliouliwa Uhud ndani ya nguo moja [sanda], kisha akisema**: Ni nani kati yao aliyehifadhi Qur-ani zaidi? Basi anapoashiriwa mmoja wao humtanguliza katika ufuko [wa kaburi]**», imepokewa na Bukhari, na watu wa Qur-ani ndiwo rafiki bora zaidi; "Wasomi wa Qur-ani ndio walikuwa watu wa vikao vyao Umar na wa washauri wake" imepokewa na Bukhari.

Nayo [Qur-ani] ni hoja [ya kuwatetea] watu wake siku ya Malipo, na ni mtetezi anayekubaliwa utetezi wake mbele ya Mola Mlezi wa walimwengu; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Someni Qur-ani; kwani itakuja siku ya Kiyama ikiwa ni yenye kwatetea watu wake**», imepokewa na Muslim.

Sahibu ya Qur-ani yupo katika daraja za juu ya Pepo ya neema, «**Sahibu ya Qur-ani ataambiwa: soma na unyanyuke, na soma kwa sauti**

**nzuri kama ulivokuwa ukisoma ulimwenguni, kwani mashukio yako yatakuwa katika aya ya mwisho utakayoisoma**», imepokewa na Abu Daaud.

**Na baada ya haya, enyi Waislamu:**

Basi kufurahi na Qur-ani tukufu na kuifunza ni katika vyeo vya juu zaidi, na hakuna yeyote asiyekihitajia Kitabu cha Allah, kwani Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie ni mkamilifu zaidi wa akili, na ukamilifu wa akili yake haukumwongoza katika usawa, na hakika si mengine kuongoka kwake ni kwa ajili ya Qur-ani; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قُلۡ إِن ضَلَلۡتُ فَإِنَّمَآ أَضِلُّ عَلَىٰ نَفۡسِيۖ وَإِنِ ٱهۡتَدَيۡتُ فَبِمَا يُوحِيٓ إِلَيَّ رَبِّيٓۚ﴾

{Sema: Ikiwa mimi nimepotea, basi nimepotea kwa kudhuru nafsi yangu mwenyewe. Na ikiwa nimeongoka, basi ni kwa sababu ya aliyonifunulia Mola wangu Mlezi} [Faatwir: 50], na mtu mwenye saada zaidi ni yule aliye karibu zaidi na Kitabu cha Allah, nacho ni [sababu ya] utukufu na ubwana kwa Waislamu, na ni kupata cheo na fahari kwa vizazi, na ni amani kwa jamii, na baraka juu yake, na mnao ndani yake pumbao, kunyanyuka, na radhi za Mola Mlezi wa walimwengu.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ قَدۡ جَآءَتۡكُم مَّوۡعِظَةٞ مِّن رَّبِّكُمۡ وَشِفَآءٞ لِّمَا فِي ٱلصُّدُورِ وَهُدٗى وَرَحۡمَةٞ لِّلۡمُؤۡمِنِينَ﴾

{Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na ponyo ya yaliyomo vifuani, na uongofu, na rehema kwa Waumini} [Yunus: 57].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Atakayefuata Qur-ani atapata uongofu, na atakayeipa mgongo atapotea katika maangamivu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَمَنِ ٱتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشۡقَىٰ * وَمَنۡ أَعۡرَضَ عَن ذِكۡرِي فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةٗ ضَنكٗا وَنَحۡشُرُهُۥ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ أَعۡمَىٰ﴾

{Basi atakayeufuata uongofu wangu, hatapotea wala hatataabika * Na atakayejiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu} [Twaaha: 123-124], wala hakuna njia ya uongofu bila yake [Qur-ani].

Aliyezuiliwa moyo wake kunufaika nayo basi hatapata kuongoka kwa chengine; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَبِأَيِّ حَدِيثِۭ بَعۡدَ ٱللَّهِ وَءَايَٰتِهِۦ يُؤۡمِنُونَ﴾

{Basi maneno gani watakayo yaamini baada ya Allah na aya zake?} [Al-Jaathiyah: 6].

Na kama vile Qur-ani inamnyanyua mtu aliyesuhubiana nayo basi [vilevile] inamporomosha asiyekuwa yeye [asiyekuwa mwenye kusuhubiana nayo], Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakika Allah anawanyanyua watu kwa Kitabu hiki na anawaporomosha kwacho wengine**», imepokewa na Muslim.

Maneno ya Allah ni azizi na matukufu, atakayekanusha herufi yake moja tu au akaifanyia shere; atakufuru, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قُلۡ أَبِٱللَّهِ وَءَايَٰتِهِۦ وَرَسُولِهِۦ كُنتُمۡ تَسۡتَهۡزِءُونَ * لَا تَعۡتَذِرُواْ قَدۡ كَفَرۡتُم بَعۡدَ إِيمَٰنِكُمۡ﴾

{Sema: Mulikuwa mkimfanyia maskhara Allah na aya zake na Mtume

wake? * Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu!} [At-Tawbah: 65-66].

Na hajawahi yeyote kufanyia shere Kitabu cha Allah, au watu wake, au mafunzo yake ila Allah humdhalilisha; basi inafaa kwa Mwislamu anusuru Kitabu cha Mola wake Mlezi, na aone ushindi kwacho, ili apate daraja za juu zaidi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake…

# KUAMINI MITUME

# MANABII NA MITUME[1]

Sifa njema zote anastahiki Allah aliyepwekeka na utukufu ujalali, aliyesifika na sifa za ukamilifu, aliyetakaswa kutokana na mifano, namhimidi Yeye aliyetakasika na namshukuru shukrani inayozidisha neema na kuihifadhi kutokana na kuondoka.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika naye, aliye mkubwa aliye juu.

Na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, mwenye sifa karimu na tukufu, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake, masahaba wake; walio masahaba bora na jamaa bora, na atakayewafuata kwa wema hadi siku ya marudio.

**Ama baada ya himdi hii**:

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - ipasavyo kumcha; kwani atakayemcha Mola wake Mlezi Yeye atamlinda, na atakayeelekea kwake basi atamsaidia na atamwongoza, na atakayemshukuru atamzidishia na amridhishe.

**Enyi Waislamu**:

Allah aliwatumiliza Mitume wake pindi kila kaumu ya watu walipotegemea kwenye magiza ya rai zao na batili ya upotevu wao, basi Allah akaongoza kwa ajili yao viumbe, na kupitia wao akaziweka wazi njia, wala hakuna njia ya kufikia saada na kufaulu ila kupitia mikononi mwao, wala radhi za Allah hazipatikani ila kwa kuwafuata wao.

Kuwaamini ni msingi miongoni mwa misingi ya Imani, tunawaamini kiujumla na kiufafanuzi.

Wamebeba mizani ya uadilifu, Allah amewataja manabii na mitume ishirini na tano katika Kitabu chake; Abu Dharr Allah amridhie amesema: «Nilisema: Ewe Mtume wa Allah! Mitume ni wangapi? Akasema: **Mia tatu na kitu mjumuiko mwingi**», imepokewa na Ahmad.

Msafara uliofungamana na uongofu na nuru, aliyetangulia miongoni mwao humbashiria aliyechelewa, na aliyechelewa humsadikisha aliyetangulia, wamepambika na ufasaha wa lugha yao na ibara zao za juu, na huruma, upole na rehema zao zilizo kamili juu ya kaumu zao. Nasaba zao ni

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na saba ya mwezi wa Rabiul Akhir, mwaka elfu moja mia nne na ishirini hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

karimu, na asili zao ni tukufu, Allah amewaumba katika upeo wa ukamilifu na uzuri:

﴿ٱللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُۥ﴾

{Allah ndiye Mjuzi kuliko wote kujua wapi anaweka ujumbe wake} [Al-An'aam: 124].

**Enyi Waislamu:**

Kuitakasa amali, nia yake na usawa wake ni msingi katika kukubaliwa ibada, na Mitume ndio watu wenye juhudi zaidi ya kuitekeleza ikhlasi kwa mwabudiwa ipasavyo:

﴿رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّآ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ﴾

{Ewe Mola Mlezi wetu! Tutakabalie! Hakika Wewe ndiye Msikizi Mjuzi} [Al-Baqarah: 127].

Na kuchuma mali ya halali kwa mlinganizi, na kuepuka kwake shubuhati na ya haramu ndio sababu ya kukubaliwa zinazotarajiwa zaidi, na zenye kufika zaidi katika nyoyo, ndio maana Manabii wamefanya bidii kuwa na machumo mazuri; akawa Daud [salamu zimshukie] hali ila kutokana na kazi ya mkono wake, na akawa Zakariya [salamu zimshukie] serumala, na hakuna Nabii ila alichunga mbuzi:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلرُّسُلُ كُلُوا۟ مِنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَٱعْمَلُوا۟ صَٰلِحًا﴾

{Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema} [Al-Muminuun: 51].

**Enyi Waislamu:**

Yaliyo mazuri katika matendo, kauli na tabia ndio uongofu wao [Mitume], na sheria walioiweka ndio mizani ambayo kwayo zinapimwa tabia na matendo, wao ndio watu walio na nyoyo njema zaidi, na wenye elimu iliyobobea zaidi, na wenye busara kunjufu zaidi.

Sifa zao ni nzuri na tabia zao ni tukufu; wenye kuwatenda wema wazazi wawili; Allah aliyetukuka amesema kuhusu Yahya [salamu zimshukie]:

﴿وَبَرًّۢا بِوَٰلِدَيْهِ وَلَمْ يَكُن جَبَّارًا عَصِيًّا﴾

{Na akawa mwema kwa wazazi wake, wala hakuwa jabari muasi} [Maryam: 14].

na wakweli katika kuweka ahadi:

﴿وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ إِسۡمَٰعِيلَۚ إِنَّهُۥ كَانَ صَادِقَ ٱلۡوَعۡدِ وَكَانَ رَسُولٗا نَّبِيّٗا﴾

{Na mtaje katika Kitabu [hiki, yaani: Qur-ani] Ismail. Bila ya shaka yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii} [Maryam: 54].

[Wenye] busara na upole:

﴿إِنَّ إِبۡرَٰهِيمَ لَحَلِيمٌ أَوَّٰهٞ مُّنِيبٞ﴾

{Hakika Ibrahim alikuwa mpole, ana huruma, na mwepesi wa kurejea kwa Allah} [Huud: 75].

Hayo yamezungukwa na ukarimu na utoaji; aliienda Ibrahim [salamu zimshukie] kwa ahli yake akaja na ndama aliyenona wa kuchoma na akamueka mbele ya wageni watatu. Vile vile mtu mmoja alimuomba Mtume swala na salamu za Allah zimshukie mali, naye akampa kikundi cha mbuzi waliojaza baina ya majabali mawili, heshima na kujichunga:

﴿وَلَقَدۡ رَٰوَدتُّهُۥ عَن نَّفۡسِهِۦ فَٱسۡتَعۡصَمَ﴾

{Na kweli mimi [mke wa mtawala wa Misri] nilimtaka [Yusuf salamu zimshukie] naye akakataa} [Yusuf: 32].

Kuhifadhi wema na kulipa mazuri ya wengine:

﴿قَالَ مَعَاذَ ٱللَّهِۖ إِنَّهُۥ رَبِّيٓ﴾ أي: سيدي: ﴿أَحۡسَنَ مَثۡوَايَ﴾

{Audhubillahi! Najikinga na Allah. Huyu bwana wangu [mtawala wa Misri] kaniweka maskani nzuri} [Yusuf: 23].

Wanawasamehe waliokosea na wanaofanya uadui:

﴿قَالَ لَا تَثۡرِيبَ عَلَيۡكُمُ ٱلۡيَوۡمَۖ يَغۡفِرُ ٱللَّهُ لَكُمۡۖ وَهُوَ أَرۡحَمُ ٱلرَّٰحِمِينَ﴾

{Akasema: Leo hapana lawama juu yenu. Allah atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu} [Yunus: 92].

Na Mtume swala na salamu zimshukie alisema kuwaambia viongozi wa makureshi pindi alipofutahi Makkah: «**Nendeni; kwani mumeachwa huru**».

Allah amewatofautisha na wengine kwa akili zilizotimia, fahamu zilizokamilika na elimu kunjufu:

﴿فَفَهَّمۡنَٰهَا سُلَيۡمَٰنَۚ وَكُلًّا ءَاتَيۡنَا حُكۡمٗا وَعِلۡمٗاۚ﴾

{Tukamfahamisha Suleiman. Na kila mmoja wao tulimpa hukumu na elimu} [Al-Ambiyaa: 79].

Unyenyekevu wao ni mwingi; mbora wao [Mtume Muhammad] swala na salamu za Allah zimshukie, alikuwa anakama mbuzi wake mwenyewe, anajihudumia nafsi yake, na anashona viatu vyake.

**Enyi Waislamu:**

Pepo haipatikani ila kwa subira:

﴿وَلَا يُلَقَّىٰهَآ إِلَّا ٱلصَّٰبِرُونَ﴾

{Lakini hawapewi wema huu ila wanao subiri} [Fusswilat: 35].

Na wakati mitihani yanapoparagana na hali kuwa ngumu wanajulikana wanaume [wa kweli] na inabainika Imani, na hakika Manabii [salamu ziwashukie] walikumbwa na majanga na mazito kutoka kwa waliowahalifu; waliwadharau, wakawakemea, wakawaudhi na wakapita mipaka katika kuwaudhi.

Muda ulikuwa mrefu na mjadala baina ya Nuuh [salamu zimshukie] na kaumu yake ulidumu miaka elfu kupungua hamsini, na, Luut [salamu zimshukie] alitumwa kwa kaumu waliokuwa wakikata njia [wavamizi wa misafara], wanamfanyia hiyana rafiki na wanafanya maovu katika vikao vyao, na Ayyuub [salamu zimshukie] ni mfano unaopigiwa katika subira; alitahiniwa katika mwili wake kwa aina tofauti za balaa, na maradhi yake yalikuwa marefu hadi wenye kukaa naye wakachukia, na akakosa wakumuguza; basi akazidi kusubiri, kuhimidi, kushukuru na kutarajia malipo [mbele ya Allah], na [makafiri] walimtoa damu [walimjuruhi] Nabii swala na salamu za Allah zimshukie katika vita vya Uhud, na wakamvunja meno yake ya mbele, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alifiliwa na watoto sita, moyo wake ukahuzunika na macho yake yakatokwa na machozi, na waliuliwa miongoni mwao [Manabii] waliouliwa, Allah amesema:

﴿وَيَقْتُلُونَ ٱلْأَنۢبِيَآءَ بِغَيْرِ حَقٍّ﴾

{Na wakiwauwa Manabii pasi na haki} [Aalu Imraan: 112].

Manabii ndio watu waliotahiniwa sana na wenye subira kubwa zaidi; [Mtume] swala na salamu zimshukie anasema: «**Watu waliotahiniwa zaidi ni: Manabii, kisha wanaofanana nao, kisha wanaofanana nao**», imepokewa na An-Nasai.

**Enyi Waislamu:**

Mja anapomtegemea Allah ipasavyo, na akategemeza amri yake kwake, na asitie upungufu katika visababu [njia za kufikia malengo zinazojuzu]; basi faraja itamjia kutoka mbinguni; *Al-Khaliil* [Ibrahim salamu zimshukie] aliwekwa katika mkono wa manati akiwa amefungwa mikono, kisha akarushwa motoni; basi hakuzidisha zaidi ya kusema:

﴿حَسْبُنَا ٱللَّهُ وَنِعْمَ ٱلْوَكِيلُ﴾

{Allah anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa} [Aalu Imraan: 173],

basi Allah akaujaalia kuwa baridi na salama, na Mtume wa Allah [Muhammad] swala na salamu za Allah zimshukie alihofishwa na wingi wa maadui na mijumuiko yao, akasema: «**Allah anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa**», basi Allah akafarakanisha mjumuiko wao na akabatilisha vitimbi vyao.

Kwa Dua, dhaifu hupata nguvu, mwenye huzuni hufurahika na kwayo hufunguliwa faraja; Ayyuub [salamu zimshukie] alimnadi Mola wake Mlezi:

﴿أَنِّي مَسَّنِيَ ٱلضُّرُّ وَأَنتَ أَرۡحَمُ ٱلرَّٰحِمِينَ﴾

{Akasema: Mimi yamenipata madhara. Na Wewe ndiye unayerehemu kuliko wote wanao rehemu} [Al-Anbiyaa: 83].

Basi Mola wake Mlezi akamuitikia akamwondolea madhara aliyokuwa nayo na akampatia watu wake [watoto walikuwa wamemfia] pamoja na mfano wao.

Na Zakariya [salamu zimshukie] alimnadi Mola wake Mlezi baada ya udhaifu wa mifupa kumfika na ajali yake kukurubia:

﴿رَبِّ لَا تَذَرۡنِي فَرۡدٗا وَأَنتَ خَيۡرُ ٱلۡوَٰرِثِينَ﴾

{Mola wangu Mlezi! Usiniache peke yangu, na Wewe ndiye Mbora wa wanaorithi} Al-Anbiyaa: 89], basi Mola wake Mlezi akamuitikia na akamzawadia Yahya [salamu zimshukie] na akamsilihishia mkewe.

**Enyi Waislamu:**

Kutimia kwa saada ni kusilihi kwa watoto; kwani wao ndio nasaba iliyosalia na umri wa pili. Pamoja na yaliyowafika Mitume wa Allah miongoni mwa mashaka na tabia mbaya za kaumu zao, hakika hayo hayakuwashughulisha na kuacha kupatia umuhimu jambo la kuwasilihisha watu wao, Ibrahim [salamu zimshukie] alimuita mwanawe Ismail [salamu zimshukie] ili wajenge pamoja nyumba tukufu [Kaaba] juu ya misingi yake, na Ismail [salamu zimshukie] alikuwa akiamrisha jamaa zake swala na zaka, na Zakariya na watu wa nyumba yake walikuwa wakimuomba Mola wao kwa kutaka mazuri yalio kwake na kuogopa adhabu yake, na walikuwa wanyenyekevu kwake.

**Enyi waja wa Allah:**

Wingi wa ibada ni dalili ya ukweli wa kuelekea kwa Allah, Ibrahim [salamu zimshukie] alikuwa ni mwenye kudumu na ibada, na Daaud [salamu zimshukie] alikuwa akifunga siku na kufungua siku, na Mtume wetu swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiswali usiku hadi miguu yake ikipasuka.

Basi ni juu ya Mwislamu kufuata uongofu wao, aige subira yao, na ajipambe na sifa zao nzuri ili aufikie msafara wao

﴿أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ هَدَى ٱللَّهُۖ فَبِهُدَىٰهُمُ ٱقۡتَدِهۡ﴾

{Hao ndio ambao Allah amewaongoza. Basi fuata uogofu wao} [Al-An'aam: 90].

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَ فَأُوْلَٰٓئِكَ مَعَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِم مِّنَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ وَٱلصِّدِّيقِينَ وَٱلشُّهَدَآءِ وَٱلصَّٰلِحِينَۚ وَحَسُنَ أُوْلَٰٓئِكَ رَفِيقٗا﴾

{Na wenye kumtii Allah na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Allah miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao} [An-Nisaa: 69].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Namhimidi Allah himdi kama anavyopenda na kuridhia Mola wetu Mlezi.

Na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika, ni zake sifa njema mwishoni na mwanzoni.

Na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, aliyetumilizwa na rehema na uogofu, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, jamaa zake, masahaba wake na kila atakayefuata uongofu wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Ufupisho wa ujumbe wa mbinguni ni: Kulingania katika kumwabudu Allah peke yake, hana mshirika naye, na kutupilia mbali vinavyoabudiwa kinyume naye; [Allah] Mwenye iza na utukufu amesema:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾

{Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu} [Al-Anbiyaa: 25].

Manabii hawanyanyuliwi zaidi ya cheo chao, wala hawateremshwi chini ya daraja yao, basi wao ni Mitume wa Allah na waja wake, hawakadhibishwi wala hawapelekewi chochote miongoni mwa aina za ibada; basi hawaombwi kinyume na Allah, wala hawatakwi msaada, wala hawatiliwi nadhiri, wala hawachinjiwi, wala haifai kuapa nao, wala haiombwi ponyo kutoka kwao.

Yanawafika yale yanayowafika binadamu; Ibrahim [salamu zimshukie] aliwaogopa wageni wake walipokataa kula chakula, na «**Nabii kati ya Manabii alitulia chini ya mti akaumwa na chungu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Na Nabii [Muhammad] swala na salamu za Allah zimshukie alisahau katika swala yake, na akasema: «**Hakika mimi mi binadamu; nasahau kama mnavyosahau, basi nikisahau nikumbusheni**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nao wanakula, wanakunywa na wanasikia njaa, wanakuwa wagonjwa na wanakufa, baba wa Manabii [Ibrahim] [salamu zimshukie] anasema:

﴿وَٱلَّذِي هُوَ يُطۡعِمُنِي وَيَسۡقِينِ ۞ وَإِذَا مَرِضۡتُ فَهُوَ يَشۡفِينِ ۞ وَٱلَّذِي يُمِيتُنِي ثُمَّ يُحۡيِينِ﴾

{Na ambaye ndiye ananilisha na kuninywesha * Na ninapougua ni Yeye

ndiye anayeniponesha * Na ambaye atanifisha, na kisha atanihuisha} [Ash-Shu'araa: 79-81].

Na Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie anasema kumwambia binti yake: «**Ewe Fatma binti Muhammad! Niombe katika mali yangu unachotaka, kwa Allah sikutoshelezi na chochote**», imepokewa na Bukhari.

Basi Allah aliyetakasika ndiye Mwenye kunufaisha na kudhuru, na amri ni yake Yeye peke yake; anatoa na ananyima, anahuisha na anafisha, [Allah] aliyetukuka anasema:

﴿وَإِن يَمْسَسْكَ ٱللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِن يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَآدَّ لِفَضْلِهِۦ ۚ
يُصِيبُ بِهِۦ مَن يَشَآءُ مِنْ عِبَادِهِۦ ۚ وَهُوَ ٱلْغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ﴾

{Na Allah akikufikishia madhara, basi hapana wa kukuondolea [madhara hayo] ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake. Huifikisha kwa amtakaye katika waja wake, na Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu} [Huud: 107].

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## HAKI ZA NABII SWALA NA SALAMU ZA ALLAH ZIMSHUKIE[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja Allah - kama ipasavyo kumcha, kwani neema ni katika kufuata uongofu, na uovu ni katika kuafiki matamanio.

**Enyi Waislamu**:

Vipawa vya Allah juu ya waja wake ni vikubwa, na neema zake kwao ni adhimu, na ni katika neema zake kubwa kule kuwatumiliza Mitume wawe wenye kumtambulisha [Yeye kwa waja], na wawe wenye kulingania katika Tawhidi yake, nao ndio ukati baina ya Allah na viumbe vyake katika amri yake na makatazo yake, nao ndio mabalozi baina yake [Allah] na waja wake, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَلَقَدۡ بَعَثۡنَا فِي كُلِّ أُمَّةٖ رَّسُولًا أَنِ ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَٱجۡتَنِبُواْ ٱلطَّٰغُوتَ﴾

{Na kwa hakika kwa kila umma tuliwatumia Mtume kwamba: Mwabuduni Allah, na muepukeni shetani} [An-Nahl: 36].

Wala hakuna njia ya kufikia saada katika dunia ila kupitia mikononi mwao, wala hakuna njia ya kujua kizuri na kibovu kwa ubainifu ila kwa upande wao, wala radhi za Allah hazipatikanwi kabisa ila kupitia njia yao, Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Utume ni jambo la dharura kwa waja, hawana budi nalo, na mahitaji yao kwa jambo hilo yanashinda mahitaji yao kwa kila kitu, na utume ni roho ya ulimwengu, nuru yake na uhai wake, wala hakuna kubaki kwa walimwengu ila zinapodumu athari za Mitume kati yao, na pindi athari za Mitume zitaisha katika ardhi, na zifutike kabisa; basi Allah atauharibu ulimwengu wa juu na wa chini na atasimamisha Kiyama."

Mbora wa Mitume ni Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe tatu ya mwezi wa Rabiul Akhir, mwaka elfu moja mia nne na thelathini na sita hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

zimshukie, na utukufu wa umma wake na ujuu wa cheo chake ni kwa ajili yake, Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Na hakika si mengine umma huu umepata ushindi kwa ajili ya Nabii wake Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie", na kwa ajili ya ubora wake ndio masahaba wake wamekuwa masahaba bora wa Nabii, na karne yake ndio karne bora zaidi, na haikufadhilishwa ila kwa ajili yake. Na kwa ajili ya fadhila za Allah juu yake ndio amekuwa Mtume mwenye wafuasi wengi zaidi siku ya Kiyama.

Allah amemchagua baina ya watu akawa bwana wa wanadamu, na Allah akamfanya mteule juu ya viumbe akawa mbora wao, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Hakika Allah amemchagua Kinana katika wana wa Ismail** [salamu zimshukie]**, na akamchagua Quraish kutoka kwa Kinana, na akawachagua katika Quraish banuu Hashim [wana wa Hashim], na akanichagua mimi katika banuu Hashim**», imepokewa na Muslim.

Allah alimwadhimisha akaapa na umri wake, na hakumnadi kwa jina lake ndani ya Kitabu chake kama vile Mitume wengine; bali hakumnadi ila kwa jina la unabii na utume. Allah alikikunjua kifua chake, akamsamehe madhambi yake, akanyanyua utajo wake, na Allah akachukua ahadi kutoka kwa Manabii kuwa watamwamini; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَإِذۡ أَخَذَ ٱللَّهُ مِيثَٰقَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ لَمَآ ءَاتَيۡتُكُم مِّن كِتَٰبٖ وَحِكۡمَةٖ ثُمَّ جَآءَكُمۡ رَسُولٞ مُّصَدِّقٞ لِّمَا مَعَكُمۡ لَتُؤۡمِنُنَّ بِهِۦ وَلَتَنصُرُنَّهُۥۚ قَالَ ءَأَقۡرَرۡتُمۡ وَأَخَذۡتُمۡ عَلَىٰ ذَٰلِكُمۡ إِصۡرِيۖ قَالُوٓاْ أَقۡرَرۡنَاۚ﴾

{Na pale Allah alipochukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hekima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha muliyonayo, ni juu yenu mumwamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekiri} [Aalu Imraan: 81].

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "Naye [Mtume Muhammad] ndio imamu mkubwa ambaye lau angepatikana katika zama zozote basi angekuwa ndiye anayewajibika kutiiwa, mwenye kutangulizwa mbele ya manabii wote; na kwa sababu hii ndio alikuwa imamu wao pale walipokusanyika katika Baytul Maqdis".

Allah alihitimisha kwaye unabii na utume:

﴿مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَآ أَحَدٖ مِّن رِّجَالِكُمۡ وَلَٰكِن رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّـۧنَۗ﴾

{Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Allah na Mwisho wa Manabii} [Al-Ahzaab: 40].

Na akaitimiza kwaye dini:

﴿ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ دِينَكُمۡ وَأَتۡمَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ نِعۡمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلۡإِسۡلَٰمَ دِينٗا﴾

{Leo nimekukamilishieni dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe ndiyo dini} [Al-Maidah: 3].

Allah alimtia nguvu kwa aya nyingi, akamteremshia kitabu bora zaidi, akaihifadhi dini yake na akaahidi kuinusuru.

Kumwamini yeye swala na salamu za Allah zimshukie, kumpenda na kumsadikisha ni msingi katika misingi ya dini. Kushuhudia utume wake kumeambatanishwa na kushuhudia upweke wa Allah, Allah amemtuma kwa waarabu na wasio waarabu, na binadamu na majini; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قُلۡ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنِّي رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيۡكُمۡ جَمِيعًا﴾

{Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote} [Al-A'raaf: 158].

Allah alimtuma kuwa ni rehema kwa walimwengu; wakanufaika kwa utume wake, na rehema yake kwa waumini ni mahususi; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَرَحۡمَةٞ لِّلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ﴾

{Naye ni rehema kwa wanaoamini miongoni mwenu} [At-Tawbah: 61].

Hajaacha kheri ila amewajulisha umma, wala shari ila amewatahadharisha nayo; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Kheri niliyonayo sitaihifadhi pasi na kuwafikishia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ambaye hatamwamini Nabii swala na salamu za Allah zimshukie na hatamfuata; Allah amemkemea na Moto, [Allah] Mwenye iza na utukufu amesema:

﴿وَمَن لَّمۡ يُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ فَإِنَّآ أَعۡتَدۡنَا لِلۡكَٰفِرِينَ سَعِيرٗا﴾

{Na asiyemwamini Allah na Mtume wake, basi kwa hakika Sisi tumewaandalia makafiri Moto mkali} [Al-Fat-h: 13].

Ni wajibu kwa watu wa Kitabu [mayahudi na manasara] kumwamini na kumfuata; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Muhammad ipo Mkononi mwake! Hatanisikia yeyote katika umma huu - myahudi wala mnasara -, kisha afariki bila ya kuamini niliotumwa nayo; ila atakuwa katika watu wa Motoni**», imepokewa na Muslim.

Wala watu hawakosi kuwa wahitaji wa kumwamini na kumtii Nabii swala na salamu za Allah zimshukie katika kila sehemu na wakati, usiku na mchana, safarini na mjini, kwa dhahiri na siri, kimakundi na kuipweke, Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Na wao ni wahitaji zaidi wa hilo kuliko chakula na kinywaji; bali kuliko hata pumzi, kwani wao pindi watakosa hilo basi Moto ndio malipo ya aliyemkadhibisha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na akakeuka kumtii."

Allah alitutakasa kupitia kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, na akatufundisha tusiokuwa tukiyajua; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿هُوَ ٱلَّذِى بَعَثَ فِى ٱلۡأُمِّيِّـۧنَ رَسُولًا مِّنۡهُمۡ يَتۡلُواْ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمۡ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ وَإِن كَانُواْ مِن قَبۡلُ لَفِى ضَلَٰلٍ مُّبِينٍ﴾

{Yeye ndiye aliyempeleka Mtume kwenye watu wasiojua kusoma, awasomee aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhahiri} [Al-Jumu'a: 2],

Ash-Shafi'iyu Allah amrehemu amesema: "Hatujakuwa na neema, si iliyodhihiri wala iliyofichika, ambayo kwayo tumepata hadhi duniani na Akhera, au kwayo tumekingwa na machukivu ndani ya sehemu hizo mbili au mojawapo, ila Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie ndiye sababu yake, mwenye kuongoza katika heri yake, na mwenye kuongoa kwenye uongofu wake."

Wala imani ya mja kumwamini Nabii swala na salamu za Allah zimshukie haitekelezeki ipasavyo ila kwa kumtii; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿مَّن يُطِعِ ٱلرَّسُولَ فَقَدۡ أَطَاعَ ٱللَّهَ﴾

{Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Allah} [An-Annisa: 80].

Allah ameamrisha kumtii ndani ya sehemu zaidi ya thelathini katika Qur-ani, na akaambatanisha kumtii Yeye [Allah] na kumtii yeye [Mtume], na akaambatanisha baina ya kumhalifu Yeye na kumhalifu mtume, atakayemtii atafaulu:

﴿وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدۡ فَازَ فَوۡزًا عَظِيمًا﴾

{Na anayemtii Allah na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa} [Al-Ahzaab: 71].

Sifa kubwa za uchamngu na iliosisitizwa zaidi na iliyo msingi wa

zilizosalia: ni kumpwekesha Allah kwa ibada, na kumpwekesha Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kwa kumwandama; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمۡ عَنۡهُ فَٱنتَهُواْ﴾

{Na anachowapa Mtume chukueni, na anachowakataza jiepusheni nacho} [Al-Hashr: 7].

Katika hilo mna uhai wa mja na saada yake; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسۡتَجِيبُواْ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمۡ لِمَا يُحۡيِيكُمۡ﴾

{Enyi mulioamini! Muitikieni Allah na Mtume anapowaita kwenye jambo la kuwapa uzima wa milele} [Al-Anfaal: 24].

Na fitina inakuwa katika kumhalifu yeye; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿فَلۡيَحۡذَرِ ٱلَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنۡ أَمۡرِهِۦٓ أَن تُصِيبَهُمۡ فِتۡنَةٌ أَوۡ يُصِيبَهُمۡ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾

{Basi watahadhari wanaokhalifu amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu} [An-Nuur: 63].

Atakayeshindana na Mtume Allah humdhalilisha; Allah aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يُحَآدُّونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ أُوْلَٰٓئِكَ فِي ٱلۡأَذَلِّينَ﴾

{Hakika wanaompinga Allah na Mtume wake, hao ndio miongoni mwa madhalili wa mwisho} [Al-Mujaadila: 20].

Na atakayeepuka sunnah yake amekemewa na kutengwa na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Atakayeepuka sunnah yangu; basi si katika mimi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Miongoni mwa haki zake swala na salamu za Allah zimshukie: ni asiabudiwe Allah ila kwa sheria aliokuja nayo, si kwa matamanio na uzushi, wala hakuna rai ya yeyote [inayozingatiwa] pamoja na kuwepo sunnah ambayo imewekwa na Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Yeyote atakayetenda amali aina yeyote, haina amri yetu; basi [amali] hiyo itakuwa ni yenye kurudishwa**», imepokewa na Muslim.

Kumpenda ni katika wajibu mkubwa wa dini, wala msingi wa mapenzi

hautoshi katika hili; bali ni wajibu yawe mapenzi yaliozidi mapenzi ya kuwapenda viumbe wote hata zaidi ya [kuipenda] nafsi; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hawi muumini mmoja wenu hadi niwe napendeza zaidi kwake kuliko mzazi wake, mwanawe, na watu wote kwa jumla**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, Wala mja hapati utamu wa imani ila kwa hilo; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Mambo matatu yeyote ambaye yatakuwa ndani yake atapata kwayo utamu wa imani: Yule ambaye atakuwa Allah na Mtume wake wanapendeza zaidi kwake kuliko wasiokuwa wao, na ampende mtu, hampendi kwa lolote ila kwa ajili ya Allah, na achukie kurudi katika ukafiri kama anavyochukia kutupwa ndani ya Moto**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Mapenzi ya ukweli yanadhihiri katika kumfuata; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ﴾

{Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Allah basi nifuateni mimi, Allah atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu} [Aalu Imraan: 31].

Aliyekuwa mkweli katika kumpenda [Mtume] atafufuliwa naye Akhera, mtu alikuja kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: «**Ewe Mtume wa Allah! Unasemaje kuhusu mtu aliyewapenda watu lakini hakuweza kuwa nao? Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: Mtu yuko pamoja na anaowapenda**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ni katika kumpenda: umfanyie nasiha kwa kumwamini na kuamini aliyokuja nayo, kushikilia kumtii, kuichagua sunnah yake, kunushuru elimu zake, kuadhimisha amri yake, kuwapenda vipenzi vyake, na kuwafanyia uadui maadui wake; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie amesema: «**Dini ni nasaha, tukasema: kwa nani? Akasema: kwa Allah, Malaika wake, Mtume wake, viongozi wa Waislamu na Waislamu kwa ujumla**», imepokewa na Muslim.

Kumwadhimisha na kumheshimu ni katika misingi ya Dini, na ni katika hekima za kutumilizwa yeye; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّآ أَرْسَلْنَٰكَ شَٰهِدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ۞
لِّتُؤْمِنُوا۟ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَتُعَزِّرُوهُ وَتُوَقِّرُوهُ وَتُسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا﴾

{Hakika tumekutuma wewe uwe shahidi, na mbashiri, na mwonyaji * Ili mumwamini Allah na Mtume wake, na mumsaidie, na mumhishimu, na

mumtakase asubuhi na jioni} [Al-Fat-h: 8-9].

Al-Huleimy Allah amrehemu amesema: "Haki za Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ni kuu, adhimu, tukufu, na lazima zaidi kwetu, na ni wajibu zaidi juu yetu kuliko haki za mabwana juu ya wamilikiwa wao, na za mababa juu ya wana wao; kwa sababu Allah aliyetukuka ametuokoa kwaye kutokana na Moto wa Akhera, na amezikinga kwaye roho zetu, miili yetu, heshima zetu, mali yetu, watu wetu na watoto wetu hapa duniani, akatuongoza kwaye katika mambo ambayo endapo tutamtii basi atatupeleka katika Pepo za neema."

Waliotambua cheo chake zaidi ni: Masahaba zake Allah awaridhie wote; Urwa ibnu Mas'uud Allah amridhie amesema: «Naapa kwa Allah! Nimeenda kwa wafalme, nimeenda kwa Kisraa, Qaiswar na Najjaashy, naapa kwa Allah sijawahi kuona mfalme katu anayeadhimishwa na watu wake kama vile masahaba wa Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie wanavyomwadhimisha Muhammad; anapozungumza wanateremsha chini sauti zao mbele yake, wala hawamkodolei jicho kwa kumwadhimisha», imepokewa na Bukhari.

Watu wenye kumpemda sana ni masahaba zaka; Amri ibnul 'Aas amesema: «Hakuwa yeyote anapendeza zaidi kwangu kuliko Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie, wala hakuna aliyekuwa mtukufu zaidi machoni mwangu kuliko yeye, wala sikuwa naweza kumjaza machoni [kumwangalia kwa upelelezi] kwa ajili ya kumtukuza, na lau nitatakiwa nimsifu sitaweza; kwa sababu sikuwa nikimwangalia kwa upelelezi», imepokewa na Muslim.

Atakayejua sera yake na sunnah yake, au akaisikia na hali yeye ni mwadilifu na nafsi yake, basi hatamiliki ila kumtukuza, wafalme wa kinaswara walimsikia wakamwadhimisha, Hiraqlu alisema: «Ningelikuwa mbele yake ningeosha miguu yake», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Ibnu Hajar Allah amrehemu amesema: "Na mnao katika kutosheka kwake na kutaja miguu ishara ya kuwa lau atafika kwake hatataka kutoka kwake suluhu, wala uongozi, wala cheo, hakika si mengine atataka jambo ambalo hupatikana kwalo baraka."

Kichwa cha adabu pamoja na Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie: ni kujisalimisha kwake kiukamilifu, na kuandama amri yake, na kupokea habari zake kwa kuzikubali na kuzisadikisha.

Na miongoni mwa kuwa na adabu naye: ni kauli yake isitiliwe ishkali, bali rai [za watu] ndio zitiliwe ishkali kinyume na kauli yake, wala kauli yake isipingwe na kiasi [Qiyas], wala kusifungamanishwe kukubali aliyokuja nayo na mwafaka wa yeyeto. Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Akili

pamoja na Wahyi [ufunuo], ni kama [mfano wa] mtu asiye na elimu mwenye kuigiza na mtu mufti mwanachuoni; bali na huweza kuwa chini ya [tofauti] hiyo kwa daraja nyingi zisizohesabika."

Miongoni mwa haki zake kubwa zaidi: Kumueka katika cheo chake alichowekwa na Mola wake Mlezi Mwenye ushindi na utukufu miongoni mwa cheo cha uja na utume; basi asinyanyuliwe hadi katika cheo cha uola, akaombwa kinyume na Allah, wala asiangushwe cheo chake akaachwa kufuatwa.

**Baada ya haya, enyi Waislamu:**

Basi Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie hakika ni Mtume wa Allah, Allah alimpenda na akatuamrisha tumpende, akamtumiliza na akatuamrisha tumsadikishe, akamtia nguvu na akatuamrisha tushikamane na sheria yake, na akampa ushindi na akatuamrisha tumkinge [na maudhi], na kamwe hataingia mtu yeyote Peponi ila kwa kumwamini yeye, na kufuata athari zake.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم
بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ﴾

{Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayokutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma} [AtTawbah: 128].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Utume ni jambo la dharura katika kumsilihisha mja katika maisha yake [ya duniani] na marudio yake [Akhera]; kana kwamba yeye hali ya Akhera yake haitashili ila kwa kuwafuata Mitume, basi vivyo hivyo maisha yake na dunia yake hayatasilihi ila kwa kuwafuata Mitume, basi utukufu upo katika kumtii Allah na Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie, na kila mja akiwa ni mwenye kumuiga Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ndipo daraja yake itanyanyuka.

Atakayemchukia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie au uongofu wake; basi Allah hatamuafikia, atamdhalilisha na atamdunisha; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ ٱلۡأَبۡتَرُ﴾

{Hakika anaye kuchukia ndiye aliye mpungufu} [Al-Kawthar: 3].

Na kila umma unamwadhimisha Nabii wake na masahaba wake, na utukufu mkubwa zaidi wa umma huu ni kumwadhimisha Nabii wake na kuwapenda masahaba wake; kwani kupitia yeye mnao kunyanyuka kwao, saada yao na kutangulia kwao mbele ya kaumu nyinginezo.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake…

## KUMUITIKIA ALLAH NA MTUME SWALA NA SALAMU ZA ALLAH ZIMSHUKIE[1].

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wala Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani maandalizi bora ni yale yaliosuhubiana na uchamngu, na amali bora ni ile iliyoambatana na kumtendea ikhlasi Mola.

**Enyi Waislamu**:

Allah amewaleta binadamu na majini ili kumwabudu Yeye, na akawaamrisha ili watekeleze maamrisho yake, na akaandika saada kwa watu wa kumtii, na ibada yake aliyetakasika ndio ngome ambayo atakayeiingia atakuwa katika waliopata amani, na atakayeitekeleza atakuwa katika watakaookoka, nayo ni heri tupu isio na madhara ndani yake; [Allah] aliyetukuka na kuwa juu amesema:

﴿وَمَاذَا عَلَيۡهِمۡ لَوۡ ءَامَنُواْ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ وَأَنفَقُواْ مِمَّا رَزَقَهُمُ ٱللَّهُۚ﴾

{Na ingeliwadhuru nini wao lau wangelimwamini Allah na Siku ya Mwisho, na wakatoa katika aliyowaruzuku Allah?} [An-Nisaa: 39].

Kila heri katika ardhi kwa hakika imepatikana kwa sababu ya kumtii Allah na Mtume wake, na shari, machungu, na ghamu inayomsibu mja katika nafsi yake hakika si mengine yamepatikana kwa sababu ya kumhalifu Mtume swala na salamu zimshukie; Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Atakayeuzingatia ulimwengu na shari zilizotokea ndani yake: atajua kuwa kila shari katika ulimwengu sababu yake ni kumhalifu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie na kuacha kumtii."

Ni katika rehema za Allah kwa waja wake: kuwa amewaamrisha

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na tatu ya mwezi wa Rabiul Awwal, mwaka elfu moja mia nne na thelathini na tano hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

kumuitikia Yeye; ili wapate heri; akasema:

﴿ٱسۡتَجِيبُواْ لِرَبِّكُم مِّن قَبۡلِ أَن يَأۡتِيَ يَوۡمٞ لَّا مَرَدَّ لَهُۥ مِنَ ٱللَّهِ﴾

{Muitikieni Mola wenu Mlezi kabla haijafika siku isiyoepukika itokayo kwa Allah} [Ash-Shuura: 47];

Basi waumini wakamuitikia Mola wao Mlezi wakafaulu:

﴿إِنَّمَا كَانَ قَوۡلَ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ إِذَا دُعُوٓاْ إِلَى ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ لِيَحۡكُمَ بَيۡنَهُمۡ أَن يَقُولُواْ سَمِعۡنَا وَأَطَعۡنَاۚ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ﴾

{Haiwi kauli ya Waumini wanapoitwa kwa Allah na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila ni kusema: Tumesikia na tumetii! Na hao ndio wenye kufanikiwa} [An-Nuur: 51].

Na Allah alihuisha nyoyo zao kwa hilo, na cheo chao kikanyanyuka; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسۡتَجِيبُواْ لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمۡ لِمَا يُحۡيِيكُمۡ﴾

{Enyi mulioamini! Muitikieni Allah na Mtume anapowaita kwenye jambo la kuwapa uzima wa milele} [Al-Anfaal: 24].

Atakayefanya haraka kumtii Mola wake Mlezi, [Allah] atamzidisha uongofu katika uongofu wake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱلَّذِينَ ٱهۡتَدَوۡاْ زَادَهُمۡ هُدٗى وَءَاتَىٰهُمۡ تَقۡوَىٰهُمۡ﴾

{Na wale walioongoka anawazidishia uongofu na anawapa uchamngu wao} [Muhammad: 17].

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Mtu kila anapokuwa ni mwenye kumfuata zaidi Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie; atakuwa mwingi zaidi wa kumtekelezea Allah Tawhidi na kumfanyia Yeye ikhlasi katika dini, na pindi atakapoepuka kumfuata, basi dini yake itapungua kwa kadri ya hilo."

Atakayemuiitikia Mola wake Mlezi basi dua zake zitaitikiwa; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَيَسۡتَجِيبُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ﴾

{Na [Allah] anawaitikia wanaoamini na wakatenda mema} [Ash-Shuura: 26], yaani: anaitikia dua zao.

﴿وَيَزِيدُهُم مِّن فَضۡلِهِۦۚ﴾

{Na anawazidishia fadhila zake} [Ash-Shuura: 26];

Bali Allah atampenda, atamrehemu na atamuingiza Peponi; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿لِلَّذِينَ ٱسۡتَجَابُواْ لِرَبِّهِمُ ٱلۡحُسۡنَىٰۚ﴾

{Waliomuitikia Mola wao Mlezi watapata Pepo} [Ar-Ra'd: 18].

Mitume [salamu ziwashukie] waliharakisha kunyenyekea na kujisalimisha [kwa Allah]; Allah alisema kumwambia kipenzi chake Ibrahim [salamu zimshukie]:

﴿أَسۡلِمۡۖ قَالَ أَسۡلَمۡتُ لِرَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾

{Jisalimishe! Alisema: Nimesilimu, nimejisalimisha kwa Mola wa walimwengu wote} [Al-Baqarah: 131].

Na alimwamrisha kumchinja mwanawe wa pekee kwa mkono wake, basi akamlaza kwa paji la uso ili amchinje, na mwanawe Ismail akamwambia:

﴿يَٰٓأَبَتِ ٱفۡعَلۡ مَا تُؤۡمَرُۖ سَتَجِدُنِيٓ إِن شَآءَ ٱللَّهُ مِنَ ٱلصَّٰبِرِينَ﴾

{Akasema: Ewe baba yangu! Tenda unavyoamrishwa, utanikuta mimi, Inshallah, katika wanao subiri} [As-Swaaffaat: 102].

Musa naye [salamu zimshukie] alikimbilia kumridhisha Mola wake Mlezi na akasema:

﴿وَعَجِلۡتُ إِلَيۡكَ رَبِّ لِتَرۡضَىٰ﴾

{Na nimefanya haraka kukujia, Mola wangu Mlezi, ili uridhike} [Twaahaa: 84].

Allah alichukua ahadi ya Manabii kuwa atakapomtuma kwao Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie ya kuwa wamwamini na wamnusuru, wakasema:

﴿أَقۡرَرۡنَاۚ﴾

{Tumekiri} [Aalu Imraan: 81].

[Allah] akasema kumwambia Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie:

﴿قُمۡ فَأَنذِرۡ﴾

{Simama uonye!} [Al-Muddaththir: 2],

basi akatoka kwa watu akiwa analingania katika Tawhidi, na [Allah] akasema kumwambia:

﴿قُمِ ٱلَّيۡلَ إِلَّا قَلِيلٗا﴾

{Simama usiku [kwa ibada], ila kidogo tu!} [Al-Muzzammil: 2],

basi akasima hadi miguu yake ikapasuma.

Na waliomnusuru Isa [salamu zimshukie] walimuitikia, Isa aliwaambia:

﴿مَنۡ أَنصَارِيٓ إِلَى ٱللَّهِۖ قَالَ ٱلۡحَوَارِيُّونَ نَحۡنُ أَنصَارُ ٱللَّهِ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ﴾

{Nani wasaidizi wangu kwa Allah? Wanafunzi wake wakasema: Sisi ni wasaidizi wa Allah. Tumemwamini Allah} [Aalu Imraan: 52].

Majini walihimizana baadhi yao kwa baadhi yao kuitikia mwito wa Allah:

﴿يَٰقَوۡمَنَآ أَجِيبُواْ دَاعِيَ ٱللَّهِ وَءَامِنُواْ بِهِۦ يَغۡفِرۡ لَكُم مِّن ذُنُوبِكُمۡ وَيُجِرۡكُم مِّنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ﴾

{Enyi kaumu yetu! Muitikieni Mwenye kuitia kwa Allah, na mwamininі, Allah atakusameheni, na atakukingeni na adhabu chungu} [Al-Ahqaaf: 31].

Masahaba Allah awaridhie walipata ubora; kwa ajili ya usuhuba wao [kwa Mtume], ikhlasi yao na kukimbilia kwao katika kumuitikia Allah na Mtume wake, basi cheo chao kikazidi mbele ya Allah, na waliamrishwa kuelekea Kaaba basi wakageuza nyuso zao kutoka 'Baytul Maqdis' kuielekea [Kaaba] punde tu waliposikia [amri] ya kugeuka ilhali wao wamo ndani ya swala, wala hawakucheleweshа kuitikia [amri] hadi swala itakayofuata.

Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliita watu kutoa sadaka, basi wakatoa mali yao bora; Umar ibnul Khattwaab Allah amridhie akatoa nusu ya mali yake, na Abu Bakar As-Swiddiq Allah amridhie akatoa mali yake yote, na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Atakayeliandaa jeshi la uzito; basi atapata Pepo, akaliandaa Uthmaan Allah amridhie**», imepokewa na Bukhari.

Ilipoteremka kauli ya Allah:

﴿لَن تَنَالُواْ ٱلۡبِرَّ حَتَّىٰ تُنفِقُواْ مِمَّا تُحِبُّونَ﴾

{Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda} [Aalu Imraan: 92], basi Abu Twalha Allah amridhie akasimama kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, akasema: «**Ewe Mtume wa Allah!**

**Hakika mali yangu yanayopendeza zaidi kwangu ni 'Bayruuhaa', nayo ni sadaka kwa ajili ya Allah**», imepokewa na Bukhari.

Kwa ishara tu kutoka kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie kuwaelekeza masahaba wadogo katika kisimamo cha usiku ilitosha kwao kuwa wafanye ibada sana ya usiku; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumwambia Abdullah ibnu Umar Allah awaridhie ilhali yeye ni mdogo: «**Abdullah ni mtu bora, lau ingelikuwa anasimama sehemu ya usiku [kwa ibada]; basi akawa baada ya hapo halali usiku ila kidogo tu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Walimkomboa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kwa roho zao ili kumtii Allah; Al-Miqdaad ibnul Aswad Allah amridhie alimjia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie naye akiwaapiza washirikina, basi akasema «Hatutasema kama walivyosema watu wa Musa:

﴿فَٱذۡهَبۡ أَنتَ وَرَبُّكَ فَقَٰتِلَآ إِنَّا هَٰهُنَا قَٰعِدُونَ﴾

{Basi nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa} [Al-Maaida: 24], lakini sisi tutapigana kwa kuliani mwako, kushotoni mwako, mbele yako na nyuma yako, Ibnu Mas'uud Allah amridhie alisema: Basi nikamwona Nabii swala na salamu za Allah zimshukie uso wako umeng'aa na amefurahishwa, yaani; na kauli yake [Al-Miqdaad]», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Masahaba walikomeka na [baadhi ya] kauli na matendo pindi tu walipomsikia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akikataza, wala hawakumuuliza kuhusiana nazo kwa ajili ya kumuitikia yeye; utapata katika 'jahiliyyah' [kabla ya Uislamu] walikuwa wakiapa na mababa zao na ndimi zao zilikuwa zimezoea hilo, basi Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasema: «**Allah anawakataza kuapa na mababa zenu**, Umar Allah amridhie alisema: basi naapa kwa Allah kuwa sikuapa kwa [kiapo] hicho tokea nilipomsikia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akikataza, si katika maneno yangu wala katika kunukuu», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Walipika chakula siku ya njaa, wakakiacha kwa ajili ya katazo la Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, siku ya [vita vya] Khaybar ilikuwa punda ni halali basi wakampika, basi akapiga mpigambia mbia wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie: «**Allah na Mtume wake wanawakataza nyama za punda; kwani hizo ni uchafu - ni katika kazi ya shetani** -, Anas Allah amridhie amesema: Basi masufuria yakapenduliwa na yaliyomo ndani yake, ilhali yanatokota nyama», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Pombe ilikuwa mubahi hadi mwanzoni mwa Uislamu, na waliposikia tu katazo lake kutoka kwa mtu aliyekuwa akitembea katika njia za Madina [akitangaza] waliimwaga, Abu An-Nu'maan Allah amridhie amesema: «Nilikuwa nanywesha watu katika nyumba ya Abu Twalha, ikateremka [aya] ya kuharamisha pombe, [Mtume] akaamrisha mwenye kunadi akanadi, Abu Twalha akasema: Toka uangalie hii sauti ni ya nini? Asema: nikatoka nikasema: huyu ni mwenye kunadi ananadi: Jueni kuwa pombe imeharamishwa. [Abu Twalha] akaniambia: Nenda ukalimwage. Akasema: Nikatoka kuenda [kulimwaga] katika vichochoro vya Madina», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na katika riwaya nyingine: «basi hawakumuuliza kuhakikisha, wala hawakuuliza tena kuhusu pombe baada ya habari ya yule mtu», imepokewa na Muslim.

Nao masahaba Allah awaridhie wanamuiga Nabii swala na salamu za Allah zimshukie katika wanayovaa bila hata yeye kuwasemesha chochote; Ibnu Umar Allah awaridhie amesema: «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alitengenezesha pete ya dhahabu, akawa anaivaa na akijaalia kito chake ndani ya kiganja, basi watu nao wakatengenezesha pete zao, kisha yeye [Mtume] alikaa juu ya mimbari akaivua, na akasema: **Mimi nilikuwa nikivaa pete hii, na nikijaalia kito chake kwa ndani**; kisha akaitupa, kisha akasema: **Naapa kwa Allah sitaivaa milele**; basi na watu wakatoa pete zao», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Abdullah ibnu Umar Allah awaridhie aliandika wasia wake pindi aliposikia kauli ya Nabii swala na salamu zimshukie: «**Ni haki ipi ya mtu Mwislamu ana kitu anataka kutoa wasia ndani yake kisha alale siku mbili ila wasia wake umeandikwa kwake**. Ibnu Umar Allah amridhie akasema: Haujanipitia hata usiku mmoja kutoka nimsikie Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akisema hivyo; isipokuwa wasia wangu uko nami», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nao masahaba Allah awaridhie walikimbilia kuhifadhi ndimi zao kutokana na yasiolingana nao, wakiitikia kwa hilo wasia wa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie; Jabir ibnu Sulaym Allah amridhie amesema: «Nilimjia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie nikasema: Ewe Mtume wa Allah! Hakika mimi ni mtu wa mashambani, na ninao ugumu wa kitabia, basi nipe wasia. Akasema: "**Usimtusi mtu yeyote**." Akasema: Basi baada ya wasia wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, sikumtusi mtu wala mbuzi wala ngamia», imepokewa na Ahmad.

Waliitikia maamrisho ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie katika harakati zao na utulivu wao, siku ya Khaybar Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alimpatia Ali Allah amridhie bendera, na akamwambia:

«**Tembea wala usigeuke, hadi Allah akufungulie**, basi Ali akatembea kidogo, kisha akasimama wala hakugeuka, akapiga kelele kuita: "Ewe Mtume wa Allah!" -Alinyanyua sauti yake kwa ajili ya kuwa yuko mbali na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, wala hakugeuka kwa ajili ya kuitikia kauli ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie-: "Niwapige vita juu ya jambo gani?"», imepokewa na Muslim.

Waliepuka aliyowakataza - hata ikiwa mna maslahi ya wazi ya kuwanusuru Waislamu ndani ya kufanya liliokatazwa -, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumwambia Hudheifa siku ya Al-Ahzaab: «"**Simama ewe Hudheifa, na uniletee habari za kaumu hii [maadui], wala usiwatishe wakakujua wakakabili kutujia**", alipowajia alimwona Abu Sufyan - na wakati huo alikuwa kiongozi wa washirikina - akiwa karibu naye, akiupatisha joto mgongo wake na moto. Asema [Hudheifa]: Nikaweka mshale katika upinde na nikataka kumrushia, lakini nikakumbuka kauli ya Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie: "**Wala usiwatishe wakakujua wakakabili kutujia**", na lau ningemrushia ningempata», imepokewa na Muslim.

Kumfuata kwao Mtume swala na salamu za Allah zimshukie katika maamrisho na makatazo ni kutokana na imani na yakini iliyokita mizizi, Raafi'u ibnu Khadiij Allah amridhie amesema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alitukataza jambo ambalo lilikuwa ni lenye kutufaa, na [lakini] kumtii Allah na Mtume wake ni manufaa zaidi kwetu», imepokewa na Muslim.

Wanawake waumini walikimbili kuitikia kwa kumtii Allah; Haajar [salamu zimshukie] alimtgemea Mola wake Mlezi, akamtii mume wake, na akaishi katika jangwa lisilo na mimea wala maji, na wakati huo Makkah hakuna hata mtu mmoja, na hali ilio dhahiri ni kuangamia yeye na mwanawe, basi akamwambia mumewe Ibrahim [salamu zimshukie]: «Allah ndiye aliyekuamrisha hili? Akasema: Ndio. Akasema: Basi hatatupoteza», imepokewa na na Bukhari.

Pindi faradhi ya hijabu ilipoteremka kwa masahaba wa kike wakati huo hawakuwa na vitambara vya kujifunka hijabu, basi wakakimbilia kupasua nguo zao ili kuitikia amri ya Allah, na wakafunika nazo nyuso zao; Aisha Allah amridhie alisema: «Allah awarehemu wanawake waliohajiri wa mwanzo, pindi Allah alipoteremsha:

﴿وَلۡيَضۡرِبۡنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ﴾

{Na waangushe mitandio yao juu ya vifua vyao} [An-Nuur: 31]; walipasua *'muruut'* zao - nayo ni sehemu ziliozidi katika nguo zao chini -,

wakajitanda nazo [uso]», imepokewa na Bukhari.

**Na baada ya haya, enyi Waislamu:**

Basi kumtii Allah na Mtume wake ni kutekeleza ipasavyo shahada mbili na ni ukamilifu katika uja; basi amri yeyote [katika amri za Allah] inapogonga sikio lako harakisha kuitekeleza hali ya kuwa umefurahika kwa kumtii Mola wako Mlezi, na endapo itakuwa ni katazo basi liepuke ukae kando nalo ukiwa na yakini kuwa ni lenye kudhuru, ukitaka [kwa hilo] radhi za Muumba wako.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَيَخۡشَ ٱللَّهَ وَيَتَّقۡهِ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَآئِزُونَ﴾

{Na mwenye kumtii Allah na Mtume wake, na akamwogopa Allah na akamcha, basi hao ndio wenye kufuzu.} [An-Nuur: 52].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Watu wenye uhai kamili zaidi ni waliowakamilifu zaidi wa kuitikia. Atakayekukosa sehemu katika hilo atakosa sehemu katika uhai, na ambaye hatamuitikia Allah basi atamuitikia asiyekuwa Yeye miongoni mwa viumbe na atamdhalilisha.

Allah ametahadharisha kumuasi akasema:

﴿فَلْيَحْذَرِ ٱلَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِۦٓ أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾

{Basi watahadhari wanaokhalifu amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu} [Al-Fur: 63].

Abu Bakr Allah amridhie alisema: «Sitaacha chochote ambacho Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akikifanya ila nitakifanya, hakika mimi nahofia nitapotea endapo nitaacha kitu katika amri yake», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Kusitasita katika kufanya utiifu au uvivu katika kuutekeleza kunapingana na ukamilifu wa kuitikia, na atakaye tanguliza kauli yeyote mbele ya kauli ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie hatakuwa katika waliomuitikia, na umma wa Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie wote siku ya Akhera «**wataingia Peponi ila aliyekataa**, wakasema: Ewe Mtume wa Allah! Na ni nani atakaye kataa? Akasema: "**Atakayenitii ataingia Peponi, na atakayeniasi hakika huyo ndiye aliyekataa**"», imepokewa na Bukhari.

Mwenye kukeuka atatamani kurudi duniani ili kumtii Allah na Mtume wake, na atatamani kujitolea fidia iliyojaa ardhi na mfano wake; ili aokoke kutokana na adhabu:

﴿وَٱلَّذِينَ لَمْ يَسْتَجِيبُواْ لَهُۥ لَوْ أَنَّ لَهُم مَّا فِي ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا وَمِثْلَهُۥ مَعَهُۥ لَٱفْتَدَوْاْ بِهِۦٓ﴾

{Na waliokosa kumuitikia, hata wangelikuwa navyo vyote viliomo katika ardhi na mfano wa hivyo, bila ya shaka wangelivitoa kujikombolea!} [A-Ra'd: 18].

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# KUAMINI SIKU YA MWISHO

## ALAMA ZA KIYAMA[1]

Sifa njema zote anastahiki Allah, Mwenye kumpa ushindi anayemtii na kumcha Yeye, na Mwenye kumdhalilisha atakayepoteza amri yake na kumuasi, namhimidi Yeye kwa Ukarimu wake mwingi na aliyotupatia, na namshukuru kwa neema zake kubwa na aliyotoa.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika, hatuna Mola Mlezi asiyekuwa Yeye, wala hatumwabudu ila Yeye.

Na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, mja bora zaidi aliyemchagua, na Mtume bora zaidi aliyemteua, ewe Allah mswalie na msalimie yeye, watu wake, masahaba wake na yule ambaye matamanio yake ni yenye kufuata uongofu wake.

**Ama baada ya himdi hii**:

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na kamateni Uislamu kwa kishikio madhubuti, na jueni ya kwamba nyayo zenu hazina nguvu ya kuwa juu ya Moto.

**Enyi Waislamu:**

Hakika kuamini siku ya Mwisho na yaliomo ndani miongoni mwa thawabu na adhabu ni mojawapo wa nguzo za Uislamu na majengo yake makubwa, na Allah alijaalia kabla ya Kiyama alama zenye kujulisha ukaribu wake; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿فَهَلۡ يَنظُرُونَ إِلَّا ٱلسَّاعَةَ أَن تَأۡتِيَهُم بَغۡتَةٗۖ فَقَدۡ جَآءَ أَشۡرَاطُهَاۚ فَأَنَّىٰ لَهُمۡ إِذَا جَآءَتۡهُمۡ ذِكۡرَىٰهُمۡ﴾

{Kwani wanangojea jengine isipokuwa iwafikie Saa [ya Kiyama] kwa ghafla? Na hakika alama zake zimekwisha kuja. Na itapo wajia kutawafaa wapi kukumbuka hapo} [Muhammad: 18].

Na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiadhimisha amri ya Kiyama; basi alikuwa anapokitaja mashavu yake yanakuwa mekundu, na sauti yake inanyanyuka na ghadhabu yake inakuwa kali, na anabainisha ndani yake na anakariri.

Masahaba walikuwa Allah awaridhie wakikumbushana jambo la Kiyama; Hudheifa Allah amridhie amesema: «Nabii swala na salamu za Allah

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe tatu ya mwezi wa Dhul Qa'dah, mwaka elfu moja mia nne na kumi na tisa hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

zimshukie alituona na hali sisi tunakumbushana, akasema: "**Mnakumbushana nini?**" Wakasema: "Tunataja na kukumbuka Kiyama"», imepokewa na Muslim,

Nabii alipokithirisha kukitaja na zikawa nyingi alama [za kuonyesha] kukurubia kwake, masahaba walijihurumia isije kikawasimamia wao.

Haya yaliotangulia, na kwa hakika zimedhihiri alama zake nyingi, na yamehakikishika yale aliyoyatolea habari Al-Mustwafaa swala na salamu za Allah zimshukie, na kila siku Waumini wanazidi kumwamini na kumsadikisha; kwani zinadhihiri dalili za unabii wake na alama za ukweli wake, zinazowajibisha kwa Waislamu kushikamana na dini hii ya Haniif [ya Tawhidi na kuepuka ushirikina] ili wajiandae kuondoka, kwani Kiyama kimeshakurubia na alama zake zimeshajitokeza, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿ٱقۡتَرَبَتِ ٱلسَّاعَةُ وَٱنشَقَّ ٱلۡقَمَرُ﴾

{Kiyama kimekaribia, na mwezi umepasuka!} [Al-Qamar: 1].

Pindi alama kubwa zikidhihiri; zitafuatana kama vile ~~tunda~~ [shanga] zinavyofuatana katika mtungo uliokatika kifungo chake; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَلِلَّهِ غَيۡبُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۚ وَمَآ أَمۡرُ ٱلسَّاعَةِ إِلَّا كَلَمۡحِ ٱلۡبَصَرِ أَوۡ هُوَ أَقۡرَبُۚ﴾

{Na ghaibu zote za katika mbingu na ardhi ziko kwa Allah. Wala halikuwa jambo la Saa [ya Kiyama] ila kama kupepesa kwa jicho, au ni karibu zaidi. Hakika Allah ni Muweza wa kila kitu} [An-Nnahl: 77], Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Yoyote itakayokuwa kabla ya mwenzake, basi nyingine inafuatia ni karibu**», imepokewa na Muslim, na katika Musnad: «**Alama ni shanga zilizotungwa katika uzi, basi uzi ukikatwa zinafuatana baadhi kwa baadhi**».

**Enyi Waislamu:**

Miongoni mwa alama za Kiyama ni: Kutumwa Al-Mustwafaa [Mteule Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie; hakika imethibiti kutoka kwake swala na salamu zimshukie kuwa alisema: «**Nimetumwa mimi na Kiyama pamoja, kimekurubia kunitangulia**», imepokewa na Ahmad.

Na miongoni mwazo ni: Kufa kwake [swala na salamu zimshukie], na kwa kufa kwake dunia ilitanda giza katika macho ya masahaba Allah awaridhie.

Na ni miongoni mwa alama zake: Kudhihiri fitina kubwa,

zinachanganyika ndani yake haki na batili, na Imani itatingisika, na «**mtu atapita katika kaburi la mtu ajigeuzegeuze kwa mwili wake juu yake,** kwa ajili ya kugeuka kwa hali na kubadilika kwa sheria, na **aseme: "Laiti ningekuwa sehemu ya aliyo ndani ya kaburi hili, hana lolote [la kumfanya aseme hivyo] ila bala**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Ibnu Mas'uud Allah amridhie anasema: «Zitawajia zama ambazo lau mmoja wenu atapata mauti yanauzwa; basi atayanunua», na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Mnao mbele [kabla] ya Kiyama fitina kama sehemu ya usiku wa giza; ndani yake mtu ataingiliwa na asubuhi akiwa muumini na jioni imuingilie akiwa kafiri, na ataingiliwa na jioni akiwa kafiri na asubuhi imuingilie akiwa muumini**», imepokewa na Ahmad.

Mwisho wa umma huu utasibiwa na balaa; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Hakika umma wenu huu: umejaaliwa afueni yake iko mwanzoni mwake, na mwishoni mwake utasibiwa na fitina na mambo mtakaoyakanusha, na zitakuja fitina kila inayokuja ni kubwa kuliko mwenzake, na itakuja fitina muumini asema: Hii ndio yenye kuniangamiza, kisha iondoke, na itakuja fitina [nyingine] muumini asema: Hii ; basi anayependa kuepushwa na Moto na aingie Peponi, basi mauti yamjie hali yeye anamwamini Allah na siku ya mwisho**», imepokewa na Muslim.

**Enyi Waislamu:**

Ni katika alama za Kiyama: Kukithiri zilizala, na itatokezea kudidimizwa mashariki, magharibi na katika Jaziiratul Arab [Uarabuni], na wanyama mwitu watazungumzisha watu, na mtu atazungumzishwa na ncha ya fimbo yake na ukanda wa kiatu chake, na paja lake litampa habari ya walioyafanya watu wake baada ya kuondoka kwake, na mnyama atawatokea watu wakati wa mchana akiwazungumzisha: Kuwa watu walikuwa hawayakinishi aya za Mola wao.

Zama zitakurubiana; mwaka utakuwa kama mwezi, na mwezi utakuwa na wiki, na wiki itakuwa kama siku, na siku itakuwa kama saa (mda mchache), na saa litakuwa kama muda kadri ya kuchomeka jani la mtende, na wanawake watakithiri na wanaume wawe wachache hadi ifikie wanawake hamsini watakuwa na msimamizi mmoja [mwanamume], na watatoka 'Ya-juuj wa Ma-juuj', imekuja katika sahihi mbili [Bukhari na Muslim] kutoka kwa Zainab binti Jahsh Allah amridhie, kuwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie aliingia kwake siku moja kwa hali ya hofu akisema: «***'Laa ilaaha illa llaah'* [Hapana apasaye kuabudiwa ila Allah], ole wao waarabu kutokana na shari iliyokurubia! Leo ngome ya 'Ya-juuj wa Ma-**

**juuj' imefunguliwa mfano wa hivi, na akafunga duara kwa vidole vyake viwili, cha gumba na kilichofuatia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Elimu itapungua na ujinga utadhihiri hadi watu wasijue faradhi za Uislamu; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Uislamu utamalizika kama inavyoisha nakshi ya nguo, hadi isijulikanwe Swaumu ni nini, wala Sadaka ni nini, wala Hija na Umra nini, na kitafutwa Kitabu cha Allah usiku, basi kusibaki katika ardhi hata aya moja, na watabakia makundi ya watu - mwanamume mkongwe na mwanamke mkongwe - wakisema: Tuliwakuta baba zetu juu ya neno hili: 'Laa ilaaha illa llaah', basi sisi twalisema**», imepokewa na Al-Haakim.

Ya haramu yatachukuliwa duni, na makatazo yatadharauliwa, basi pombe inywiwe, zinaa ienee, na ubahili utatiwa katika nyoyo za watu, na mauwaji yatakithiri, «**hadi iwaijie watu siku, aliyeuwa asijue kwanini ameuwa, wala aliyeuliwa asijue kwanini ameuliwa**, ikaulizwa: Vipi litakuwa hilo? Akasema [Nabii]: ***Al-Harj*** **[Mauwaji ya kiholela]; muuwaji na aliyeuliwa wote wataingia Motoni**», imepokewa na Muslim.

Shingo za watu zitanyanyuka kuangalia ulimwengu; basi washindane kujenga majengo marefu, na waipe mgongo dini ya Allah, na ushirikina ujitokeze katika umma huu, na makabila ya kiarabu wafuate washirikina; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Kiyama hakitasimama hadi makabila katika umma wangu waungane na washirikina, na hadi makabila katika umma wangu [warudi] kuabudu masanamu**», imepokewa na Ahmad.

Pindi umma utaepuka dini yake, upoteze mila yake, na uisahau sheria yake; utapotea na utefute uongofu kutoka kwengine kusiokuwa Wahyi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Kiyama hakitasimama hadi umma wangu uandame waliokuwa nayo karne za kabla yake, shubiri kwa shubiri, na kiraa kwa kiraa**», imepokewa na Bukhari.

Utakithiri urongo na hadaa, na watatoka madajjali [warongo] karibia thelathini, wote wanadai Unabii.

Sifa njema zitaondolewa kwa watu, basi amana itakurubia kutotekelezwa; «**Basi kusemwe: Katika kabila fulani kuna mtu mwaminifi, na aambiwe mtu: ni mwenye akili ilioje, na mwerevu alioje, mkakamavu alioje, na hakika hana kifuani mwake hata uzito wa chembe ndogo ya Imani**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na ni katika kupoteza amana: Kutegemeza jambo kwa asiyestahili.

Na «**Kiyama hakitasimama hadi Madina iwatoe waovu wake kama**

**vile ala ya uhunzi inavyotoa uchafu wa chuma**», na Madina iachwe ikiwa imeimarika «**juu ya kheri iliokuweko, hakuna ndani ila wanyama mwitu na ndege, kisha watoke wachunga wawili kutoka 'Muzainah' wakikusudia Madina, wakiwapigia kelele mbuzi wao [wakiwachunga], basi waikute - Madina - iko tupu, hakuna mtu ndani yake, hadi wakifika *'Thaniyyatal Wadaai'* wataporomoka kwa nyuso zao**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

**Enyi Waislamu**:

Baina ya kuumbwa Adam na kusimama Kiyama hakuna kiumbe shari zaidi na fitina kubwa zaidi kuliko Dajjali, na hakuna Nabii yeyote ila ametahadharisha umma wake kutokana naye, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akijilinda na Allah kutokana naye, na hakika [Nabii] swala na salamu amekithirisha kumtaja kwa masahaba wake [akiwatahadharisha]; An-Nawwaas ibnu Sam'aan Allah amridhie amesema: «hadi tukadhani kuwa yupo katika upande wa mitende, tulipomuendea alitambua hali hiyo [ya wasiwasi] tuliyokuwa nayo, akasema: "**Mnanini?**" Tukasema: Ewe Mtume wa Allah! Umemtaja Dajjali asubuhi, ukateremsha sauti na ukanyanyua, hadi tukadhani yupo katika upande wa mitende! Akasema: "**Mimi nawahofia zaidi asiyekuwa Dajjali, lau atatoka na mimi niko baina yenu basi mimi ndio nitakayemtahini pasi na nyinyi, na lau atatoka na mimi siko baina yenu basi kila mtu ajitetee kivyake, na Allah ndiye halifa wangu juu ya kila Mwislamu** [yaani ni mwenye kumhifadhi na kumwepushia shari ya Dajjali]"», imepokewa na Muslim.

Katika hali ya kufifia dini na kuondoka elimu atatoka Masihi wa upotevu kutokea upande wa mashariki; basi watu wamkimbie kuelekea majabalini, na atembee juu ya ardhi, asiache mji ila auingie, isipokuwa Makkah na Madinah; Kwani Allah amemuharamishia kuingia miji hii miwili, kila akitaka kuingia Malaika anamkabili akiwa na upanga mkononi anamzuilia kuiingia, katika kila njia miongoni mwa njia zake mna Malaika wanailinda, na Madinah itatetemeka mara tatu basi atoke kila mnafiki na kafiri, na ashuke katika ardhi ambayo haijaimarishwa katika 'Jurfi', na wengi watakaotoka kumuendea watakuwa wanawake, mpaka mtu atarudi kwa mke wake, mamake, binti yake, ukhti yake na amati yake, amfunge katika kiguzo, kwa kuhofia asije akatoka kumuendea Dajjali.

**Enyi Waislamu:**

Hakika Dajjali ana fitina kubwa, anao pamoja naye mito miwili yanayotembea: mmojawapo kwa mtazamo wa jicho ni maji meupe, na mwengine kwa mtazamo wa jicho ni moto unaorurumba; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Mmoja wenu akikuta hayo basi aujie**

**mto anaouona kuwa ni moto, na afunge macho, kisha ainamishe kichwa chake na anywe; kwani hakika huo ni maji baridi**», imepokewa na Muslim. Upande mwingine, na ule wanaouona watu kuwa ni maji, basi hakika ni moto unaochoma.

Allah atawatahini waja wake na Dajjali; kwa yale atakayomjalia miongoni mwa mambo yanayovuka ada ya kilimwengu, yatakayoonekana katika wakati wake, na atamuezesha vitu ambavyo ni katika uwezo wa Allah; miongoni mwa kumhuisha mtu maiti ambaye atamuuwa, na kudhihiri pambo la dunia pamoja na urutuba, na pepo yake, moto wake na mito yake miwili, na kanzi za ardhi kumfuata yeye, na kuamrisha kwake mbingu inyeshe nayo itanyeshe, na ardhi iote [mimea nayo] iote, na ambaye hatamuitikia na atarudisha amri yake atafikwa na ukame, uchache, kufa kwa wanyama na kupungua kwa mali, nafsi na matunda, yote hayo yatatokeya kwa uwezo wa Allah aliyetukuka na matakwa yake, kisha Allah atamkosesha uwezo baada ya hapo, basi asiweze tena kumuua mtu yule ambaye alimhuisha baada ya kumuuwa wala mwengineo.

Mola Mlezi atawatahini waja wake na Dajjali katika mwisho wa zama; basi awapoteze kwa ajili yake wengi na awaongoze wengi, na walio na shaka wakufuru, na Waumini wazidi imani, kukaa kwake katika ardhi ni siku arubaini; siku moja ni kama mwaka, na siku moja ni kama mwezi, na siku moja ni kama wiki, na siku zilizosalia ni kama siku zenu, na kutembea kwake haraka katika ardhi ni kama mfano wa mvua iliosukumwa na upepo.

Ama sifa zake: Ni barobaro mwenye mwili mwekundu, mwenye komo, ana shingo pana, ilioinama, mwenye nywele ngumu, chongo wa jicho moja, kana kwamba jicho lake ni zabibu ilioharibika, hazaliwi mtoto, Tamim Ad-Daary Allah amridhie alisema katika kumsifu: «ni mtu mkubwa zaidi kimaumbile tuliowahi kumwona, na aliyefungwa na vifungo vigumu sana», na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema katika kumwlezea: «**Baina ya macho yake ameandikwa *'Kaafir'*, ataisoma kila muumini, anayejua kuandika na asiyejua kuandika**», imepokewa na Muslim.

Imam As-Saffaariiny Allah amrehemu anasema: "Inampasa kila mwanachuoni anushuru hadithi za Dajjali baina ya watoto, wanawake na wanaume, sana sana katika zama zetu hizi ambazo fitina zimeinuka ndani yake, na mitihani imekithiri ndani yake".

Hakika kuhifadhika na Dajjali ni kwa kushikamana na Uislamu, kijihami na silaha ya Imani na kujua Majina ya Allah na Sifa zake njema zaidi juu mwangaza wa yaliokuja katika Kitabu cha Allah na Sunnah ya Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie.

Masihi [Dajjali] ni mtu anakula na kunywa, na Allah aliyetukuka ametakasika na hayo, na Dajjali ni chongo jicho moja na Mola wetu Mlezi si

chongo, na Allah haonekani na yeyote kabla hajafa, na Dajjali watu wanamwona; Muumini wao na kafiri wao.

Basi kithirisheni kuomba ulinzi kutokana na fitina yake, na atakayekutana naye miongoni mwenu basi amsomee aya za mwanzo za suratul Kahf, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Atakayehifadhi aya kumi za mwanzo wa suratul Kahf; atalindwa na fitina ya Dajjali**», imepokewa na Muslim, na katika mapokezi mengine: «**aya za mwisho wa suratul Kahf**», imepokewa na Abu Daud. Na utakapomsikia Dajjali basi muepuke wala usimuendee; kwani mtu humuendea naye akijidhani ni muumini mara akamfuata kwa ajili ya shubuha anazozieneza.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿ٱقۡتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمۡ وَهُمۡ فِي غَفۡلَةٖ مُّعۡرِضُونَ﴾

{Imewakaribia watu hesabu yao, nao wamo katika mghafala wanapuuza} [Al-Anbiyaa: 1]

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahiki Allah ambaye humtaja anayemtaja, na humzidishia anayemshukuru, na hukubali toba ya aliyetubia kwake na akaomba msamaha, na anamwadhibu aliyemkanusha na akamkufuru, namhimidi kwa wingi wa neema zake, na namuomba ziada ya fadhila zake.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika, amewaamrisha Waumini kumcha Yeye.

Nanashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, mbora wa wenye kumdhukuru Allah na kielelezo cha wenye kumshukuru, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, watu wake, masahaba wake na waliowandama.

**Ama baada ya haya, enyi Waislamu:**

Pindi atakapotoka Dajjali katika zama za mwisho watakithiri wafuasi wake na fitina itaenea, na hatasalimika naye ila Waumini wachache, na hapo ndio atateremka Isa mwana wa Maryam katika Mashariki ya Shaam, katika mnara mweupe, na wakutane pembeni mwake waja wa Allah Waumini; basi aende nao wakimkusudia masihi wa upotevu. Wakati huo wa kuteremka Isa, Dajjali atakuwa aelekea Baytul Maqdis, basi Isa [salamu zimshukie] amfikie akiwa katika 'Baab Ludd' huko Palestina, Dajjali atakapomwona atayayuka kama vile inavyoyayuka chumvi ndani ya maji, basi Isa amwambie: Hakika mimi nina dharuba kwako sitaikosa, basi Isa amfikie na amuue kwa mkuki, na wafuasi wake washindwe, na kwa kuuliwa yeye itaisha fitina yake kubwa, na amri ni ya Allah kabla ya hapo na baada.

**Enyi waja wa Allah:**

Zama za Isa baada ya kumuua Dajjali ni zama za imani, starehe na ukunjufu wa maisha, Allah atatuma mvua ambayo haitasitirika nayo nyumba ya udongo wala ya sufi, na itaambiwa: otesha matunda yako na rudisha baraka zako, basi siku hiyo kundi la watu watakula kokomanga [komamanga/kudhumani] moja [washibe], na watawekea uvuli kwa ganda lake.

Maziwa yatabarikiwa hadi iwe ngamia wa maziwa mmoja anawatosha kundi kubwa la watu, na ng'ombe wa maziwa mmoja atatosha kabila la watu, na mbuzi mmoja wa maziwa atatosha ukoo [ambao ni chini ya kabila], na amani ienee katika ardhri; basi simba walishe pamoja na ngamia, na chui pamoja na ngo'mbe, na mbwamwitu pamoja na mbuzi, na watoto wacheze na nyoka wala wasiwadhuru.

Baada Isa [salamu zimshukie] kukaa katika ardhi miaka saba Allah atatuma upepo baridi kutoka upande wa Shaam, asibakie yeyote juu ya uso wa ardhi ambaye moyoni mwake mna imani uzito wa chembe ya mchanga ila utamkabidhi [roho yake].

Na Kiyama kisimame na hali hakuna juu ya uso wa ardhi anayesema: Allah Allah, na jua lichomoze upande wa magharibi, basi pindi litakapotoka [upande huo] na watu walione hapo wataamini wote; «**basi huo ni wakati ambao**

﴿لَا يَنفَعُ نَفْسًا إِيمَٰنُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِن قَبْلُ﴾

{Kuamini hapo hakutomfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake} [Al-An'aam: 158]».

Na kila moyo ufungwe na yale yaliomo ndani yake, na watu watoshelezwe jukumu la kufanya amali.

Alama kubwa ya mwisho ya Kiyama, na ya kwanza yenye kutangaza kusimama Kiyama ni: Moto mkubwa utakaotoka Yemen, utakaowafukuza watu hadi uwanja wao wa kukusanya, unatulia mchana nao wanapotulia, unalala nao wanapolala, unapambazuka nao wanapopambazuka, na unatembea nao wanapotembea.

**Ama baada ya haya, enyi Waislamu:**

Basi ahadi ya Allah ni haki, na Kiyama kinakuja hakuna shaka ndani yake, na dunia imetangaza kumalizika, na imegeuka kuondoka kwa haraka, na Kiyama kimekurubia, na aliyeghafilika na nafsi yake wakati wake utaisha kisha hasara zake zitakuwa kubwa.

Matamanio yanakunjwa na miaka inaisha, na aliyerefusha kutamani husahau amali, na hughafilika na ajali yake, na mwangaza wa asubuhi ya kila siku unakutangazia kifo, basi mwema ni yule aliyeandaa maandalizi na akajiandaa kuondoka, baadhi ya wenye hekima walisema: "Nastaajabu na yule anayehuzunika kwa kupungukiwa na mali yake wala hahuziniki kwa kupungua umri wake."

Basi jitahidi katika ibada, lilia makosa yako na ikimbie adhabu; kwani aliyeafikiwa ni yule aliye na matamanio katika yenye kubaki [Akhera], na akakata [matamanio] na yale yenye kuisha [dunia], pindi mauti yalipomfikia Muhammad ibnu Siriin alilia, akaambiwa: "Ni lipi linalokuliza? Akasema: Nalilia kasoro yangu katika masiku yaliopita, na uchache wa amali yangu yakunifikisha katika Pepo ya juu."

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Mtume mbashiri, na mwonyaji...

## MASIHI DAJJALI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii**:

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani atakayemcha Yeye humwongoza, na atakayekimbilia kwake Yeye humuhifadhi na humlinda.

**Enyi Waislamu:**

Allah ameujaalia umma huu kuwa umma wa mwisho, na ndani yake [umma huu] zitadhihiri alama za Kiyama, na juu yake Kitasimama Kiyama, Allah aliyetakasika ametolea habari ya kukurubia hilo; akasema:

﴿ٱقۡتَرَبَتِ ٱلسَّاعَةُ وَٱنشَقَّ ٱلۡقَمَرُ﴾

{Kiyama kimekaribia, na mwezi umepasuka!} [Al-Qamar: 1].

Na «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa anapotaja Kiyama, macho yake yawa mekundu, na sauti yake inanyanyuka, na ghadhabu yake huzidi, hadi utaona kana kwamba anatahadharisha [watu wake] jeshi [linalotaka kuwavamia], anasema: Wanawaingilia asubuhi, wanaingilia jioni», imepokewa na Muslim.

Washirikina walimuuliza Nabii swala na salamu za Allah zimshukie kwa kukariri kuhusu wakati wa kusimama Kiyama, Mola wake Mlezi akamwambia:

﴿يَسۡـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلسَّاعَةِ أَيَّانَ مُرۡسَىٰهَاۖ قُلۡ إِنَّمَا عِلۡمُهَا عِندَ رَبِّيۖ لَا يُجَلِّيهَا لِوَقۡتِهَآ إِلَّا هُوَ﴾

{Wanakuuliza hiyo Saa [ya Kiyama] itakuwa lini? Sema: Kuijua kwake kuko kwa Mola wangu Mlezi. Haidhihirishi hiyo kwa wakati wake ila Yeye} [Al-A'raf: 187].

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na mbili ya mwezi wa Muharram, mwaka elfu moja mia nne na thelathini na tano hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Ni katika rehema zake [Allah] aliyetakasika: kuwa amejaalia Kiyama kuwa na alama zinazotokea kabla kusimama kwake; ili watu warudi kwa Mola wao Mlezi, na [Allah] aliyetukuka akatoa habari za kuhusu alama za kukurubia kwake; akasema:

﴿فَهَلۡ يَنظُرُونَ إِلَّا ٱلسَّاعَةَ أَن تَأۡتِيَهُم بَغۡتَةٗۖ فَقَدۡ جَآءَ أَشۡرَاطُهَا﴾

{Kwani wanangojea jengine isipokuwa iwafikie Saa [ya Kiyama] kwa ghafla? Na hakika alama zake zimekwisha kuja} [Muhammad: 18].

Alama kubwa za Kiyama zikitokea, basi nyingine zinafuatia nyuma yake ikiwa karibu nazo.

Kuna jambo kubwa Allah amelijalia ni katika alama za Kiyama, hakuna Nabii ila alitahadharisha umma wake kutokana nalo, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Allah hajamtuma Nabii yeyote ila alitahadharisha umma wake, Nuuh na Manabii baada yake walitahadharisha** [jambo hilo]», imepokewa na Bukhari, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alitahadharisha umma wake, akasema: «**Hakika mimi nawatahadharisheni** [na jambo hilo]», imepokewa na Bukhari.

[Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiomba ulinzi ndani ya swala yake kutokana na fitina yake [dajjali], na akiwafundisha masahaba wake kuomba ulinzi kutokana nalo kama anavyowafundisha sura ya Qur-ani, na awapa mawaidha masahaba na akiwapa habari ya kukurubia kudhihiri jambo hilo, An-Nawwaas ibnu Sam'aan amesema: «Hadi tukadhani yupo katika upande wa mitetende - yaani: katika mitende iliyokuwa ubavuni mwao -», imepokewa na Muslim.

Wema waliotangulia walikuwa wakiamrisha kukumbusha [watu] jambo hili mara kwa mara, As-Saffaariiny Allah amrehemu amesema: "Inampasa kila mwanachuoni anushuru hadithi za Dajjali baina ya watoto, wanawake na wanaume, sana sana katika zama zetu hizi ambazo fitina zimeinuka ndani yake, na mitihani imekithiri ndani yake, na athari za Sunnah zimefutika."

Dajjali saa hii yupo hai katika kisiwa miongoni mwa visiwa vya baharini, amefungwa kwa vifungo vigumu, mikono yake imekusanya katika shingo yake, yakiwa baina ya magoti yake na vifundo vya miguu yake, yamefungwa kwa chuma, na kutoka kwake kumekurubia; alisema kuhusu nafsi yake: «Na hakika mimi nimekurubia kuidhinishwa kutoka», imepokewa na Muslim.

Alama ya kutoka kwake: ni mitetende ya Baysaan - nao ni mji baina ya Mji wa Hawraan na Palestina - iache kuzaa matunda baada kuwa yakizaa, Yaquut Al-Hamawy amesema: "Hakika nimeiona mara kwa mara; na sijaona

kati yake isiokuwa mitetende miwili ambayo hayakuzaa."

Na miongoni mwa alama za kutoka kwake: Kuisha maji ya ziwa la Twabariyya, na maji yake hivi sasa yamekuwa machache, nalo linazidi kupungua.

Na ni miongoni mwa alama zake: Kuisha maji ya mto wa Zughar - mji katika Shaam -, na kutolima watu wake na maji ya mto huo.

Mwanzo wa kutoka kwake ni kutoka kijiji kinachoitwa "Al-Yahuudiyyah", katika mji wa Asbahaan kutoka ardhi za Khuraasaan, atatoka wakiwa naye mayahudi elfu sabiini wa mji huo, naye ako na walinzi na wasaidizi.

Naye ni barobaro mwekundu, mwenye mwili na umbile kubwa, mwenye komo pana, anao kuinama, mwenye nywele nyingi ngumu, kana kwamba jicho lake ni zabibu iliyoharibika, Tamim Ad-Daary Allah amridhie alisema naye alimwona: «Ni mtu mkubwa zaidi kimaumbile tuliowahi kumwona», naye ndio kiumbe katika huu ulimwengu; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Baina ya kuumbwa Adam hadi kusimama kwa Kiyama hakuna kiumbe kikubwa kuliko Dajjali**», imepokewa na Muslim.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alibainisha sifa zake ili watu wamjue pindi atakapotoka, na kuwa yeye ni Dajjali wala si Mola Mlezi wa walimwengu kama anavyodai; na kwa kuwa Dajjali atatoka katika umma huu Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alituhadithia sifa ambayo hajawahi yeyote katika Manabii kuitaja, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Nitawaambia kauli kumhusu ambayo hajawahi Nabii yeyoto kuwaambia kaumu yake, jueni kuwa yeye ni chongo, na Allah si chongo**», imepokewa na Bukhari.

Kutoka kwake ni katika hali ya kufifia kwa dini na kuondoka kwa elimu; ili atofautike muumini kutokana na Kafiri, na abainike Mwislamu kutokana na aliye na shaka, basi atadai kuwa yeye ni Mola Mlezi wa walimwengu, na waja watafitinika naye kwa ajili ya mambo aliyojaaliwa na Allah miongoni mwa mambo yanayovuka ada za kilimwengu.

Ni katika fitina yake kuwa ataua mtu kisha atamhuisha - kwa idhini ya Allah -, na atampiga mwengine upanga amkate vipande viwili, kisha baada ya kumuua atamuita, basi yule aliyeuliwa asimame kumjia hali uso wake ukimemetuka, na atamkata mtu kwa msumeno kutoka utosini mwake hadi amkate baina ya miguu yake miwili, kisha Dajjali atembee baina ya vipande viwili hivyo, kisha amwambie: Simama, basi yule mtu astawi hali ya kusimama. Na atamshika mtu kwa miguu yake miwili na mikono yake miwili

na amtupe ndani ya moto alionao, basi idhaniwe kuwa amemtupa motoni, na hakika si mengine ametiwa Peponi - kwani moto wake ni Pepo na Pepo yake ni Moto.

Anao pamoja naye mito miwili inayotembea, mmojawapo: kwa mtazamo wa jicho ni maji meupe, na mwengine kwa mtazamo wa jicho ni moto unaorurumba; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Mmoja wenu akikuta hayo basi aujie mto anaouona kuwa ni moto, na afunge macho, kisha ainamishe kichwa chake na anywe; kwani hakika huo ni maji baridi**», imepokewa na Muslim.

Ataiamrisha mbingu inyeshe nayo itanyesha, na ardhi ioteshe mimea nayo itaotesha, na atapita katika gofu alimbiye: toa kanzi zako, basi kanzi zake zimfuate, ibnul Araby amesema: "Na hayo yote ni mambo ya kuogopewa."

Kutembea kwake juu ya ardhi ni kwa kasi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliuelezea mwendo wake kwa kauli: «**Ni kama mvua inayosukumwa na upepo**», imepokewa na Muslim.

Atakaa katika ardhi siku arubaini; siku moja ni kama mwaka, na siku moja ni kama mwezi, na siku moja ni kama wiki, na siku zake zilizosalia ni kama siku zetu, wala hataacha kijiji ila atakiingia isipokuwa Makkah na Madinah, kwani mnao Malaika juu ya kila mlango katika milango yake wanailinda, na akitaka kuingia mji mmoja kati ya hiyo miwili Malaika anamkabili akiwa na upanga mkononi mwake uliotolewa nje ya uo tayari kumzuia na kuingia.

Na miji yote inamuogopa Dajjali ila Madinah, haiingiwi na uoga wa Dajjali wala kumuogopa.

Ni katika kumshukuru Allah juu ya neema ya watu wa Makkah na Madinah: Ni waiimarishe kwa kumtii Allah; kule kuwa ameihusu na hifadhi yake kutokana na Dajjali, na atakapozuiliwa kuingia Madinah atashuka Jurf katika ardhi ambayo haijaimarishwa -upande wa magharibi wa jabali la uhud-, na aweke hapo bendera yake, na wengi watakaotoka kumuendea watakuwa wanawake, na Madinah itawatingisa watu wake mitingiso mitatu, watoke kuenda kwake [Dajjali] kila kafiri na mnafiki.

Watu bora katika kila zama na sehemu: ni yule anayekanusha maovu alioyaona; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ﴾

{Nyinyi mmekuwa umma bora waliotolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu} [Aalu Imraan: 110], na atakapokaa

nje ya Madinah atatoka barobaro amuendea kumkanusha kudai kwake uola na urongo wake uliopita mipaka; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Naye [barobaro huyo] ndio mbora wa watu [wakati huo] -** au **ni miongoni mwa watu bora -, basi aseme: «Nashuhudia kuwa wewe ni Dajjali ambaye tumehadithiwa habari yake na Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Hasara ya Waislamu kwa kufa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ni kubwa; kwani angekuwa hai angetutosheleza [shari] yake [Dajjali], [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Lau atatoka na mimi niko baina yenu basi mimi ndio nitakaye kuwa hasimu wake pasi na nyinyi**», imepokewa na Muslim, na baada ya kufa kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie basi kila mtu atajisimamia amri yake na yenye kumkinga na shari ya Dajjali, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: **«na akitoka nami siko baina yenu, basi kila mtu ajisimamie nafsi yake na Allah ndiye halifa wangu juu ya kila Mwislamu**», imepokewa na Muslim.

Katika sababu za kupata ulinzi kutokana naye ni: Elimu ya sheria kwa kutambua Majina ya Allah na Sifa zake, kwani Dajjali ni chongo, na Allah si chongo, na Allah haonekani na yeyote duniani, na Dajjali watu watamwona, na Dajjali ameandikwa baina ya macho yake *'Kaafir'*, ataisoma kila anayejua kusoma na asiyejua kusoma. Sheikul Islaam Allah amrehemu amesema: "Muumini anabainikiwa na yasiombainikia mwengine, hasa hasa katika fitina".

Kuzikimbia fitina na kuziepuka ni kinga kutokana nazo - kwa idhini ya Allah -; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Atakayemsikia Dajjali; basi amuepuke, naapa kwa Allah kuwa mtu humjia hali akidhania kuwa yeye ni muumini; kisha akamfuata kwa ajili ya shubuha anazozieneza**», imepokewa na Abu Daud.

Mnao katika kushikamana na dini kuokoka kutokana na Dajjali; kwani wafuasi wake si waumini, na kukithirisha maombi ya kutaka ulinzi kutokana naye ni ngome na amani, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Anapoleta *Tashahhudi* mmoja wenu - yaani: ndani ya swala - ; basi ajilinde na Allah kutokana na manne, aseme: Ewe Allah mimi najilinda nawe kutokana na adhabu ya jahanamu, na kutokana na adhabu ya kaburi, na kutokana na fitina ya uhai na kifo, na kutokana na fitina ya masihi Dajjali**», imepokewa na Muslim. Twauus Allah amrehemu alikuwa akimwamrisha mwanawe arudie kuswali tena endapo hakuisoma dua hii katika swala yake.

Qur-ani tukufu ni msingi wa ulinzi kutokana na kila fitina, na atakayesikia kuhusu kutoka kwake [Dajjali] na hali yeye amehifadhi aya kumi za mwanzo wa suratul Kahf atalindwa kutokana naye - kwa idhini ya Allah - , na atakayemwona basi amsomee aya za mwazo wa suratul Kahf, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Basi atakayekutana naye miongoni mwenu; basi amsomee aya za mwanzo wa suratul Kahf**», imepokewa na Muslim.

Watakapokithiri wafuasi wake na fitina yake ikawa kubwa, basi hapo atateremka Isa [salamu zimshukie] katika mnara wa mashariki ya 'Dimishk', basi waja wa Allah wamzunguke ubavuni mwake, basi Isa [salamu zimshukie] amfukuze Dajjali pindi atakapokuwa anaelekea 'Baytul Maqdis', basi amdiriki akiwa katika 'Baab Ludd' huko Palestina, basi Dajjali atakapomwona [Isa] atayayuka kama inavyoyayuka chumvi [ndani ya maji], basi Isa amfukuze na amuue kwa mkuki.

**Na baada ya haya, enyi Waislamu:**

Basi ahadi ya Allah ni haki, na Kiyama kinakuja hamna shaka ndani yake, na kusimama kwake ni kwa haraka; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: **«Kiyama kitasimama na mtu anakama ngamia wa maziwa, basi chombo [cha maziwa] hakitafika mdomoni tayari kitakuwa kimesimama, na watu wawili watakuwa wanauziana nguo, basi hawatamaliza kuuziana tayari kitakuwa kimesimama, na mtu atakuwa anatengeneza birika lake, basi hamalizi hadi kitakuwa kimesimama**», imepokewa na Muslim.

Mwislamu ni mwenye kukimbilia kufanya mema katika kila wakati, naye hutekeleza mema zaidi na kukithirisha katika kipindi cha ugeni wa dini na wingi wa fitina; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Harakisheni kutenda amali kabla ya mambo sita: Kuchomoza jua kutoka magharibi yake, au moshi, au Dajjali, au mnyama** [atakayezungumzisha watu]**, au jambo linalomhusu mmoja wenu** [kama vile kifo, au yenye kumshughulisha katika nafsi yake, au mali yake au yenye kumtia hamu], **au jambo la jumla** [kama vile uongozi au Kiyama]», imepokewa na Muslim.

Kumtii Nabii swala na salamu za Allah zimshukie ni hifadhi kwa mja katika raha na shida, Dajjali alimuuliza Tamimi Ad-Daary na waliokuwa naye miongoni mwa Mashaba pindi walipomwona; aliwauliza kuhusu Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «Amefanyaje? Wakasema: ametoka Makkah na ameshukia Yathrib. Akasema: Waarabu wamempiga vita? Wakasema: Ndio. Akasema: Yeye amewafanyaje nini? Wakampa habari kuwe yeye amenusuriwa juu ya wale waliokaribu naye na waarabu wamemtii.

Akawaambia: Limeshakuwa hilo? Wakasema: Ndio. Ama hilo ni heri kwao wamtii», imepokewa na Muslim.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿ٱقۡتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمۡ وَهُمۡ فِي غَفۡلَةٖ مُّعۡرِضُونَ﴾

{Imewakaribia watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala wanapuuza} [Al-Anbiyaa: 1].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Na hata likiwa jambo la Dajjali ni kubwa, kwa hakika riya katika amali ni ya kuogopesha zaidi mbele ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie juu ya umma wake kuliko Dajjali; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Siwajulisheni jambo ambalo nalihofia zaidi juu yenu kuliko masihi Dajjali? Wakasema: kwa nini [yaani: tujulishe], akasema: Ni shirki iliyofichika; ni asimame mtu kuswali, basi aipambe swala yake kwa ajili ameona mtu anamwangalia**», imepokewa na Ahmad, amesema [sheikh Suleiman] katika [kitabu chake] *'Taysiirul aziizil hamiid'*: "Hakika riya imekuwa hivyo kwa ajili ya kufichika kwake, na nguvu yenye kulingania kwake, na uzito wa kujisalimisha nayo; kwa ajili ya anayoyapamba shetani na nafsi yenye kuamrisha maovu ndani ya moyo wake", na muumini hukusanya katika amali yake baina ya uzuri wa amali kwa kumwandama Nabii swala na salamu za Allah zimshukie na kuitakasa nia ndani yake kwa Allah peke yake.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## SIKU YA MWISHO: SIKU YA MALIPO[1].

Sifa njema zote anastahiki Allah, ambaye kwa neema yake ndio wameongoka walioongoka, na kwa uadilifu wake wamepotea waliopotea, haulizwi analolifanya, nao [viumbe] ndio wanaoulizwa, namhimdi Yeye aliyetakasika himdi ya mja aliyemtakasa Mola wake Mlezi kutokana na wanayoyasema madhalimu.

Nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika, shahada ambayo waliiridhia watu wema.

Na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake mkweli aliye mwaminifu, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, watu wake na masahaba wake ambao wao ndio walioshikamana na uongofu wake na wanaotembea katika njia yake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi nawausia nyinyi na nafsi yangu kumcha Allah; kwani kumcha Yeye ndio uongofu kesho [siku ya Kiyama] na saada ya milele.

**Enyi Waislamu**:

Kusadikisha siku ya mwisho ni miongoni mwa misingi ya Imani ambayo Mitume wote waliilingania. Hakika manabii waliwafikishia kaumu zao [habari ya] siku ya mwisho tulioahidiwa, na wakawabashiria Pepo na wakawahofisha Moto, na sifa ya kwanza miongoni mwa sifa za wachamngu katika Kitabu cha Allah: ni kuamini ghaibu:

﴿ذَٰلِكَ ٱلۡكِتَٰبُ لَا رَيۡبَۛ فِيهِۛ هُدٗى لِّلۡمُتَّقِينَ * ٱلَّذِينَ يُؤۡمِنُونَ بِٱلۡغَيۡبِ﴾

{Hiki ni Kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake; ni uongofu kwa wachamungu * Ambao huyaamini ya ghaibu} [Al-Baqarah: 2-3].

Pindi Adam [salamu zimshukie] alipoteremshwa ardhini Allah alimwambia:

﴿فِيهَا تَحۡيَوۡنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنۡهَا تُخۡرَجُونَ﴾

{Humo mtaishi, na humo mtakufa, na kutoka humo mtatolewa} [Al-A'raf: 25],

Nuuh [salamu zimshukie] aliwatahadharisha kaumu yake na Siku ya

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na moja ya mwezi wa Muharram, mwaka elfu moja mia nne na ishirini hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

malipo, na akawapigia mifano yenye kujulisha [ukweli wa] kutokezea kwake [siku ya malipo]; akasema:

﴿وَٱللَّهُ أَنۢبَتَكُم مِّنَ ٱلۡأَرۡضِ نَبَاتٗا * ثُمَّ يُعِيدُكُمۡ فِيهَا وَيُخۡرِجُكُمۡ إِخۡرَاجٗا﴾

{Na Allah amekuotesheni katika ardhi kama mimea * Kisha atakurudsheni humo na atakutoeni tena} [Nuuh: 17-18].

Na Shueib [salamu zimshukie] aliwaambia kaumu yake:

﴿ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَٱرۡجُواْ ٱلۡيَوۡمَ ٱلۡأٓخِرَ وَلَا تَعۡثَوۡاْ فِي ٱلۡأَرۡضِ مُفۡسِدِينَ﴾

{Mwabuduni Allah na iogopeni Siku ya Akhera, wala msiende katika ardhi mkifisidi} [Al-Ankabuut: 36],

Muda wa mja katika maisha haya [ya duniani] ni mfupi, na masiku yake katika ulimwengu huu wakuisha yana kikomo, na haja zake juu ya ardhi haziishi, na matamanio yake ni marefu, na ataondoka na hali ndani ya nafsi yake mnao mahitaji, na juu ya ardhi aliyoiacha mnao matamanio yake, na hakika itakuja siku ambayo ndani yake maisha yataisha na vilivyohai vitaisha; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿كُلُّ شَيۡءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجۡهَهُۥ﴾

{Kila kitu kitaangamia isipokuwa Yeye} [Al-Qaswas: 88].

Kisha itakuja wakati ambao Allah atawarudisha ndani yake waja na awafufue, na awasimamishe mbele yake na awahasibu katika amali walizozitanguliza, na waja siku hiyo watakutana na vitisho vikubwa, hatasalimika navyo ila yule aliyeiandalia siku hiyo maandalizi yake - miongoni mwa imani na amali njema -, na mwisho wa hilo waja watapelekwa makazini mao, Pepo au Moto.

Siku hii ni siku ya Kiyama; ni siku inayogonga nyoyo, na inapasua masikio hadi ikurubie kuyatia uziwi masikio, ni siku ngumu imejaa kila jambo la kutisha, na inafunika watu kwa hofu zao:

﴿هَلۡ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ٱلۡغَٰشِيَةِ﴾

{Je! Imekufikia khabari ya msiba wa kufudikiza} [Al-Ghaashiya: 1],

Waja wataona hasara na watajuta ndani yake:

﴿وَأَنذِرۡهُمۡ يَوۡمَ ٱلۡحَسۡرَةِ إِذۡ قُضِيَ ٱلۡأَمۡرُ وَهُمۡ فِي غَفۡلَةٖ وَهُمۡ لَا يُؤۡمِنُونَ﴾

{Na waonye siku ya majuto itakapokatwa amri. Nao wamo katika mghafala, wala hawaamini} [Maryam: 39],

na nafsi iseme:

﴿يَٰحَسۡرَتَىٰ عَلَىٰ مَا فَرَّطتُ فِي جَنۢبِ ٱللَّهِ وَإِن كُنتُ لَمِنَ ٱلسَّٰخِرِينَ﴾

{Ee majuto yangu kwa yale niliyo poteza upande wa Allah, na hakika nilikuwa miongoni mwa wanao fanya maskhara!} [Az-Zumar: 56].

Hasara itafikia kileleni mwake kwa watu wa kufuru pindi viongozi watakapowakana wafuasi wao:

﴿وَقَالَ ٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُواْ لَوۡ أَنَّ لَنَا كَرَّةٗ فَنَتَبَرَّأَ مِنۡهُمۡ كَمَا تَبَرَّءُواْ مِنَّاۗ كَذَٰلِكَ يُرِيهِمُ ٱللَّهُ أَعۡمَٰلَهُمۡ حَسَرَٰتٍ عَلَيۡهِمۡۖ وَمَا هُم بِخَٰرِجِينَ مِنَ ٱلنَّارِ﴾

{Na watasema wale waliofuata: Laiti tungeweza kurudi tukawakataa wao kama wanavyotukataa sisi! Hivi ndivyo Allah atakavyowaonyesha vitendo vyao kuwa majuto yao; wala hawatakuwa wenye kutoka Motoni} [Al-Baqarah: 167].

Itakithiri ndani yake [siku hiyo] kuitana, kila mtu ataitwa kwa jina lake kwa ajili [ya kuhudhuria] hesabu na malipo [yake], na watu wa Peponi watawaita watu wa Motoni, na watu wa Motoni watawaita watu wa Peponi, na watu A'raaf [sehemu ilionyanyuka baina Pepo na Moto] watawaita hawa [watu wa Peponi] na hawa [watu wa Motoni]:

﴿ذَٰلِكَ يَوۡمٞ مَّجۡمُوعٞ لَّهُ ٱلنَّاسُ وَذَٰلِكَ يَوۡمٞ مَّشۡهُودٞ﴾

{Hiyo ndiyo siku itakayo kusanyiwa watu, na hiyo ndiyo siku itakayoshuhudiwa} [Huud: 103].

Hakika hiyo ni ya kupunjana; ndani yake watu Peponi watawapunja watu wa Motoni; kwani hawa wataingi Peponi na wachukue walioandaliwa na Allah, na warithi sehemu za makafiri Peponi, na itimie ndani yake ahadi njema na makemeo, na yatadhihiri ndani yake mambo na yaliofichika vifuani. Siku ambayo yatafufuliwa makaburi na yatatolewa yaliomo ndani ya vifua, ni siku ngumu kwa makafiri sio nyepesi, ndani yake binadamu atapewa habari ya aliyoyatanguliza na aliyoyacheleweshа.

**Enyi Waislamu**:

Baina ya kuwa watu wako katika kushughulika na mali yao na maisha yao wanazozana na wanalumbana, mara tu kumepulizwa parapanda, basi kusibaki yeyote juu ya mgongo wa ardhi, «**ila atateremsha ubavu wa shingo na anyanyue upande mwengine wa shingo**, anasikiliza sauti kutoka mbinguni, basi hatamakinika kuandika wasia wala kurudi kwa watu wake [nyumbani]; [Allah] aliyetukuka anasema:

﴿مَا يَنظُرُونَ إِلَّا صَيۡحَةٗ وَٰحِدَةٗ تَأۡخُذُهُمۡ وَهُمۡ يَخِصِّمُونَ ۝﴾

﴿فَلَا يَسۡتَطِيعُونَ تَوۡصِيَةٗ وَلَآ إِلَىٰٓ أَهۡلِهِمۡ يَرۡجِعُونَ﴾

{Hawangojei ila ukelele mmoja tu utakaowachukua nao wamo kuzozana * Basi hawataweza kuusia, wala kwa watu wao hawarejei} [Yaasiin: 49-50].

«**Na wa kwanza atakayeusikia [ukelele wa parapanda] ni mtu atakayekuwa akitengeneza birika la [kunywesha] ngamia wake, asema: basi afe na watu wote wafe**», na katika Hadithi: «**Hakika Kiyama kitasimama na watu wawili tayari wametandaza nguo yao baina yao** [ili kuuziana]**; basi hawatauziana wala hawataikunja, na hakika Kiyama kitasimama na mtu ameondoka na maziwa ya ngamia wake; wala asiyanywe, na hakika Kiyama kitasimama naye akitengeneza birika yake; wala asinyeshe ndani yake, na hakika Kiyama kitasimama na hali amenyanyua chakula chake mdomoni; wala asikile**», imepokewa na Bukhari.

**Enyi waja wa Allah**:

Parapanda ni pembe inayovuviwa ndani yake, na mwenye parapanda yuko tayari kuvuvia ndani yake kutoka Allah amuumbe, anaangalia upande wa Arshi kwa hofu isije akamrishwa [kuvuvia] kabla ya kupepesa jicho lake; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Vipi nijineemeshe na hali mwenye pembe ameshaitia mdomoni, na ameinamisha paji lake, na ametuliza sikio lake kusikiliza, anangojea kuamrishwa kupuliza; ndio apulize**! Waislamu wakasema: Ewe Mtume wa Allah! Tusemeje? Akasema: "**Semeni: '*Hasbuna llahu wa ni' mal wakiil, tawakkalna ala llahi rabbinaa*' - Allah anatutoshelaza naye ni mbora wa kuwakilishwa, tumemtegemea Allah Mola wetu Mlezi -**», imepokewa na Tirmidhi.

**Enyi Waislamu**:

Kiyama kitasimama siku ya ijumaa, na katika kila siku ya ijumaa viumbe vyote vinahofu kutokea jua lichomoze hadi lichwe, ila binadamu na majini; wakihofia kusimama Kiyama ndani ya siku hiyo, na pindi Allah atataka kuwarudisha waja na kuwahuisha atamwamrisha Israafil akapulize katika parapanda, basi roho zirudi katika miili yake, na watu wamsimamie Mola Mlezi wa walimwengu:

﴿وَنُفِخَ فِي ٱلصُّورِ فَإِذَا هُم مِّنَ ٱلۡأَجۡدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمۡ يَنسِلُونَ﴾

{Na litapulizwa parapanda, mara watatoka makaburini wakikimbilia kwa Mola wao Mlezi} [Yaasiin: 51].

Mtu wa kwanza atakayeamka na wa kwanza ambaye ardhi itapasuka atoke ni: Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie.

Baada ya mpulizo wa kufa Allah atateremsha maji kutoka mbinguni ambayo yataota kwayo miili ya waja kama inavyoota mimea, hakuna kitu katika [mwili wa] binadamu ila kilioza isipokuwa kifandugu [kifupa cha mwisho wa uti wa mgongo], na kutokana nacho ndio litapandanishwa umbile [la binadamu] siku ya Kiyama.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿وَأَنذِرْهُمْ يَوْمَ ٱلْـَٔازِفَةِ إِذِ ٱلْقُلُوبُ لَدَى ٱلْحَنَاجِرِ كَـٰظِمِينَ ۚ مَا لِلظَّـٰلِمِينَ مِنْ حَمِيمٍ وَلَا شَفِيعٍ يُطَاعُ﴾

{Na waonye siku inayokurubia, wakati nyoyo zitakapofika kooni, nao wamejaa huzuni. Madhaalimu hawatakuwa na rafiki, wala mwombezi wa kuitikiwa} [Ghaafir: 18].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu**:

Allah atawakusanya waja wote siku ya malipo, na katika mkusanyiko watakuwa sawa wa mwanzo na wa mwisho:

﴿قُلۡ إِنَّ ٱلۡأَوَّلِينَ وَٱلۡأٓخِرِينَ * لَمَجۡمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَٰتِ يَوۡمٖ مَّعۡلُومٖ﴾

{Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho * Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu} [Al-Waaqi'a: 49-50].

Namna yoyote waliokufa waja - ndani ya giza la bahari, au ndani ya matumbo ya wanyama mwitu, au chini ya ardhi - basi hakika Allah ni muweza wa kuwaleta:

﴿أَيۡنَ مَا تَكُونُواْ يَأۡتِ بِكُمُ ٱللَّهُ جَمِيعًاۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٞ﴾

{Popote mulipo Allah atakuleteni nyote. Hakika Allah ni Muweza wa kila kitu} [Al-Baqarah: 148].

Elimu ya Allah aliyetukuka imewazunguka popote walipokufa na vyovyote vile walivyoangamia, hakuna yeyote miongoni mwao atasahaulika kukusanywa [siku ya Kiyama], wala hatakosekana katika kisimamo hicho mtu yeyote, [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَحَشَرۡنَٰهُمۡ فَلَمۡ نُغَادِرۡ مِنۡهُمۡ أَحَدٗا﴾

{na tukawafufua -wala hatutamwacha hata mmoja kati yao-} [Al-Kahf: 47].

Akasema tena Allah aliyetakasika:

﴿إِن كُلُّ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِ إِلَّآ ءَاتِي ٱلرَّحۡمَٰنِ عَبۡدٗا * لَّقَدۡ أَحۡصَىٰهُمۡ وَعَدَّهُمۡ عَدّٗا﴾

{Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Ar-Rahmaan Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa wake * Yeye hakika amewadhibiti na amewahisabu sawa sawa} [Maryam: 93-94].

Basi mche Allah na jaalia siku ya mwisho katika akili yako, na utajo wake katika ulimi wako, na jiandae nayo kwa imani na amali njema, na ishi

utakavyoishi hakika wewe utakufa, na penda utakachopenda hakika utakiepuka, na tenda utakalo hakika utalipwa, na jiandae na uchamngu hakika safari ni ya mbali, na jihafifishie mzigo kwani kizingiti ni kigumu kukipanda. Yahya ibnu Muadh Allah amrehemu anasema: "Anayo heri na saada aliyeiacha dunia kabla haijamuacha, na akajenga kaburi lake kabla hajaliingia, na akamridhisha Mola wake Mlezi kabla hajakutana naye."

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## VITISHO VYA SIKU YA KIYAMA[1].

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii**:

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na mchungeni katika siri na mnong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Watu katika maisha haya wamo ndani ya mghafala, na matamanio yao ndani yake ni mapana, na hapana budi kuitia hatamu nafsi kwa kuikumbusha inapoelekea; ili ipate kuimarisha Akhera kwa dunia, na apatilize muda uliopo kwa manufaa ya mustakabali, na Allah amejaalia kuwa na yakini ya siku ya mwisho ni katika nguzo za Imani, na itakuja siku ambayo viumbe wataisha ndani yake, kusadikisha kauli yake [Allah]:

﴿كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ﴾

{Kila kilioko juu yake kitatoweka} [Ar-Rahmaan: 26].

Kisha itakuja siku ambayo Allah atarudisha ndani yake waja na awafufue kutoka makaburini mwao.

Wa kwanza atakayefufuliwa na ardhi ipasuke kumtoa ni: Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie, na waja watafufuliwa wakiwa miguu tupu, uchi na hawajatahiriwa,

﴿كَمَا بَدَأْنَآ أَوَّلَ خَلْقٍ نُّعِيدُهُۥ﴾

{Kama tulivyoanza umbo la mwanzo tutalirudisha tena} [Al-Anbiyaa: 104],

Waja watavishwa, na wa kwanza kuvishwa ni Ibrahim [salamu zimshukie], na watu wema watavishwa nguo nzuri, na watu waovu

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe thalahini ya mwezi wa Rajab, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na moja hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

watavishwa nguo za shaba ilioyayushwa na nguo za upele, na viumbe watafufulia katika ardhi ya kukusanywa sio hii; Aisha Allah amridhie amesema: «Ewe Mtume wa Allah! Watu watakuwa wapi [wakati itakapobadilishwa ardhi]? Akasema: "**Juu ya *'Swiraat'*** [Sirati]"», imepokewa na Muslim, na katika tamshi [lingine]: «**watakuwa katika giza kabla ya daraja**.»

Ardhi ya kukusanya ni nyeupe, hamna juu yake alama ya mtu yeyote, hakujamwagwa juu yake damu ya haramu wala hakujafanywa kosa juu yake, jicho linawaona wote, na mwenye kuita anawasikizisha, ni siku yenye shida na taabu, makafiri walisema kuihusu:

﴿هَٰذَا يَوۡمٌ عَسِرٞ﴾

{Hii ni siku ngumu} [Al-Qamar: 8].

Waja hawatapata siku mfano wake, Allah ameisifu na uzito na ugumu, kwa ajili yake nywele za mtoto mchanga zinatokwa na mvi:

﴿فَذَٰلِكَ يَوۡمَئِذٖ يَوۡمٌ عَسِيرٌ﴾

{Siku hiyo, basi, itakuwa siku ngumu} [Al-Muddaththir: 9].

Mwenye kunyonyesha atamsahau anayemnyonyesha, na mwenye mimba ataangusha mimba yake.

Ni siku ambayo akili zinapigwa na butwaa ndani yake, na akili zinapotea, binadamu atamkimbia mtu anayempenda zaidi - miongoni mwa mamake, babake, ndugu yake, mke wake na watoto wake -. Aliyeasi atatamani awatie Motoni watu walioghali zaidi kwake ili yeye aokoke:

﴿يُبَصَّرُونَهُمۡۚ يَوَدُّ ٱلۡمُجۡرِمُ لَوۡ يَفۡتَدِي مِنۡ عَذَابِ يَوۡمِئِذِۭ بِبَنِيهِ * وَصَٰحِبَتِهِۦ وَأَخِيهِ * وَفَصِيلَتِهِ ٱلَّتِي تُـٔۡوِيهِ * وَمَن فِي ٱلۡأَرۡضِ جَمِيعٗا ثُمَّ يُنجِيهِ﴾

{Wataonyeshwa waonane [wasiulizane wala hilo lisiwashughulishe kitu, bali mmoja ashughulishwe na nafsi yake]. Atatamani mkosefu lau ajikomboe na adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa fidia wanawe * Na mkewe, na nduguye * Na jamaa zake waliokuwa wakimkimu * Na wote waliomo duniani, kisha aokoke yeye} [Al-Ma'arij: 11-14].

Ardhi itatetemeshwa na itavunjwavunjwa mara moja, na itatandikwa kama ngozi, na itakuwa uwanja mmoja hamna kombo ndani yake wala miinuko, Allah ataikabidhi na aishike kwa kidole kimoja.

Majabali yatang'olewa na yatakuwa chengachenga, na yatakuwa kama tifutifu la mchanga ulioenea, na kama aina za sufi zilizochambuliwa, na

mwenye kuona anasawirishiwa kuwa ni kitu nayo ni sarabi si chochote:

﴿وَسُيِّرَتِ ٱلْجِبَالُ فَكَانَتْ سَرَابًا﴾

{na majabali yataondolewa na yatakuwa kama sarabi} [An-Naba': 20].

Majabali yataondolewa sehemu zake, na yatasawazishwa na ardhi, basi hapatabaki miinuko ndani yake wala miteremko

﴿لَّا تَرَىٰ فِيهَا عِوَجًا وَلَآ أَمْتًا﴾

{hutaona humo mididimio wala muinuko} [Twaahaa: 107].

Bahari zitapasuliwa na zitawashwa moto. Mbingu nayo itapasuka na itatingisika; itakuwa dhaifu, na itabadilika rangi:

﴿فَإِذَا ٱنشَقَّتِ ٱلسَّمَآءُ فَكَانَتْ وَرْدَةً كَٱلدِّهَانِ﴾

{Itakapo pasuka mbingu ikawa nyekundu kama mafuta} [Ar-Rahmaan: 37]

Mbingu itakashifiwa na kusiwe na cha kuisitiri wala hakuna kufichika, na Mola wetu Mlezi ataikunja kwa mkono wake wa kuume kama vile mwenye kuandika anavyokunja nyaraka, na ataishika kwa kidole kimoja.

Jua nalo litakunjwa na likusanywe na mwangaza wake upotee, na mwezi nao utapoteza nuru yake:

﴿فَإِذَا بَرِقَ ٱلْبَصَرُ ۝ وَخَسَفَ ٱلْقَمَرُ ۝ وَجُمِعَ ٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ﴾

{Basi jicho litakapoduwaa * Na mwezi utapokosa nuru yake * Na likakusanywa jua na mwezi} [Al-Qiyaama: 7-9].

Nyota zenye kumemetuka nazo zitazima, na mashiko yake yatafunguka basi zisambaratike, na ardhi itande giza kwa sababu ya kuzima taa zake na kuondoka nuru zake.

Ngamia wenye mimba wataachwa bila kushughulikiwa, na wanyama mwitu watakusanywa, na viumbe watapigana mawimbi baadhi yao kwa baadhi, atakayewaona watu siku hiyo atadhani kuwa ni walevi na wala si walevi, lakini adhabu ya Allah ni kali.

Macho yamekodoka, na nyonyo zipo kooni zinapigapiga, na Malaika nao wamepiga safu wakiwatazama viumbe, ni jambo kubwa, na mgongo wenye kutisha, Nabii swala na salamu zimshukie anasema: «**Najilinda na Allah kutokana na dhiki ya kisimamo siku ya Kiyama**», imepokewa na An-Nasai.

Katika siku hii kila nafsi itajua ilichokihudhurisha [katika amali iliyozitanguliza], binadamu atasimama akijuta baada ya fursa kupotea, na

maficho ya nyoyo yatahesabiwa vikali na yatolewe yaliomo ndani yake, basi hakutakuwa na kitu kilichofichwa ndani yake ila kitadhihiri, na hakuna kilichofanywa kwa siri ila kitatangazwa, [kutakuwa na] kimya cha kutisha, hakuna mazungumzo baina yake wala hakikatishwi na kutoka udhuru:

﴿هَٰذَا يَوۡمُ لَا يَنطِقُونَ ۝ وَلَا يُؤۡذَنُ لَهُمۡ فَيَعۡتَذِرُونَ﴾

{Hii ni siku ambayo hawatatamka kitu * Wala hawataruhusiwa kutoa udhuru} [Al-Mursalaati: 35-36].

Kutakuwa na nyuso nyeupe zilizong'aa zenye bishara, zenye kucheka na zenye kumemetuka, na nyuso nyingine nyeusi zilizokunjana, zimetandwa na vumbi, zimefunikwa na giza tororo. Wachaji Allah watakusanywa kwa Mola wao Mlezi kimakundi, na waovu watakusanywa siku hiyo wakiwa rangi ya samawati.

Jua nalo litakurubia vichwa vya waja hadi kusiwe baina yake na baina yao ila kadri ya uti wa wanja, wala hakuna kivuli cha yeyote ila kivuli cha Arshi ya Ar-Rahmaan, basi kuna watakaokuwepo chini ya kivuli cha Arshi, na watakaodhihiri katika harara ya jua, na kaumu zitasongamana na zitasukumana, basi miguu itapitana na shingo zitakatika, na jasho litiririke hadi lifunike dhiraa sabiini chini ya ardhi, na lituame juu ya ardhi kisha lipande miili ya watu kwa kulingana na daraja zao, kuna ambao litawafikia katika kifundo cha mguu, na kunao watakaonyongwa sawa sawa; basi hamu itande, na nafsi idhikike, na kaumu zianguke kwa magoti kutokana na vitisho, na utaona kila kaumu imepiga goti; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Watu watafikwa na ghamu na majanga hali wasioiweza wala si wenye kuihimili**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Waasi watajuta na wataona hasara kwa upungufu wao katika ibada, na kwa ukubwa wa hasara yao watauma mikono yao; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu anasema:

﴿وَيَوۡمَ يَعَضُّ ٱلظَّالِمُ عَلَىٰ يَدَيۡهِ يَقُولُ يَٰلَيۡتَنِي ٱتَّخَذۡتُ مَعَ ٱلرَّسُولِ سَبِيلٗا﴾

{Na siku ambayo mwenye kudhulumu atajiuma mikono yake, na huku anasema: Laiti ningelishika njia pamoja na Mtume!} [Al-Furqan: 27],

Muasi ataichukia nafsi yake vipenzi vyake na wendani wake, na kila mapenzi ambayo hayakusimama juu ya msingi wa dini basi yatageuka kuwa uadui, na mtu atavijadili viungo vyake, na waliokuwa na kiburi watafufuliwa wakiwa mfano wa chungu wadogo wakikanyagwa na watu kwa nyao zao kwa kuwadhalilisha, na mwenye kupitisha nguo yake chini ya kifundo cha mguu Allah hatamzungumzisha siku hiyo wala hatamwangalia wala hatamtakasa na atakuwa na adhabu chungu.

Kila aliyefanya hiyana atawekewa bendera nyuma yake, na itasemwa: Hii ni hiyana ya fulani mwana wa fulani, na atakayechukua kitu katika ardhi pasi na haki siku ya Kiyama atadidimizwa ndani yake hadi afike ardhi ya saba, na dhuluma ya dunia siku ya Kiyama itakuwa maradufu: «**Dhuluma [hapa duniani] ni magiza mingi siku ya Kiyama**», na haki hazipotei; bali atalipwa kisasi mdhulimiwa haki yake kutoka kwa dhalimu, hadi kulipwe kisasi baina ya Wanyama.

Mtu wa shari zaidi siku hiyo ni: «**Mwenye nyuso mbili; mwenye kuwajia hawa kwa uso, na hawa [wengine] kwa uso mwengine», na «Atakayemwondoshea muumini janga katika majanga ya duniani; Allah atamwondoshea janga katika majanga ya siku ya Kiyama, na atakayemfanyia wepesi mwenye uzito; basi Allah atamfanyia wepesi duniani na Akhera, na atakayemsitiri Mwislamu; Allah atamsitiri duniani na Akhera**.»

Waadilifu watakuwa juu ya mimbari za nuru kuliani mwa Ar-Rahmaan, na kila mja atafufuliwa juu ya hali aliokufia; aliyekufa katika ihramu atafufuliwa akileta talbiya, na aliyejuruhiwa katika njia ya Allah atakuja hali ikiwa rangi ni rangi ya damu na harufu ni harufu ya miski, na wenye kuadhini ndio watu wenye shingo ndefu zaidi [siku ya Kiyama], wala hakuna yeyote atasikia upeo wa sauti yake ila atamtolea ushahidi siku ya Kiyama, na atakayetokwa na mvi ndani ya Uislamu utakuwa kwake ni nuru, na kila mtu atakuwa chini ya kivuli cha sadaka yake hadi kuhukumiwe baina ya watu.

Na *Swiraat* [Sirati] ni sehemu ya mtelezo; basi kuna atakayesalimika juu yake, na atakayenyanyurwa, na atakayetupwa ndani ya Moto.

Mizani [ya siku ya Kiyama] ni ya uadilifu haina kuharibika, na hesabu ndani ya siku hiyo ni kwa uzito wa chungu mdogo:

﴿فَمَن يَعۡمَلۡ مِثۡقَالَ ذَرَّةٍ خَيۡرٗا يَرَهُۥ ۞ وَمَن يَعۡمَلۡ مِثۡقَالَ ذَرَّةٖ شَرّٗا يَرَهُۥ﴾

{Basi anayetenda chembe ya wema, atauona! * Na anayetenda chembe ya uovu atauona!} [Az-Zalzala: 7-8].

[Dhikri ya] '*Al-Hamdu lillahi*' inaijaza [mizani], na '*Sub-hana llahi wa bihamdih, Sub-hana llahil adhwiim*' ni nzito ndani yake, na «Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa: ni jambo gani lenye kuingiza watu Peponi kwa wingi? Akasema: "**Uchaji Allah, na tabia njema**"», imepokewa na Tirmidhi.

Kurasa zilizokunjwa nazo zitanushuriwa, ni balaa ngapi ulizisahau?! Na ni maovu mangapi umeyaficha?! Na kitabu [cha matendo yako] kitasomwa, na viungo [vya watu] vitasemeshwa, na Malaika watahudhuria,

na Allah ni Mwenye kushuhudia amali zote, [Allah] aliyetukuka anasema:

﴿وَلَا تَعۡمَلُونَ مِنۡ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيۡكُمۡ شُهُودًا إِذۡ تُفِيضُونَ فِيهِ﴾

{Wala hamutendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo} [Yunus: 61].

Na baada ya Allah kumaliza kuhukumu baina ya wanyama ataanza kuhukumu baina ya waja. Na umma wa kwanza utakaohukumiwa baina yao ni umma huu [wa mwisho], nao ndio wa kwanza kuvuka *'Swiraat'* [Sirati], na wa mwanzo kuingia Peponi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Sisi ni wa mwisho [kuja duniani], watakaotangulia siku ya Kiyama**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na katika riwaya: «**Watakaohukumiwa kabla ya waja**», imepokewa na Muslim.

Na Allah atamkirimu mja wake Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie katika kisimamo kikubwa kwa kumpatia birika lenye kingo pana, [upana wake] ni mwendo wa kutembea mwezi, na maji yake ni meupe kushinda maziwa, tamu kuliko asali, na yenye harufu nzuri kuliko miski, utaona ndani yake mabuli ya dhahabu na fedha kwa idadi ya nyota za mbinguni.

Atakayekunywa mara moja hatashikwa na kiu baada yake milele, na watakuja watu katika umma wake [Mtume] kisha wazuiliwe, basi [Mtume] swala na salamu zimshukie aseme: «**"Hakika hawa ni katika mimi", isemwe [kujibiwa]: "Wewe haujui walizusha nini baada yako", basi [Mtume] aseme: "Mbali mbali kwa aliyebadilisha baada yangu"**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Hakika kuokoka kutokana na vitisho hivyo kunapatikana kwa rehema ya Allah kisha kwa amali njema, na mwenye kufanya upungufu atajuta hapana budi, katika siku ambayo kutoa udhuru hakunufaishi, wala hakutarajiwi siku hiyo isipokuwa msamaha. Na uhai uwe mrefu kwako au mfupi; bila shaka mwisho wako ni ima kuelekea Peponi au Motoni.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّ وَعۡدَ ٱللَّهِ حَقّٞۖ فَلَا تَغُرَّنَّكُمُ ٱلۡحَيَوٰةُ ٱلدُّنۡيَا وَلَا يَغُرَّنَّكُم بِٱللَّهِ ٱلۡغَرُورُ﴾

{Enyi watu! Hakika ahadi ya Allah ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala mdanganyifu [ibilisi] asikudanganyeni juu ya Allah} [Fatwir: 5].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Aliyefilisika siku ya Kiyama ni: yule atakayekuja na swala, saumu na zaka, na aje akiwa amemtusi huyu, amemtuhumu huyu, amekula mali ya huyu, amemwaga damu ya huyu, na amempiga huyu, basi apewe huyu mazuri yake, na huyu apewe katika mazuri yake, na endapo mazuri yake yataisha kabla madeni aliyonayo hayajaisha kulipwa; basi yatachukuliwa makosa yao atupiwe yeye kisha atupwe Motoni.

Swaleh Al-Murry Allah amrehemu asema: "Niliigia makaburini nusu mchana, basi nikaangalia makaburi kana kuwa ni watu walionyamaza, nikasema: Ametakasika ambaye atawahuisha na awafufue baada ya kipindi kirefu cha kuoza, basi nikapigiwa ukelele kutoka baadhi ya mashimo yale: Ewe Swaleh!

﴿وَمِنۡ ءَايَٰتِهِۦٓ أَن تَقُومَ ٱلسَّمَآءُ وَٱلۡأَرۡضُ بِأَمۡرِهِۦۚ ثُمَّ إِذَا دَعَاكُمۡ دَعۡوَةٗ مِّنَ ٱلۡأَرۡضِ إِذَآ أَنتُمۡ تَخۡرُجُونَ﴾

{Na katika aya zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa amri yake. Kisha atakapokuiteni mwito mmoja tu, hapo mtatoka kwenye ardhi} [Ar-Ruum: 25]. Asema: basi nikaanguka kuzimia."

Al-Hasan Al-Basriy Allah amrehemu: "Michana miwili na usiku miwili waja hawajawahi kusikia mfano wake katu: Usiku tutakaolala pamoja na watu wa makaburini, na hali hatujawahi kulala usiku kama huo kabla, na usiku ambao asubuhi yake itafungua siku ya Kiyama. Na siku ambayo atakujia mwenye kubashiria kutoka kwa Allah; ima bishara ya Pepo au ya Moto, na siku utakayopatiwa kitabu chako ima kwa mkono wa kuume au wa kushoto."

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# KUAMINI KADHAA NA QADAR

## TAWAKKUL (KUMTEGEMEA ALLAH)[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani atakayemcha Mola wake Mlezi atanyanyuka, na atakayempa mgongo basi atakuwa na maisha ya dhiki.

**Enyi Waislamu:**

Waja wenye saada zaidi ni wale wenye hadhi kubwa ya kumwabudu Allah, na kila mja akiwa mdhalilifu zaidi kwa Allah na mwenye kumhitajia Yeye zaidi basi atakuwa karibu zaidi naye na mwenye cheo kikubwa zaidi mbele yake [Allah] na mbele ya viumbe vyake. Na mja si mueza wa kupwekeka katika kujiletea maslahi na kujikinga na madhara, ni muhitaji wa kuomba msaada kutoka kwa Muumba wake. Allah aliyetakasika ndiye Mwenye kuelekewa katika kukidhi mahitaji na asiyemhitajia yeyote asiyekuwa Yeye, na kila asiyekuwa Yeye ni fukara kwake. Na madhambi ya waja ni mingi, wala hakuna kuokoka kutokana nayo ila kwa msaada wa Allah na msamaha wake, na katika mdhambi mengi makubwa ya kimoyo - miongoni mwa riya, kiburi, hasad na kuacha kumtegemea Allah - huenda mtu akayaingia hali yeye hayatambui, na huenda akajizuia na baadhi ya madhambi madogo ya dhahiri na hali yupo katika kughafilika na haya makubwa.

Na sababu tupu [zisizokuwa Pamoja nazo kumtegemea Allah] zinamfelisha mtu kutekeleza malengo yake, na huenda akabisha mlango akidhania kuwa ndani yake mna manufaa yake kumbe ni madhara matupu, wala hakuna la kuokoa kutokana na hali hiyo ila kumtegemea Mwenye ushindi na Mwenye kurehemu. Na kwa sababu hiyo, ndio Mola wetu Mlezi ameadhimisha shani ya kumtegemea Yeye, na akaijalia kuwa daraja katika

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi ya mwezi wa Jumaadal Akhir, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na nne hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

daraja za dini, na akaiambatisha na ibada katika kauli yake:

﴿فَٱعۡبُدۡهُ وَتَوَكَّلۡ عَلَيۡهِۚ﴾

{Basi mwabudu Yeye na umtegemee Yeye} [Huud: 123].

Na akaijalia kuwa sababu ya kupata mapenzi yake akasema:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلۡمُتَوَكِّلِينَ﴾

{Hakika Allah huwapenda wanaomtegemea} [Aalu Imraan: 159],

Na akaijaalia kuwa ni sharti la kupatikana imani, akasema:

﴿وَعَلَى ٱللَّهِ فَتَوَكَّلُوٓاْ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ﴾

{Na mtegemeeni Allah ikiwa nyinyi ni Waumini} [Al-Ma'idah: 23].

Ni makamu yenye cheo kitukufu, yenye athari kubwa, na faradhi ya kutoka kwa Mola Mlezi wa walimwengu, kwayo zinapatikana radhi za Ar-Rahmaan, na mnao ndani yake kinga kutokana na shetani, cheo chake ndio cheo kikunjufu zaidi na chenye kukusanya zaidi, ndio njia yenye nguvu zaidi mbele ya Allah na inayopendeza zaidi, Allah alimwamrisha nayo Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie akasema:

﴿وَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِۚ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ وَكِيلٗا﴾

{Na umtegemee Allah. Na Allah ni Mtegemewa wa kutosha} [An-Nisaa: 81].

Mitume ndio viongozi wa wenye kumtegemea Allah na ndio vielelezo wao; [Allah] aliyetukuka amesema kumhusu Nuuh [salamu zimshukie] kuwa aliiambia kaumu yake:

﴿إِن كَانَ كَبُرَ عَلَيۡكُم مَّقَامِي وَتَذۡكِيرِي بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِ فَعَلَى ٱللَّهِ تَوَكَّلۡتُ﴾

{Ikiwa kukaa kwangu nanyi na kuwakumbusha kwangu aya za Allah kunakutieni mashaka basi mimi namtegemea Allah} [Yunus: 71],

Na *Al-Khaliil* [Ibrahim] [salamu zimshukie] alisema:

﴿رَّبَّنَا عَلَيۡكَ تَوَكَّلۡنَا وَإِلَيۡكَ أَنَبۡنَا وَإِلَيۡكَ ٱلۡمَصِيرُ﴾

{Mola wetu Mlezi! Juu yako tumetegemea, na kwako tumeelekea, na kwako ndio marejeo} [Al-Mumtahinah: 4].

Na Huud [salamu zimshukie] alisema:

﴿إِنِّي تَوَكَّلۡتُ عَلَى ٱللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمۚ مَّا مِن دَآبَّةٍ إِلَّا هُوَ ءَاخِذُۢ بِنَاصِيَتِهَآۚ﴾

{Hakika mimi nimemtegemea Allah, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu. Hapana kiumbe yeyote ila Yeye anamwendesha atakavyo} [Huud: 56],

Na Yakub [salamu zimshukie] alisema:

﴿إِنِ ٱلۡحُكۡمُ إِلَّا لِلَّهِۖ عَلَيۡهِ تَوَكَّلۡتُۖ وَعَلَيۡهِ فَلۡيَتَوَكَّلِ ٱلۡمُتَوَكِّلُونَ﴾

{Hukumu haiko ila kwa Allah tu. Juu yake Yeye mimi nimetegemea, na juu yake Yeye wategemee wanaotegemea} [Yusuf: 67].

Na Shueib [salamu zimshukie] alisema:

﴿وَمَا تَوۡفِيقِيٓ إِلَّا بِٱللَّهِۚ عَلَيۡهِ تَوَكَّلۡتُ وَإِلَيۡهِ أُنِيبُ﴾

{Na sipati kuwezeshwa haya ila na Allah. Kwake Yeye ninategemea, na kwake Yeye naelekea} [Huud: 88].

Na Mitume wa Allah walisema kuwaambia kaumu zao:

﴿وَمَا لَنَآ أَلَّا نَتَوَكَّلَ عَلَى ٱللَّهِ وَقَدۡ هَدَىٰنَا سُبُلَنَا﴾

{Na tuna nini hata tusimtegemee Allah, na hali Yeye ametuongoa kwenye Njia zetu} [Ibrahim: 12].

Na muumini wa watu wa Firauni alisema:

﴿وَأُفَوِّضُ أَمۡرِيٓ إِلَى ٱللَّهِۚ إِنَّ ٱللَّهَ بَصِيرُۢ بِٱلۡعِبَادِ﴾

{Nami namkabidhi Allah mambo yangu. Hakika Allah anawaona waja wake} [Ghaafir: 44].

Na mwanzoni mwa kupewa unabii na kuteremshiwa [wahyi, Mtume] aliamrishwa kumtegemea Allah, na kuwa *Tawakkul* inafungua yaliofungwa,

﴿ٱقۡرَأۡ وَرَبُّكَ ٱلۡأَكۡرَمُ﴾

{Soma! Na Mola wako Mlezi ni Karimu kushinda wote!} [Al-Alaq: 3].

Allah ameijalia kuwa sifa ya watu wa imani, wanatofautiana kwayo na wengine:

﴿إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ ٱللَّهُ وَجِلَتۡ قُلُوبُهُمۡ وَإِذَا تُلِيَتۡ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتُهُۥ زَادَتۡهُمۡ إِيمَٰنٗا

وَعَلَىٰ رَبِّهِمۡ يَتَوَكَّلُونَ﴾

{Hakika Waumini ni wale ambao pindi anapotajwa Allah nyoyo zao hujaa khofu, na wanaposomewa aya zake huwazidisha imani, na

wakamtegemea Mola wao Mlezi} [Al-Anfaal: 2].

Na shetani hana madaraka juu ya waja wa Allah wanaomtegemea; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّهُۥ لَيۡسَ لَهُۥ سُلۡطَٰنٌ عَلَى ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَلَىٰ رَبِّهِمۡ يَتَوَكَّلُونَ﴾

{Hakika yeye hana madaraka juu ya walioamini na wakamtegemea Mola wao Mlezi} [An-Nahl: 99].

*Tawakkul* inakinga na adhabu ya Allah; kama alivyosema [Allah] aliyetakasika:

﴿قُلۡ أَرَءَيۡتُمۡ إِنۡ أَهۡلَكَنِيَ ٱللَّهُ وَمَن مَّعِيَ أَوۡ رَحِمَنَا فَمَن يُجِيرُ ٱلۡكَٰفِرِينَ مِنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ * قُلۡ هُوَ ٱلرَّحۡمَٰنُ ءَامَنَّا بِهِۦ وَعَلَيۡهِ تَوَكَّلۡنَاۖ فَسَتَعۡلَمُونَ مَنۡ هُوَ فِي ضَلَٰلٖ مُّبِينٖ﴾

{Sema: Mwaonaje, ikiwa Allah ataniangamiza mimi na walio pamoja nami, au atanirehemu, ni nani atakaye walinda makafiri na adhabu chungu? * Sema: Yeye ndiye Ar-Rahmaan Mwingi wa Rehema; tunamwamini Yeye, na juu yake tunategemea. Mtakuja jua ni nani aliye katika upotovu ulio dhahiri} [Al-Mulk: 28-29].

Na inawajibisha kuingia Peponi; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَنُبَوِّئَنَّهُم مِّنَ ٱلۡجَنَّةِ غُرَفٗا تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَاۚ نِعۡمَ أَجۡرُ ٱلۡعَٰمِلِينَ ٥٨ ٱلَّذِينَ صَبَرُواْ وَعَلَىٰ رَبِّهِمۡ يَتَوَكَّلُونَ ٥٩﴾.

{Na ambao wameamini na wakatenda mema, bila ya shaka tutawaweka katika maghorofa ya Peponi yenye kupitiwa chini yake mito, wakidumu humo. Ni mwema ulioje huo ujira wa watendao * Ambao walisubiri, na wakamtegemea Mola wao Mlezi} [Al-Ankabuut: 58-59].

Bali wenye kumtegemea Allah kwa hakika wataingia Pepo ya Mola wao Mlezi bila ya hesabu; kama alivyowasifu kwa hilo Nabii wao swala na salamu za Allah zimshukie katika kauli yake: «**Wao ni wale ambao hawaombi kufanyiwa zunguo, wala hawajipishi moto, wala haitakidi nuksi, na ni wenye kumtegemea Mola wao**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alimuusia ibnu Abbaas Allah awaridhie kumtegemea Allah, na hali yeye ni kijana mdogo, ili akitishe itikadi ndani ya nafsi yake kutokea mwanzoni mwa maisha yake, akasema: «**Ewe kijana! Mimi nakufundisha maneno, mhifadhi Allah Naye atakuhifadhi, mhifadhi Allah utamkuta mbele yako, unapoomba basi muombe Allah,**

**na unapotaka msaada basi taka kutoka kwa Allah**», imepokewa na Tirmidhi. Ibnul Qayyim amesema: "Kumtegemea Allah ndio msingi wa daraja za Imani na Ihsani, na matendo ya Uislamu, na cheo chake katika Usilamu ni cheo cha mwili kwa kichwa."

Mnao katika *Tawakkul* mapumziko ya mawazo, na utulivu wa hali, na kinga vitimbi vya waovu, na ni katika sababu zenye nguvu zaidi ambazo mja hujikinga kwazo na asioyaweza miongoni mwa maudhi ya viumbe na dhuluma zao, na kwayo inakatwa tamaa ya yaliyomo mikononi mwa watu. Imam Ahmad Allah amrehemu aliulizwa kuhusu kumtegemea Allah, akasema: "Ni kukata tamaa ya jambo la kuchungulia vilivyomo mikononi mwa watu."

Na kumtegemea asiyekuwa Allah ni kuidhalilisha na kuidunisha nafsi, na kiumbe kumuomba kiumbe ni sawa na fukara kumuomba fukara, [Mtume] swala na salamu zimshukue alisema: «**Na jua kuwa lau umma mzima utakusanyika ili wakunufaishe na kitu, basi hawawezi kukunufaisha na chochote ila na kile alichokuandikia Allah, na lau watakusanyika ili wakudhuru na kitu, basi hawawezi kukudhuru na chochote ila na kile alichokuandikia Allah**», imepokewa na Tirmidhi.

Pindi moyo utageuka kwa asiyekuwa Allah basi Allah atamtegemeza kwa yule aliyemgeukia, na atakuwa si mwenye kuafikiwa, [Mtume] swala na salamu zimshukue alisema: «**Atakayejifunga [moyo wake] na kitu atamtegemeza kwake**», imepokewa na Tirmidhi. Sheikul Islaam Allah amrehemu amesema: "Mtu yeyote hajawahi mtarajia kiumbe au akamtegemea ila dhana yake kwake huambulia patupu, na kila atakayependa kitu kwa ajili ya asiyekuwa Allah basi hapana budi kitamdhuru, na hili lijulikane kupitia ufuatiliaji na upekuzi kamili". Wala jambo la kutowatarajia viumbe lisikupeleke kuwaamili vigumu watu, na kuacha kuwatendea wema na kuhimili udhia wao; bali watendee wema kwa ajili ya Allah; wala si kwa kuwatarajia [yaani: kutarajia malipo ya wema wako kutoka kwao], na kama vile wewe huwaogopi basi pia usiwatarajie, na mtarajie Allah katika [mahitaji yako] kwa watu, wala usiwatarajie watu [mahitaji yako] kwa Allah.

**Enyi Waislamu**:

Riziki zipo katika Mkono wa Muumba, basi itakayokuwa ni yako itakujia pamoja na udhaifu wako, na iliokuwa ya mwenzako basi hutaipata kwa nguvu zako, na riziki ya Allah hailetwi kwako na bidii ya mwenye bidii, wala haizuiliwi kukufikia na chuki ya mwenye chuki.

Riziki zimegawanywa kwa kila mtu - miongoni mwa wema na waovu na muumini na kafiri -; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٖ فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزۡقُهَا﴾

{Na hakuna yeyote anayetembea katika ardhi ila riziki yake iko kwa Allah} [Huud: 6].

Riziki zinapelekwa kwa wanyama pamoja na udhaifu wa wengi wao na kutoweza kwao katafuta riziki; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَكَأَيِّن مِّن دَآبَّةٖ لَّا تَحۡمِلُ رِزۡقَهَا ٱللَّهُ يَرۡزُقُهَا وَإِيَّاكُمۡ﴾

{Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Allah anawaruzuku hao na nyinyi pia} [Al-Ankabuut: 60].

Na huenda Allah akakusahilishia riziki kupitia kibarua au bila kibarua, na watu hujiwa [na udhaifu] kupitia uchache wa kumtegemea Allah, na kupitia kusimama katika sababu za dhahiri kwa nyonyo zao na kujidhalilisha kwazo, na lau wangemtegemea Allah kwa nyoyo zao ipasavyo; basi Allah angewapelekea riziki zao pamoja na sababu ndogo kabisa; kama vile anavyompelekea ndege riziki zao kwa kutoka kwao asubuhi na jioni tu - nayo ni aina ya kutafuta; hata kama ni kutafuta kuchache [juhudu ndogo], [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Lau mgelikuwa mkimtegemea Allah kama ipasavyo kumtegemea, basi angewaruzuku kama anavyowaruzuku ndege; wanatoka asubuhi wakiwa na njaa, na wanarudi jioni wakiwa wameshiba**», imepokewa na Ahmad;

Basi usipoteze muda wako kwa kubeba hamu ya jambo ambalo tayari umeshadhaminiwa, Al-Hasan Al-Basriy Allah amrehemu amesema: "Nilipojua kuwa riziki yangu katu hataila mwengine basi moyo wangu ulitulia."

**Enyi Waislamu:**

Allah aliwekea kadari kila jambo wakati wake, na akayaandalia malengo sababu zake, na mvivu huenda akapata mambo ya dunia na mapambo yake na mwenye bidii akakosa, na akapata katika hayo asiye na uwezo, akakosa mwenye maamuzi madhubuti, na kuzigeukia sababu ni kasoro katika Tawhidi, na kutozizingatia sababu kabisa ni upungufu katika akili, na kuzipa mgongo sababu zilizoamrishwa ni kutia dosari sheria, na ni juu ya mja kuufanya moyo wake uwe ni wenye kumtegemea Allah wala si kutegemea sababu, na Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie ni mkamilifu zaidi wa wanaomtegemea Allah, wala hakufanya upungufu na sababu; alijitokeza siku ya vita vya Uhud akiwa baina ya nguo mbili za vita, na alimuajiri mjuzi wa njia ili amuelekeza njia ya kuhajiri, na alifukua mitaro siku ya vita vya Al-Ahzaab [yaani: hakuzitegemea sababu

badali ya Allah, wala hakuzitupilia mbali kwa madai ya kumtegemea Allah].

Uhakika wa *Tawakkul* ni: Kusimama na sababu na kuufanya moyo umtegemee [Allah] Mwenye kuzipelekesha sababu, na kuitakidi kuwa [sababu] zipo Mkononi mwa Allah, akitaka atazijaalia kutenda kazi yake, na akitaka atajaalia utenda kazi wake uende kinyume na hukumu zake, na akitaka atazisimamishia vizuizi zitakazopinga utenda kazi wake na kuuepusha. Na mwenye Tawhidi na mwenye *Tawakkul* hapati utulivu na sababu wala hazitarajii, kama ambavyo hazipuuzi wala kuzibatilisha; bali anazitekeleza huku akimuangalia na kumtarajisa Mwenye kuziendesha [Allah].

*Tawakkul* inapokuwa na nguvu na kumtarajia Allah kukawa kukubwa Allah huidhinisha faraja. *Al-Khaliil* [Ibrahim salamu zimshukie]] alimuacha mkewe Haajar na mwanawe Ismail akiwa mchamga wa kunyonya katika bonde ambalo halikuwa na harakati ndani yake wala pumbao, wala hakukuwa na mimea kando yake wala wanyama wa maziwa, yote hayo kwa hali ya kumtegemea Allah na kutekeleza amri yake, basi Allah akawazunguka na utunzaji wake, mara tu mwanawe mdogo anakuwa Nabii ambaye Allah amemsifu na busara, subira, ukweli katika ahadi, kuihifadhi swala na kuiamrisha, na maji ya Zamzam yaliobarikiwa ni miongoni mwa matunda ya *Tawakkul* ya *Al-Khaliil*.

Na pindi balaa ilipokuwa kubwa kwa wana wa Israili, wakafuatwa na kuzungukwa na Firauni na jeshi lake, na mbele kulikuwa na bahari:

﴿قَالَ أَصۡحَٰبُ مُوسَىٰٓ إِنَّا لَمُدۡرَكُونَ﴾

{Watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana!} [Ash-Shu'araa: 61].

Nabii wa Allah Musa [salamu zimshukie] aliyekuwa na yakini na nusra ya Allah alisema:

﴿قَالَ كَلَّآۖ إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهۡدِينِ﴾

{Akasema: Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa!} [Ash-Shu'araa: 62].

Basi Allah akamwamrisha kuipiga bahari [na fimbo], basi kukatoka njia kavu, bahari ikatengana na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa.

Yunus [salamu zimshukie] naye alimezwa na samaki akiwa katika mawimbi ya bahari na magiza yake; basi akamuelekea Mola wake na akampelekea mahitaji yake kwake:

﴿لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

{Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe, *Subhaanaka* Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu} [Al-Anbiyaa: 87];

Basi akatupwa ufukoni patupu akiwa mgonjwa, wala hakupotea akiwa peke yake katika sehemu tupu.

Na mamake Musa almitupa mwanawe Musa ndani ya bahari akiwa na yakini na Allah, na kwa kuitikia amri ya Allah; kumbe [mwanawe] ni Mtume kati ya watume bora [*Ulul Azmi*] waliokurubishwa kwa Allah.

Na Yakub [salamu zimshukie] aliambiwa: Mwanako ameliwa na mbwa mwitu, akategemeza amri yake kwa Allah na akamuomba, basi Allah amrudishia mwanawe na nduguye baada ya huzuni na kuepukana kurefu.

Na pindi hali ilipodhikika kwa Maryam [salamu zimshukie], na nafasi zikafungika, na akashindwa kusema, *Tawakkul* yake ilizidi kwa [Allah] Mwenye ukubwa na utukufu, na haikubaki naye ila ikhlasi na kumtegemea Allah, basi akamuashiria [Isa akiwa mchanga] yaani zungumzeni naye:

﴿قَالُواْ كَيۡفَ نُكَلِّمُ مَن كَانَ فِي ٱلۡمَهۡدِ صَبِيّٗا﴾

{Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika mlezi?} [Maryam: 29],

Basi hapo Allah alimsemesha:

﴿قَالَ إِنِّي عَبۡدُ ٱللَّهِ ءَاتَىٰنِيَ ٱلۡكِتَٰبَ وَجَعَلَنِي نَبِيّٗا﴾

{Akasema: Hakika mimi ni mja wa Allah. Amenipa Kitabu, na amenifanya Nabii} [Maryam: 30].

Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie naye anajificha yeye na sahibu yake katika jabali tupu, ndani ya pango tupu lenye kuhofisha, basi hofu ikamjaa sahibu yake na akasema: «Ewe Mtume wa Allah! Lau mmoja wao ataangalia miguuni mwake atatuona chini ya miguu yake, basi [Mtume] akasema - akiwa na yakini na Mola wake -: **Ewe Abu Bakr! Ni ipi dhana yako kuhusu wawili, Allah ndiye watatu wao?**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea; Basi Allah akateremsha nusra yake na akatuma wanajeshi wasioonekana, basi moyo ukatulia, ikapatikana amani na kuhajiri kukatimia, na utume ukang'oa nanga.

Masiku yatakapokuvamia, na maduara ya balaa yakakuzunguka, basi usimtarajie ila Allah, na nyanyua viganja vya unyenyekevu, na uuweke ubavu wako mbele ya Muumba, na fungamanisha matarajio yake naye, na egemeza

amri yako kwa Ar-Rahiim [Mwenye kurehemu], na ukate mafungamano na waja, umnadi Mtukufu, ukitafuta nyakati za kuitikiwa - kama vile katika sijida na mwisho wa usiku -. Na pindi *Tawakkul* na matarajio yatakapokuwa na nguvu, na moyo ukakusanywa katika maombi [ukahudhuria na usiwe wenye kughafilika]: maombi hayatakataliwa,

﴿أَمَّن يُجِيبُ ٱلۡمُضۡطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكۡشِفُ ٱلسُّوٓءَ﴾

{Au nani yule anayemjibu mwenye shida pale anapomwomba, na akaiondoa dhiki} [An-Naml: 62], Basi salimisha amri yako kwa Mfalme.

Allah ni Mwenye ushindi, na mwenye kujilinda naye hadhaliliki, wala hampotezi aliyekimbilia kwake, na faraja ya majanga ni yanapofikia upeo, na wepesi umeambatana na uzito, na jitambulishe kwa Mola wako Mlezi wakati wa raha atakutambua wakati wa shida, na «***Hasbuna llaahu wa ni'mal wakiil***» waliisema vipenzi vya Allah wawili [Ibrahim na Muhammad swala salamu ziwashukie] katika hali nzito.

Ambaye kumtegemea kwake Allah katika kupata kitu kutakuwa kwa kikweli basi atakipata kitu hicho, na atakayetegemeza amri yake kwa Allah basi atamtosheleza yaliomtia hamu, na atakayemtegemea Yeye ipasavyo basi hatamtegemeza kwa asiyekuwa Yeye; bali atatawali amri yake Yeye mwenyewe:

﴿وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓ﴾

{Na anayemtegemea Allah, basi Yeye humtosha} [At-Twalaaq: 3].

Na kwa kadri ya dhana yako njema kwa Mola wako Mlezi na kumtarajia kwako ndio itakuwa *Tawakkul* yako kwake, basi mjaalie Mola wako Mlezi peke yake ndio sehemu ya kupeleka mashtaka yako, Al-Fudhwail Allah amrehemu amesema: "Naapa kwa Allah, lau utakata tamaa kwa waja hadi usitake chochote kutoka kwao, basi Mola wako hakika atakupatia kila unachotaka."

Naye Allah aliyetakasika ni muweza, haitaharaki chembe ndogo ila kwa idhini yake, wala halipiti tukio lolote ila kwa matakwa yake, wala halianguki jani ila kwa elimu yake:

﴿وَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱلۡعَزِيزِ ٱلرَّحِيمِ * ٱلَّذِي يَرَىٰكَ حِينَ تَقُومُ * وَتَقَلُّبَكَ فِي ٱلسَّٰجِدِينَ﴾

{Na umtegemee Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye kurehemu * Ambaye anakuona unaposimama * Na mageuko yako kati ya wanaosujudu} [Ash-Shu'araa: 217-219],

Ibrahim Al-Khawwaas Allah amrehemu amesema: "Baada ya aya hii,

haimpasi mja kumkimbilia yeyote asiyekuwa Allah."

Atakaye jifunga na asiyekuwa Allah au akapata utulivu kwa elimu yake, akili yake, dawa yake na hirizi zake, na akategemea uwezo wake na nguvu yake, Allah atamtegemeza kwake [huyo asiyekuwa Allah] na hatamuafikia, Asema katika [kitabu] *'Taysiirul aziizil hamiid'*: "Na hili linajulikana kupitia dalili na tajiriba."

Mapato mazito zaidi ni: kuwa na yakini na utoshelezaji wa Allah na kuwa na dhana njema naye, na atakayedhania kuwa yalioko kwa Allah yanapatikana kwa kumuasi na kumhalifu kama vile yanavyopatikana kwa kumtii na kujikurubisha kwake, au akadhania kuwa endapo ataacha kitu kwa ajili yake [Allah] hatampa badala iliyobora kukiliko, au akadhania kuwa lau yeye atakuwa mkweli katika kumtegemea Yeye [Allah] kuwa atamkosesha na hatampa aliyomuomba; basi huyo hakika amemdhania Allah dhana mbaya, wala hasalimiki na haya ila aliyemtambua Allah na akatambua Majina yake na Sifa zake, na akatambua mujibu wa hekima yake ya himdi yake. Amesema Ibnul Qayyim Allah amrehemu: "Waja wengi; bali wote, ila wale aliowataka Allah wanamdhania Allah yasiokuwa ya haki na dhana mbaya; kwani binadamu wengi wanaitakidi kuwa wao wanastahiki zaidi ya yale aliyowatakia Allah, na atakayeitafiti nafsi yake na akapekuwa pekuwa kujua yalio ndani [ya nafsi] yake, ataliona hilo limefichana ndani yake; basi mwerevu mwenye kuinasihi nafsi yake ajishughulishe na hili, na atubie kwa Allah na amuombe msamaha katika kila wakati kwa kumdhania Mola wake Mlezi uovu, na badala yake aidhanie nafsi yake uovu."

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿وَٱذۡكُرِ ٱسۡمَ رَبِّكَ وَتَبَتَّلۡ إِلَيۡهِ تَبۡتِيلٗا * رَّبُّ ٱلۡمَشۡرِقِ وَٱلۡمَغۡرِبِ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ فَٱتَّخِذۡهُ وَكِيلٗا﴾

{Na lidhukuru jina la Mola wako Mlezi, na ujitolee kwake kwa ukamilifu * Mola Mlezi wa mashariki na magharibi, hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako} [Al-Muzzammil: 9-10].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

*Tawakkul* ya mja haiwi sawa hadi Tawhidi yake iwe sahihi, na kadri atakavyoitakasa Tawhidi ndio itasihi *Tawakkul*, na pindi mja atageuka kumuelekea asiyekuwa Allah hilo litachukua sehemu katika sehemu za moyo wake; basi *Tawakkul* yake itapungua kwa kadri ya vile zitakavyoondoka sehemu hizo.

Na aliyefikwa na mahitaji, akayapeleka kwa viumbe, basi hayatakuwa ni yenye kutekelezwa, na anayependa kuwa mtu mwenye nguvu zaidi basi amtegemee Allah, na anayependa kuwa mtu mkwasi zaidi basi awe ni mwenye yakini na yaliyoko katika mkono wa Allah kuliko yaliyoko katika mkono wake.

Ridhaa [Kuridhika] na *Tawakkul* zinazunguka makadirio, *Tawakkul* ni kabla ya kutokea kwake [makadirio], na kuridhia ni baada ya kutokea kwake, na kuridhia ni matunda ya *Tawakkul*. Roho ya *Tawakkul* ni kusalimisha mambo yako yote kwa Allah, amesema Daud ibnu Suleiman Allah amrehemu: "Uchamngu wa muumini huthibitishwa kwa mambo matatu: Uzuri wa *Tawakkul* katika mambo ambayo hajayapata, uzuri wa kuridhika katika aliyoyapata, na uzuri wa kusubiri katika yaliokwisha pita."

Na kila mja akiwa ni mwenye kumtambua Allah zaidi, basi *Tawakkul* yake kwake [Allah] inakuwa na nguvu zaidi, kwani nguvu ya *Tawakkul* na udhaifu wake ni kulingana na nguvu ya imani na udhaifu wake.

Anayemtegemea Allah haharakishi faraja, kwani Allah ametaja kwamba anayemtegemea Yeye humtosheleza. Pengine huenda ikadhaniwa kuwa utoshelezaji wake Allah unapatikana kwa haraka wakati huo huo mtu anapomtegemea. Allah amejaalia kila kitu kina kiasi na wakati maalumu; basi aliyemtegemea Allah asifanye haraka akasema: Nimemtegemea Allah na nikaomba na sikuona kitu, kwani Allah anatimiza amri yake, amejaalia kila kitu na kipimo chake.

Na Allah ndiye aliyepwekeka na uchaguzi na uendeshaji, na uendeshaji

wake kwa mja wake ni bora zaidi kuliko uendeshaji wa mja kwa nafsi yake, naye ni Mwenye rehema zaidi kwake kuliko yeye [mja] kwa nafsi yake.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha jambo ambalo Yeye mwenyewe ameanza kulitekeleza..

## KUWA NA DHANA NJEMA KWA ALLAH[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Tawhidi ni haki ya Allah juu ya waja, na kwa ajili yake alitumiliza Mitume, na akateremsha vitabu. Uhakika wa Tawhidi ni: kumpwekesha Allah kwa ibada, na ibada ni: Jina liliokusanya kila anayoyapenda Allah na kuyaridhia - miongoni mwa kauli na matendo; ya dhahiri na ya batini -. Kwa hivyo, moyo unao ibada zinazouhusu, na ibada zake ni kubwa zaidi, nyingi zaidi na za kudumu zaidi kuliko ibada za viungo. Na kuingia kwa amali za moyo katika imani ni aula zaidi kuliko amali ya viungo; kwani imani inayosimama kwa moyo kielimu na kihali ndio msingi unaokusidiwa, na amali za dhahiri ni zenye kutimiza [msingi huo] na kuuandama, wala [amali za dhahiri] haziwi njema zenye kukubaliwa ila kwa kupitia amali ya moyo; Basi hiyo ndiyo roho ya ibada na kiini chake, na endapo amali za dhahiri zitaikosa zitakuwa ni kama mwili uliokufa usio na roho. Kwa kutengea kwa moyo ndio unatengea mwili wote; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Jueni ya kwamba ndani ya mwili mna kinyama, endapo kitatengea basi mwili mzima utatengea, jueni kuwa hicho kinyama ni moyo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Kuzidiana kwa waja kunakuwa kwa kuzidiana yaliomo ndani ya nyoyo, na kwayo ndio amali zinazidiana, na hapo [moyoni] ndipo sehemu Mola Mlezi anapoangalia kutoka kwa waja wake; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakika Allah haangalii miili yenu, wala sura zenu, lakini anaangalia nyoyo zenu na amali zenu**», imepokewa na Muslim.

Kuwa na dhana njema na Allah ni katika amali za nyoyo zilizosisitizwa;

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na nane, mwezi wa Rabiul Aakhir, mwaka elfu moja mia nne na thelathini na tisa hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

kwani hilo ni katika faradhi za Uislamu na mojawapo wa haki za Tawhidi na yanayowajibishwa nayo, na maana yake yenye kukusanya ni: Kila dhana inayolingana na ukamilifu wa dhati ya Allah aliyetakasika, majina yake na sifa zake. Na kuwa na dhana njema na Allah ni tagaa la elimu ya kumjua Allah na kumtambua, nayo inajengewa juu ya kujua ukunjufu wa rehema ya Allah, ushindi wake, ihsani yake, kudura yake, elimu yake, na uzuri wa kuchagua kwake, na huenda likawa hilo kupitia kushuhudia baadhi ya Majina ya Allah na Sifa zake.

Na yule ambaye moyoni mwake kutasimama maana hakika ya majina ya Allah na sifa zake basi itasimama ndani yake [moyo wake] dhana njema inayonasibiana na kila jina na sifa, kwa sababu kila sifa ina ibada mahususi na dhana njema inayoihusu.

Ukamilifu wa Allah, utukufu wake, uzuri wake na kuwaneemesha kwake waja wake, yote hayo yanawajibisha kuwa na dhana njema naye Mwenye ushindi na utukufu. Na Allah amewaamrisha waja wake hilo katika kauli yake:

﴿وَأَحۡسِنُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلۡمُحۡسِنِينَ﴾

{Na fanyeni wema. Hakika Allah huwapenda wafanyao wema} [Al-Baqarah: 195],

Sufyan Ath-Thauri amesema: "Hisinisheni dhana [zenu] kwa Allah", na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisisitiza hilo kabla ya kufa kwake kwa ajili ya utukufu wa cheo chake [jambo hili]; Jabir Allah amridhie alisema: «Nilimsikia Mtume wa Allah kabla kufa kwake kwa siku tatu akisema: "Asife mmoja wenu isipokuwa yeye ni mwenye kumdhania wema Allah mwenye ushindi na utukufu», imepokewa na Muslim.

Allah amewasifu waja wake wanyenyekevu kwa kuwa na dhana njema Naye, na akawajaalia bishara yao ya hapa duniani ni kuwasahilishia ibada na akaifanya [dhana yao njema] ni msaada kwao; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱسۡتَعِينُواْ بِٱلصَّبۡرِ وَٱلصَّلَوٰةِۚ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى ٱلۡخَٰشِعِينَ ۞ ٱلَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُم مُّلَٰقُواْ رَبِّهِمۡ وَأَنَّهُمۡ إِلَيۡهِ رَٰجِعُونَ﴾

{Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kuswali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu * Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi na ya kuwa hakika watarejea kwake} [Al-Baqarah: 45-46].

Na Mitume [salamu ziwashukie] walipata cheo cha juu katika kumjua

kwao Allah; basi wakategemeza mambo yao kwake kwa dhana yao njema kwa Mola wao Mlezi, Ibrahim [salamu zimshukie] alimuacha [mke wake] Haajar na mwanawe Ismail sehemu ya nyumba [Kaaba] na hali Makkah siku hiyo hakuna mtu yeyote, wala hakuna maji, kisha Ibrahim akageuka kuondoka, na Haajar akamwandama na akasema:

«"Ewe Ibrahim! Unaenda wapi na kutuacha katika jangwa hili ambalo ndani yake hakuna mtu wala kitu?" Akamwambia hilo mara kadhaa, na akawa [Ibrahim] hamgeukii, basi [Haajar] akamwambia: "Je ni Allah ndiye amekuamrisha hivi?" [Ibrahim] akasema: "Ndio", naye akasema: "Basi hatatupoteza"», imepokewa na Bukhari; Basi yakawa yale yaliokuwa natija ya dhana yake njema kwa Allah, kukatoka maji yaliobarikiwa, na nyumba [Kaaba] ikaimarishwa, Ismail naye akawa Nabii, na wa mwisho wa Manabii na kiongozi wa Mitume akawa katika kizazi chake.

Yakub [salamu zimshukie] aliwakosa wanawe wawili, akasubiri, na akamtegemezea Allah amri yake, na akasema:

﴿إِنَّمَآ أَشۡكُواْ بَثِّي وَحُزۡنِيٓ إِلَى ٱللَّهِ﴾

{Akasema: Hakika mimi namshitakia Allah sikitiko langu na huzuni yangu [Yusuf: 86],

Moyo wake ukabakia ukiwa umejaa dhana njema kwa Allah na kwamba Yeye ni mbora wa wenye kuhifadhi, na akasema:

﴿عَسَى ٱللَّهُ أَن يَأۡتِيَنِي بِهِمۡ جَمِيعًاۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلۡعَلِيمُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Asaa Allah akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye hekima} [Yusuf:83],

Naye [salamu zimshukie] akawaamrisha watoto wake hilo, akasema;

﴿يَٰبَنِيَّ ٱذۡهَبُواْ فَتَحَسَّسُواْ مِن يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَاْيۡـَٔسُواْ مِن رَّوۡحِ ٱللَّهِۖ
إِنَّهُۥ لَا يَاْيۡـَٔسُ مِن رَّوۡحِ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡقَوۡمُ ٱلۡكَٰفِرُونَ﴾

{Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa na faraji ya Allah. Hakika hawakati tamaa na faraji ya Allah isipokuwa watu makafiri} [Yusuf:87].

Wana wa Israili walikumbwa na udhia wasioweza kuhimili. Pamoja na kuwa na ukubwa janga [liliokuwepo] inabakia kuwa ndani ya dhana njema kwa Allah mnao matarajio na njia; basi Musa [salamu zimshukie] akaiambia kaumu yake:

﴿ٱسْتَعِينُوا۟ بِٱللَّهِ وَٱصْبِرُوٓا۟ ۖ إِنَّ ٱلْأَرْضَ لِلَّهِ يُورِثُهَا مَن يَشَآءُ مِنْ عِبَادِهِۦ ۖ وَٱلْعَٰقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ﴾

{Ombeni msaada kwa Allah, na subirini. Hakika ardhi ni ya Allah. Naye humrithisha amtakaye katika waja wake. Na mwisho [mwema] ni wa wachamngu} [Al-a`raaf:128],

Mazito yalipomlemea Musa [salamu zimshukie] na waliokuwa pamoja naye, bahari iko mbele yao, na Firauni na jeshi lake wako nyuma yao; wakati huo:

﴿قَالَ أَصْحَٰبُ مُوسَىٰٓ إِنَّا لَمُدْرَكُونَ﴾

{Watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana} [Ash-Shu'araa: 61].

Jibu liliotoka kwa Nabii aliyezungumzishwa [na Allah, yaani Musa] likawa ni lenye kushuhudia ukuu wa kumtegemea kwake Allah, na dhana yake njema kwa Mola Mlezi mwenye uwezo:

﴿قَالَ كَلَّآ ۖ إِنَّ مَعِىَ رَبِّى سَيَهْدِينِ﴾

{[Musa] akasema: Hasha! Hakika yuko pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa} [Ash-Shu'araa: 62].

Wahyi ukaja na yasiopita katika fikra:

﴿فَأَوْحَيْنَآ إِلَىٰ مُوسَىٰٓ أَنِ ٱضْرِب بِّعَصَاكَ ٱلْبَحْرَ ۖ فَٱنفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَٱلطَّوْدِ ٱلْعَظِيمِ ۞ وَأَزْلَفْنَا ثَمَّ ٱلْءَاخَرِينَ ۞ وَأَنجَيْنَا مُوسَىٰ وَمَن مَّعَهُۥٓ أَجْمَعِينَ ۞ ثُمَّ أَغْرَقْنَا ٱلْءَاخَرِينَ﴾

{Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa * Na tukawajongeza hapo wale wengine * Tukawaokoa Musa na walio kuwa pamoja naye wote * Kisha tukawazamisha hao wengine} [Ash-Shu'araa: 62].

Kiumbe mwenye kumwabudu Allah zaidi na mwenye dhana njema naye zaidi ni: Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie; kaumu yake walimuudhi, akabaki akiwa ni mwenye kuamini ahadi ya Allah kuinusuru dini yake, Malaika wa majabali alimwambia: «**Ukitaka niwafunike na '*Akhshabaini*' [majabali mawili ya Makkah]**. Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: **Bali natarajia Allah atoe migongoni mwao watakaomwabudu Allah wala hawatamshirikisha na chochote**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Katika hali ya dhiki kabisa na nyakati za giza kubwa kabisa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, twakuta haachi kumdhania Mola wake Mlezi

dhana njema. Alitolewa Makkah, na akiwa njiani aliingia katika pango la 'hiraa', makafiri wakamfuata, mara tu wakawa wamemzingira, basi akawa anamwambia sahibu wake ili kumtia nguvu:

﴿لَا تَحۡزَنۡ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَنَا﴾

{Usihuzunike. Hakika Allah yu pamoja nasi} [At-Taubah: 40].

Abubakar Allah amridhie amesema: «Nilisema kumwambia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie na hali nipo ndani ya pango: "Lau mmoja wao ataangalia miguu yake atatuona chini ya miguu yake", [Mtume] akasema: "**Ewe Abubakar! Ni ipi dhana yako kwa wawili Allah ndiye watatu wao?**"» Wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Pamoja na yaliomfika miongoni mwa udhia, majanga, na vita kutoka kila upande, ila yeye alikuwa ni mwenye yakini ya kufika kwa Dini hii pande zote katika zama zote, na alikuwa akisema: «**Hakika litafika jambo hili [la dini] sehemu zote zilizofika usiku na mchana, wala Allah hataacha nyumba ya udongo wala ya sufi, isipokuwa Allah ataiingiza dini hii, kwa kupitia ushindi wa mshindi au udhalilifu wa dhalili**», imepokewa na Ahmad.

*Aarabi* [Bedui] naye alimtolea upanga Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akiwa amelala, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**"Nikaamka nao [upanga] uko mkononi mwake ukiwa wazi".** [*Aarabi*] akasema: "Ni nani atakukinga na mimi?" Nikasema: "**Allah**" -mara tatu-; wala hakumwadhibu, na ['aarabi'] akakaa», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na katika riwaya ya Ahmad: «Upanga ukamwanguka mkononi mwake».

Masahaba ni waja wenye yakini zaidi baada ya manabii kwa dhana zao njema kwa Allah, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿ٱلَّذِينَ قَالَ لَهُمُ ٱلنَّاسُ إِنَّ ٱلنَّاسَ قَدۡ جَمَعُواْ لَكُمۡ فَٱخۡشَوۡهُمۡ فَزَادَهُمۡ إِيمَٰنٗا
وَقَالُواْ حَسۡبُنَا ٱللَّهُ وَنِعۡمَ ٱلۡوَكِيلُ﴾

{Walioambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia imani, wakasema: Allah anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa} [Aalu Imraan: 173].

Ibnu Ad-Daghina alimwendea Abubakar Allah amridhie ili [Abubakar] aswali na asome kwa siri au amrudishie hifadhi yake - yaani: avunje ahadi yake ya kumkinga, na awamakinishe makafiri wa kikureshi naye -, Abubakar Allah amridhie akasema: «Basi mimi nakurudishia hifadhi yako, na naridhia

hifadhi ya Allah mwenye ushindi na utukufu», imepokewa na Bukhari.

Umar naye Allah amridhie alisema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alituamrisha tutoe sadaka, hilo likaafiki niko na mali, nikasema: "Ikiwa nitashinda siku, basi leo nitamshinda Abubakar". Akasema: "Nikaja na nusu ya mali yangu". Akasema: "Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akaniambia: **"Umewabakishia nini watu wako?"**" Nikasema: "Mfano wake". Abubakar akamjia na yote aliyokuwa nayo. Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akamwambia: **"Umewabakishia nini watu wako?"** Akasema: "Nimewabakishia Allah na Mtume wake"», imepokewa na Abu Daaud.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alimkujia Khadija nana wa wanawake wa ulimwenguni mwanzoni mwa wahyi kuanza akamwambia: «**"Nimejiogopea nafsi yangu"** Khadija Allah amridhie akamwambia: "Hapana; chukua bishara njema! Wallahi Allah hatakutweza kabisa, Wallahi wewe unaunga kizazi, unazungumza ukweli, unambeba asiyejiweza, unachuma yalioadimika na kuyawasilisha kwa watu, unakirimu mgeni, na unasaidia katika misiba ya haki"», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na wema waliotangulia wa umma huu walifuata mwenendo huu, Sufyan Allah amrehemu amesema: "Sipendelei iwe hisabu yangu - yaani: kulipwa kwangu kwa mema na maovu - wamewakilishwa nayo wazazi wangu, Mola wangu ni bora kwangu kuliko wazazi wangu», na miongoni mwa dua ya Said ibnu Jubair Allah amrehemu ilikuwa: "Ewe Allah, mimi nakuomba *Tawakkul* ya ukweli, na dhana njema kwako».

Na wamo miongoni mwa majini waliowema, dhana zao kwa Allah ni njema, wana yakini ya nguvu za Allah, na ukunjufu wa elimu yake; na katika kauli zao ilikua:

﴿وَأَنَّا ظَنَنَّآ أَن لَّن نُّعۡجِزَ ٱللَّهَ فِي ٱلۡأَرۡضِ وَلَن نُّعۡجِزَهُۥ هَرَبًا﴾

{Nasi tulijua kuwa hatutomshinda Allah duniani, wala hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia} [Al-jinn: 12].

Hakika wako miongoni mwa waja wa Allah ambao lau ataapa basi Allah atamtekelezea, si kuapa kwa kumlazimisha Allah na kumkatia kauli, lakini ni dhana njema kwake [Allah] aliyetukuka. Na ni katika shani ya muumini kuwa na dhana njema kwa Allah katika nyakati zote na kila hali, na ni aula kuwa hivyo pindi anapomuomba na kuzungumza naye, akiwa na yakini ya ukaribu wake, na kuwa Yeye humuitikia anayemuomba, wala hamkoseshi anayemtarajia.

Na dhana njema ya mtu kwa Mola wake Mlezi, ni miongoni mwa sababu za kukubaliwa toba, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema katika anayoyapokea kutoka kwa Mola wake Mlezi: «**Mja wangu ametenda dhambi; akajua kuwa ana Mola Mlezi anayesamehe dhambi na anaadhibu kwa dhambi, fanya utakalo; nimekusamehe**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Wakati wa misiba na mazito zinabainika dhana njema na zinakashifika dhana mbovu; katika vita vya Uhud [kwa mfano], waumini walikuwa imara, na wasiokuwa wao walikuwa wakimdhania Allah yasio ya haki dhana ya kijahili, na katika vita vya Al-Ahzaab dhana kwa Allah zilikuwa tofauti, Allah amesema kuhusu kipote:

﴿هُنَالِكَ ٱبۡتُلِيَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ وَزُلۡزِلُواْ زِلۡزَالٗا شَدِيدٗا * وَإِذۡ يَقُولُ ٱلۡمُنَٰفِقُونَ وَٱلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٞ مَّا وَعَدَنَا ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ إِلَّا غُرُورٗا﴾

{Hapo ndipo waumini walipojaribiwa, na wakatikiswa mtikiso mkali. Na waliposema wanafiki na wale wenye maradhi katika nyoyo zao: Allah na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu} [Al-Ahzaab:11-12],

Ama masahaba walikuwa na yakini kuwa mazito ni mtihani utokao kwa Allah na baada yake huja ushindi na faraja. Allah aliyetakasika alisema kuwahusu:

﴿وَلَمَّا رَءَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلۡأَحۡزَابَ قَالُواْ هَٰذَا مَا وَعَدَنَا ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَصَدَقَ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥۚ وَمَا زَادَهُمۡ إِلَّآ إِيمَٰنٗا وَتَسۡلِيمٗا﴾

{Na Waumini walipoyaona makundi, walisema: Haya ndiyo aliyotuahidi Allah na Mtume wake. Na Allah na Mtume wake wamesema kweli. Na hayo hayakuwazidisha ila imani na utiifu} [Al-Ahzaab: 22].

Njia ya kutokea katika dhiki, majanga, na hamu ni dhana njema kwa Allah; kwani wale watatu waliobaki nyuma [wasihudhurie vita vya Tabuk] Allah hakuwaondolea janga lililowashukia ila kwa dhana yao njema kwa Allah, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَعَلَى ٱلثَّلَٰثَةِ ٱلَّذِينَ خُلِّفُواْ حَتَّىٰٓ إِذَا ضَاقَتۡ عَلَيۡهِمُ ٱلۡأَرۡضُ بِمَا رَحُبَتۡ وَضَاقَتۡ عَلَيۡهِمۡ أَنفُسُهُمۡ وَظَنُّوٓاْ أَن لَّا مَلۡجَأَ مِنَ ٱللَّهِ إِلَّآ إِلَيۡهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيۡهِمۡ لِيَتُوبُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ﴾

{Na pia wale watatu walioachwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjufu wake, na nafsi zao zikabanika, na wakayakinisha kuwa hapana pa kumkimbia Allah isipokuwa kwake Yeye. Kisha akawaafikia toba ili

watubu. Hakika Allah ndiye Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu} [At-Taubah:118]

Allah ni mwenye nguvu, muweza, na nusra yake kwa waja wake na vipenzi vyake hakuna mwenye kuighilibu, na katika yakini ni kuwa na imani na nusra yake, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِن يَنصُرۡكُمُ ٱللَّهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمۡۖ وَإِن يَخۡذُلۡكُمۡ فَمَن ذَا ٱلَّذِي يَنصُرُكُم مِّنۢ بَعۡدِهِۦ﴾

{Akikunusuruni Allah hapana wa kukushindeni, na akikutupeni ni nani basi, baada yake Yeye ataye kunusuruni?} [Aalu Imraan: 160].

Naye [Allah] aliyetakasika ni mwenye kurehemu [Ar-Rahiim] mwingi wa rehema [Ar-Rahmaan], atakayemwamini, akatenda mema na akatarajia vipawa vya rehema zake basi atazipata, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Pindi Allah alipomaliza kuumba aliandika katika kitabu chake, nacho kiko kwake juu ya Arshi: Hakika rehema zangu zimeshinda hasira zangu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Yule aliyefikwa na dhiki ya maisha basi dhana njema yake [kwa Mola wake Mlezi] ni ukunjufu na faraja, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Aliyefikwa na mahitaji, akawapelekea watu basi mahitaji yake hayatatekelezwa, na aliyefikwa na mahitaji akampelekea kwa Allah; basi imekurubia Allah kumfungulia riziki karibuni au baadaye**», imepokewa na Tirmidhi.

Zubair ibnul Awwaam alisema kumwambia mwanawe Abdallah Allah awaridhie wote wawili: «Ewe mwanangu! Unaposhindwa na chochote katika hili -yaani: deni kulilipa-, basi taka msaada kwa Bwana wangu". [Abdallah] akasema: "Wallahi sikujua aliyoyakusudia hadi niliposema: Ewe babangu! Ni nani Bwan wako?" Akasema: "Ni Allah". Basi wallahi sikuwahi kuingia katika janga la deni lake [babake] ila nikisema: "Ewe Bwana wa Zubair! Mkidhie deni lake"; basi [Allah] akilikidhi», imepokewa na Bukhari.

Naye Allah aliyetakasika ni mkunjufu wa msamaha na kutoa, na atakayekuwa na dhana njema naye katika ukwasi wake, ukarimu wake, na msamaha wake atampa anayoyaomba. [Allah] aliyetakasika anashuka kila usiku akisema: «**Ni nani ananiita nimuitikie? Ni naniananiomba nimpatie? Ni nani ananiomba msamaha nimsamehe?**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na Mikono yake miwili imejaa, «**Hayapunguwi kwa kutoa, naye ni mtoaji sana usiku na mchana**».

Naye Allah ni mwenye kukubali sana toba, hufurahi kwa toba za waja, na hukunjua Mkono wake usiku ili aliyefanya makosa mchana atubie, na

hukunjua Mkono wake mchana ili aliyefanya makosa usiku atubie, na ni katika sifa zake za ukamilifu kuwa Yeye Allah mtukufu hamrudishi aliyemjia, na wakati ambao mja ahitajia zaidi kuwa na dhana njema kwa Allah ni pindi ajali yake inapokurubia, akaaga dunia, na akaelekea kwa Mola wake Mlezi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Mmoja wenu asife ila hali ya kuwa ni mwenye dhana njema kwa Allah mwenye ushindi na utukufu**», imepokewa na Muslim.

Katika ibada hii [ya kuwa na dhana njema kwa Allah] kuna kutekeleza amri ya Allah, na kutekeleza ibada yake, na mja atapata kutoka kwa Mola wake Mlezi yale aliyomdhania nayo, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Allah aliyetukuka anasema: "Mimi niko katika dhana ya mja wangu kwangu, na niko naye pindi anaponidhukuru"**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ibnu Mas'uud Allah amridhie amesema: "Mja hawi na dhana njema kwa Allah; ila Allah humpatia yale aliyoyadhania, hilo ni kwa kuwa heri ipo Mkononi mwake Allah aliyetakasika".

Pindi mja anaporuzukiwa dhana njema kwa Mola wake Mlezi; basi hakika Allah amemfungulia mlango mkubwa wa heri katika dini, Ibnu Mas'uud Allah amridhie amesema: "Naapa na yule ambaye hakuna apasaye kuabudiwa ila Yeye! Hajawahi mja muumini kupatiwa kitu bora zaidi kuliko dhana njema kwa Allah".

Amali za watu ni kwa kadri ya dhana zao kwa Mola wao Mlezi; Muumini amemdhania Allah vyema kwa hivyo akafanya amali njema, ama kafiri amemdhania vibaya Allah basi akafanya amali mbaya. Katika ibada hii kunaonekanwa ubora wa Uislamu na ukamilifu wa imani, nayo ndio njia ya kumfikisha mwenye kuifuata Peponi. Ni ibada ya kimoyo inayorithisha kumtegemea Allah na kuwa na imani naye.

Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Kumtegemea kwako Mola wako Mlezi kunakuwa kwa kadri ya dhana njema yako kwake na kumtarajia kwako, na kwa sababu hiyo baadhi yao [wafasiri] waliitafsiri *Tawakkul* kuwa ni dhana njema kwa Allah, na tafsiri ya undani ni kuwa: Kumdhania vyema Allah kunamuita [mtu] katika kumtegemea Yeye; kwa kuwa haiwezekani kutemgemea uliye na dhana mbaya kwake, wala kumtegemea usiyemtarajia".

Ni katika athari za ibada: Utulivu wa moyo, kumuelekea Allah na kutubia kwake, wala hakuna lenye kuukunjua moyo zaidi baada ya imani kuliko kumtegemea Allah na kumtarajia, kwani mnao ndani yake yenye kumfanya mja awe na fali njema, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Hakuna maambukizo wala nuksi, na napenda fali njema**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Al-Haliimi Allah amrehemu amesema: "*Tashaaum* [nuksi]: ni dhana mbaya kwa Allah, na *Tafaaul* [fali njema]: ni dhana njema kwa Allah".

[Dhana njema] ni usaidizi kwa mtu juu ya kuwa mkarimu, shujaa, na inampa nguvu, Abu Abdillah As-Saaji Allah amrehemu amesema: «Atakayemtegemea Allah, hakika amekusanya nguvu zake [zote], nayo ndio maandalizi bora na matayarisho mazuri zaidi". Salamah ibnu Diinar Allah amrehemu aliambiwa: "Ewe Abu Haazim! Ni yapi mali yako? Akasema: Kumtegemea Allah na kukata tamaa na vilivyoko katika mikono ya watu".

Atakayemdhania vyema Mola wake Mlezi, basi nafsi yake itakuwa karimu na itatoa mali yake ikiwa na yakini na kauli ya Allah:

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن شَيۡءٖ فَهُوَ يُخۡلِفُهُۥ﴾

{Na chochote mtakachokitoa, basi Yeye [Allah] atakilipa badala yake} [Saba`:39],

Suleiman Ad-Daaraani Allah amrehemu amesema: "Atakayemtegemea Allah katika riziki yake, basi tabia yake njema itazidi, na itamletea busara, na nafsi yake itakuwa karimu katika matumizi yake, na wasiwasi wake katika swala yake utapungua".

Nayo [dhana njema] ni yenye kupelekea kutarajia yalio kwa Allah, na kuaminia ahadi yake, na kutenda heri hali ya kuwa na matumaini na fadhila zake [Allah], kwa mujibu wa yaliokuja katika kauli yake:

﴿وَمَا يَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ فَلَن يُكۡفَرُوهُۗ﴾

{Na heri yoyote wanayoifanya hawatanyimwa malipo yake} [Aalu Imraan: 115].

Na Allah anawaamili waja wake kwa kadri ya dhana zao kwake, na malipo ni kwa kulingana na amali; basi atakayedhania heri atapata hilo, na atakayedhania mengineo, basi hakika amehasirika, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Allah mwenye ushindi na utukufu amesema: Mimi niko kama anavyonidhania mja wangu; basi anidhanie anavyotaka, akinidhania heri ataipata, na akinidhania shari ataipata**», imepokewa na Ahmad

Kwa hivyo, mja anapomdhania vyema Allah basi hakika Allah hatomtamausha katu, na aliyekuwa na dhana njema na Mola wake Mlezi atasema siku ya Kiyama:

﴿هَآؤُمُ ٱقۡرَءُواْ كِتَٰبِيَهۡ ۝ إِنِّي ظَنَنتُ أَنِّي مُلَٰقٍ حِسَابِيَهۡ ۝ فَهُوَ فِي عِيشَةٖ رَّاضِيَةٖ ۝ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٖ﴾

{Haya someni kitabu changu! * Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu * Basi yeye atakuwa katika maisha ya kupendeza * Katika Pepo ya juu} [Al-Haaqqah: 19-22].

**Na baada ya haya, enyi Waislamu:**

Allah ni Mkarimu, mkubwa, mwenye nguvu, aliye adhimu, anapokitaka kitu hukiambia: Kuwa, nacho kikawa. Ameahidi kukihifadhi Kitabu chake, na kuinusuru dini yake, na amejaalia mwisho mwema ni wa wachamngu, anamruzuku anayemtaka bila hesabu, na huyaondoa majanga ya mwenye kukimbilia kwake.

Na yule itakayozidi elimu yake kumhusu Allah; basi yakini yake itazidi, na atakaye kuwa na dhana mbaya naye; basi ni kwa sababu ya ujinga wake katika Majina yake na Sifa zake za ukamilifu, na hilo ni katika sifa za watu wa kijahili, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿يَظُنُّونَ بِٱللَّهِ غَيۡرَ ٱلۡحَقِّ ظَنَّ ٱلۡجَٰهِلِيَّةِ﴾

{Wakamdhania Allah dhana isiyokuwa ya haki, dhana ya kijahili} [Aalu Imraan:154]

Na katika matunda ya kuamini Majina ya Allah na Sifa zake ni: kuwa na dhana njema kwake, kumtegemea Yeye, na kusalimisha mambo [yote] kwake.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿فَمَا ظَنُّكُم بِرَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾

{Mnamdhania nini Mola Mlezi wa walimwengu wote?} [As-Swaaffaat: 87].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Uhakika wa dhana njema kwa Allah unadhihiri katika amali njema, na inakuwa ni yenye kunufaisha inapokuwa pamoja na ihsani, na watu wenye dhana njema zaidi kwa Mola wao Mlezi ni wale wenye kumtii zaidi, na kila mja anapomdhania vyema Mola wake Mlezi basi hapana budi amali yake nayo itakuwa njema, na yule ambaye matendo yake yatakuwa maovu basi dhana zake [kwa Mola wake] zitakuwa mbovu. Na pindi dhana njema inapoambatana na kufanya maasi basi huko itakuwa ni kuhisi amani ya makri [mipango] ya Allah, na endapo dhana njema itampelekea mtu kufanya utiifu basi hiyo ndio yenye kunufaisha, na inapopungua hiyo [dhana njema] katika moyo basi maasi yatadhihiri katika viuongo.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## KHERI IPO NDANI YA ALIYOYAJAALIA ALLAH[1].

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani uchamngu ndio jambo zuri zaidi kati ya mnayoyadhirisha, na bora zaidi kati ya mnayoyaficha.

**Enyi Waislamu:**

Allah alijiita nafsi yake majina mazuri zaidi, na amesifika na sifa kamili zaidi, ameumba viumbe na akafanya hilo kwa ukamilifu, akaumba ulimwengu kwa vizuri, na amemiliki ufalme wake sawa sawa, hataharaki wa kutaharaki wala hatulii wa kutulia ila kwa elimu yake na matakwa yake, anahukumu wala hakuna wa kupinga hukumu yake, na anapitisha wala hakuna wa kurudisha anayoyapitisha, ni Mwenye nguvu; hazuiliwi katika kutenda kwake, ni Mtukufu Mkubwa; haulizwi analolifanya nao viumbe wataulizwa. Naye Allah aliyetakasika pamoja hivyo ni Mwenye kurehemu; viumbe wanageukageuka ndani ya athari za rehema yake, ni Mwenye rehema kuliko hata mama kwa mwanawe, ni Mwenye kushukuru mno; atakayeacha kitu kwa ajili yake humpatia ziada, ni Mwenye upole kwa waja wake; anawapelekea neema na hali wao hawatambui, ni Mwenye kuruzuku Mwenye kufungua; amewafungulia waja wake milango ya riziki kutoka mbinguni na ardhini:

﴿قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۖ قُلِ ٱللَّهُ ۖ﴾

{Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Sema: ni Allah} [Saba': 24].

Allah ni Mkarimu; anatoa na anakithirisha katika utoaji, hakuna baina yake na baina ya viumbe vyake pazia.

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na mbili ya mwezi wa Rabiul Akhir, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na tisa hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Mja ni dhaifu, amesifiwa na ufukara na kuwa na haraka, amefunikwa na ujinga, hajui yatakayokuwa kesho, wala atakufa wapi:

﴿وَٱللَّهُ أَخۡرَجَكُم مِّنۢ بُطُونِ أُمَّهَٰتِكُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ شَيۡـٔٗا وَجَعَلَ لَكُمُ ٱلسَّمۡعَ وَٱلۡأَبۡصَٰرَ
وَٱلۡأَفۡـِٔدَةَ لَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ﴾

{Na Allah amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru} [An-Nahl: 78],

Allah aliyetakasika naye ni Mwenye rehema na Mpole kwa waja wake, amewaamrisha wasalimishe mambo yao kwake, wamtegemee Yeye, na waridhie aliyowagawanyia.

Kuamini hukumu ya Allah na kadari: ni mojawapo wa nguzo za Imani. Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiwafundisha masahaba wake sababu za [kuzidisha] imani na kuridhia yale Allah aliyoyawachagulia kama anavyowafundisha sura katika Qur-ani; kwa ajili ya kufichimana kwa ghaibu na kufichimana hekima ya mambo kwao wao, Jabiri Allah amridhie amesema: «Mtume wa Allah alikuwa akitufundisha *Istikhaara* [dua ya kumtaka Allah ushauri] katika mambo yote, kama anavyotufundisha sura katika Qur-ani», imepokewa na Bukhari.

Na yale Allah anamuhukumia mja ni bora kuliko yale mja anayojitakia mwenyewe, kwani Yeye ni Mwenye huruma kwa mja kuliko nafsi yake. Na yale Allah anayomuekea mja akiba pindi amemnyima anayoyapenda ni bora kwake hata lau nafsi yake ikiwa inapapia kinyume chake [cha yale aliyowekewa akiba]; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Ajabu ya jambo la muumini! Hakika jambo lake lote ni heri kwake, na hanayo hali hiyo ila muumini; akifikwa na ya furaha hushukuru ikawa ni heri kwake, na akifikwa na ya kudhuru husubiri ikawa ni kheri kwake**», imepokewa na Muslim.

Aliofikwa nayo Mwislamu miongoni mwa misiba na huzuni, hakika si mengine Allah anamtahini nayo ili amwongoze, anamtahini nayo ili ampatie, na anamnyima ili amnyanyue, na pengine yanayochukiwa huenda yakaleta yanayopendwa, na yanayopendwa huenda yakaleta yanayochukiwa, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ وَأَنتُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ﴾

{Na Allah anajua na nyinyi hamjui} [Al-Baqarah: 216].

Ni mangapi ambayo Allah amemhukumia mja miongoni mwa daraja za juu na vipawa kwa sababu ya misiba na hali yeye hajui?! Ibrahim [salamu

zimshukie] alipewa [mtoto] Ismail baada ya kuzeeka na akampenda; kisha Allah akamwamrisha kumchinja ili amtahini; *Al-Khaliil* [Ibrahim] akatekeleza amri ya Allah ya kumchinja, basi chaguo likawa lake [la kumnufaisha na kumridhisha]; Allah akamwokoa mwanawe kutokana na kumchinja, na Ismail akajenga Kaaba pamoja naye. Allah pia akampa Is-haaq pamoja na Ismail, na nyuma ya Is-haaq kuna Yaquub, na hakuja Nabii baada yake ila kutokana na kizazi cha *Al-Khaliil* Ibrahim [salamu zimshukie].

Hajar mamake Ismail [salamu ziwashukie] aliachwa Makkah na mumewe Ibrahim [salamu zimshukie] akiwa na mwanawe wa kunyonya kwa amri ya Allah, katika bonde tupu, hakuna sauti ndani yake wala pumbao, alikurubia kuangamia, hakuna maji [Makkah wakati huo] wala pakushukia, akawa anakimbia baina ya majabali mawili [Swafaa na Marwa] akiangalia: Je ataona mtu yeyote? Na hakuona yeyote. Uchaguzi bora ukawa ni ule aliouchagua Allah; Jibril aliteremka akapiga ardhi na ubawa wake; hapo Zamzam ikatoka kwa wingi, maji yanayoonekanwa juu ya ardhi, wanakunywa mahujaji, wanaotekeleza umra na wengineo, kwa baraka ya *Tawakkul* ya Haajar kwa Allah, na watu wanakimbia baina ya Swafaa na Marwa kama alivyokimbia [Hajar].

Yusuf [salamu zimshukie] naye aliishi katika malezi ya baba aliyekuwa na huruma, anamuogopea kutoka kuenda kucheza na nduguze:

﴿أَرْسِلْهُ مَعَنَا غَدًا يَرْتَعْ وَيَلْعَبْ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ﴾

{Mpeleke kesho pamoja nasi, ale kwa furaha na acheze; na bila shaka sisi tutamhifadhi} [Yusuf: 12].

Kisha akatolewa kutoka kwenye ulezi na huruma ile, na akakosa huruma ya baba na pumbao la undugu, na akatupwa ndani ya kisima peke yake, Allah alimpatia nasaba bora, uzuri na ubarobaro, basi baada ya [msiba wa kutupwa] kisimani mwanamke akamtaka bila ya yeye kumtaka, [Yusuf] akasema pamoja na kupatikana vishawishi vingi:

﴿مَعَاذَ ٱللَّهِۖ إِنَّهُۥ رَبِّيٓ أَحۡسَنَ مَثۡوَايَ﴾

{Audhubillahi! Najikinga na Allah. Huyu bwana wangu kaniweka maskani nzuri} [Yusuf: 23],

Basi Allah akampa baada ya hayo sifa njema, akamjaalia ni mfano wa heshima ya ubarobaro na kumuogopa Allah katika maficho, na akampa utume baada ya [msiba wa kutupwa] kisimani, na akajaaliwa hazina za ufalme [wa ardhi] mikononi mwake, na ikateremshwa sura kwa jina lake inasomwa hadi siku ya Kiyama.

Ayyuub [salamu zimshukie] naye anatahiniwa na maradhi, masahibu

wakamtoroka, na wakamfia watoto -akiwa katika hali ile-, lakini Allah kwa rehema zake alimuekea akiba ya ponyo na neema; na akapewa afueni kutokana na mtihani aliopewa, na Allah akamruzuku watoto idadi mfano wa wale [walifariki], na akamjaalia kuwa mfano wa wenye kusubiri:

﴿وَأَيُّوبَ إِذۡ نَادَىٰ رَبَّهُۥٓ أَنِّي مَسَّنِيَ ٱلضُّرُّ وَأَنتَ أَرۡحَمُ ٱلرَّٰحِمِينَ ❁
فَٱسۡتَجَبۡنَا لَهُۥ فَكَشَفۡنَا مَا بِهِۦ مِن ضُرّٖۖ وَءَاتَيۡنَٰهُ أَهۡلَهُۥ وَمِثۡلَهُم مَّعَهُمۡ رَحۡمَةٗ مِّنۡ عِندِنَا
وَذِكۡرَىٰ لِلۡعَٰبِدِينَ﴾

{Na Ayyubu, alipomwita Mola wake Mlezi, akasema: Mimi yamenipata madhara. Na Wewe ndiye unayerehemu kuliko wote wanaorehemu * Basi tukamwitikia, na tukamwondolea madhara aliyokuwa nayo, na tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao kuwa ni rehema inayotoka kwetu, na ukumbusho kwa wafanyao ibada} [Al-Anbiyaa: 83-84].

Yunus [salamu zimshukie] naye anatupwa katika mawimbi ya bahari kutoka jahazini, akamezwa na samaki, lakini Allah alimwokoa na uangamivu na akamchunga kwa hifadhi yake; basi samaki akamtapika katika ufuko wa bahari baada ya kukaa matumboni mwake masiku, na Allah akamuoteshea mmea wa malenge, na akamtuma kwa watu elfu mia moja au wanazidi, basi wote wakaamini, Allah akawaneemesha hadi muda maalumu; basi mtihani wake ukawa ni kheri kwake na kwa kaumu yake na waliofinikwa na majanga baada yake, basi hakuna yeyote aliyeomba kwa dua yake [Yunus] ila Allah alimwokowa na janga lake. [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَذَا ٱلنُّونِ إِذ ذَّهَبَ مُغَٰضِبٗا فَظَنَّ أَن لَّن نَّقۡدِرَ عَلَيۡهِ فَنَادَىٰ فِي ٱلظُّلُمَٰتِ
أَن لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ❁
فَٱسۡتَجَبۡنَا لَهُۥ وَنَجَّيۡنَٰهُ مِنَ ٱلۡغَمِّۚ وَكَذَٰلِكَ نُـۨجِي ٱلۡمُؤۡمِنِينَ﴾

{Na *Dhun-Nun* alipoondoka hali ameghadhibika, na akadhani ya kwamba hatutakuwa na uwezo juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe *Subhanaka* Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu * Basi tukamwitikia na tukamwokoa kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo tunavyo waokoa Waumini} [Al-Anbiyaa: 87-88],

[Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «**Maombi ya *Dhun-Nun* alipoomba naye yumo ndani ya tumbo la samaki:**

**﴿لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾**

**{Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe *Subhanaka* Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu}; hakika katu hajawahi kuomba kwayo Mwislamu yeyote katika kitu chochote ila Allah alimuitikia**», imepokewa na Tirmidhi.

Zakariya [salamu zimshukie] naye alinyimwa kizazi muda mrefu, mifupa yake ikadhoofika na nywele zake zikaenea mvi, na alimwelekea Allah kwa dua; basi ukawa wa mwisho wa kuchelewa huku ni malaika kumwita kumwambia kuwa Allah anakubashiria mtoto wa kiume, na aliyempa jina kijana huyu ni Allah, na akamwita jina ambalo hajawahi itwa nalo kiumbe kabla ya hapo:

﴿يَٰزَكَرِيَّآ إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَٰمٍ ٱسۡمُهُۥ يَحۡيَىٰ لَمۡ نَجۡعَل لَّهُۥ مِن قَبۡلُ سَمِيّٗا﴾

{Ewe Zakariya! Hakika Sisi tunakubashiria mwana; jina lake ni Yahya. Hatujapata kumpa jina hilo yeyote kabla yake} [Maryam: 7].

Na hata kabla ya mamake kubeba mimba yake tayari Allah alimfunulia babake hali atakayokuwa nayo mwanawe maishani; ili nafsi yake ipate utulivu kwa kuongoka kwake [mwanawe].

﴿مُصَدِّقَۢا بِكَلِمَةٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَسَيِّدٗا وَحَصُورٗا وَنَبِيّٗا مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Allah, na ni bwana na ni mwenye kujihifadhi na Nabii kwa watu wema} [Aalu Imraan: 39].

Mamake Musa naye aliamrishwa na Allah kumtupa mwanawe Musa baharini ilhali ni mchanga wa kunyonya, na dhahiri ya hilo ni maangamivu, lakini Allah alimhifadhi, na akamnyima kunyonya kwa wanyonyeshaji, akamrudisha kwa mamake ili amyonyeshe na achukue malipo ya kumyonyesha.

Kisha Musa [salamu zimshukie] anaishi katika majumba ya Firauni katika neema na raha, na atahiniwa na balaa nyingine, mara wakuu wanashauriana kumuua, basi akatoka Misri akiwa na uoga akipeleleza, na akatembea katika jangwa tupu, na anafika mji wa Madyan - mji asioujua -, akainua jicho lake mbingu na kusema:

﴿رَبِّ إِنِّي لِمَآ أَنزَلۡتَ إِلَيَّ مِنۡ خَيۡرٖ فَقِيرٞ﴾

{Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia} [Al-Qaswas: 24];

Basi Allah akampa - baada ya uzito huu na mtihani - utume na unabii, na akazungumza naye moja kwa moja bila ukati, na akamchagua miongoni mwa mitume bora [*Ulul Azmi*].

Mamake Maryam naye alitamani aruzukiwe mtoto wa kiume ila Allah alimruzuku wa kike; basi mwisho ukawa ni kheri nyingi, yule msichana akazaa nabii mtume.

Maryam [salamu zimshukie] naye alihifadhi uchi wake; basi Allah akapuliza ndani yake miongoni mwa roho zake [alioziumba], akabeba mimba kwa amri ya Allah bila ya kuwa na mume, na kutokana na ukubwa wa msiba wake alisema:

﴿يَٰلَيۡتَنِي مِتُّ قَبۡلَ هَٰذَا وَكُنتُ نَسۡيٗا مَّنسِيّٗا﴾

{Laiti ningelikufa kabla ya haya, na nikawa niliye sahaulika kabisa!} [Maryam: 23].

Lakini Allah ni Mwenye hekima na elimu, alijaalia mimba hii ni alama kwa watu, aliibeba pasi na mume, na ikazaliwa mimba ile na akawa nabii, na Allah akadumisha utajo wake yeye na mwanawe katika Qur-ani:

﴿وَجَعَلۡنَٰهَا وَٱبۡنَهَآ ءَايَةٗ لِّلۡعَٰلَمِينَ﴾

{Na tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni alama kwa walimwengu} [Al-Anbiyaa: 91].

Na nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie alikulia yatima wa wazazi wawili, wala hana ndugu atakaokaa nao; basi akawa Allah ndiye aliyempa makazi:

﴿أَلَمۡ يَجِدۡكَ يَتِيمٗا فَـَٔاوَىٰ﴾

{Kwani hakukukuta yatima akakupa makaazi?} [Adh-Dhuhaa: 6],

Na akampandisha hadi mbinguni akisuhubiana naye Jibrili, na Allah akamwandalia makazi mazuri katika pepo ya juu kabisa, na akamwambia:

﴿وَلَلۡأٓخِرَةُ خَيۡرٞ لَّكَ مِنَ ٱلۡأُولَىٰ﴾

{Na Akhera ni bora kwako na yenye kudumu zaidi} [Al-A'laa: 17].

Masahaba Allah awaridhie nao waligura kutoka Makkah hadi Madinah, waliacha mji wao na watu wao na kuiendea ardhi nyingine na watu wengine; basi Allah akawajaalia kuwa ni wenye kuibeba dini, na akawajaalia kuwa miongoni mwa watu wa peponi:

﴿رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُۚ وَأَعَدَّ لَهُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِي تَحۡتَهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗا﴾

{Allah yu radhi nao, na wao waradhi Naye. Hayo ni kwa anayemwogopa Mola wake Mlezi} [Al-Bayyinah: 8].

Katika mwaka wa sita hijria Nabii swala na salamu za Allah zimshukie pamoja na masahaba wake waliekea Makkah kupitia Hudaybiyyah, na idadi yao ikiwa ni elfu moja na mia nne, washirikina wakawazuilia kuingia [Makkah], na wakakubaliana kuwa [waislamu] waje mwaka unaokabili, basi nyoyo za masahaba zikahisi uchungu, na nafsi zao zikahuzunika, kwa kuwa wamezuiliwa na nyumba [takatifu] baada ya kuwa washaikurubia, na wakaamrishwa kurudi ilhali wameijia, basi wakaitikia amri ya Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie ya kurudi na kutoingia [Makkah] mwaka huu; na wakairudia mwaka uliokabili, na Allah akawapa badala ya umra yao walioiacha umra nyingine na nguvu na ushindi, na wakawa elfu kumi, na wakaingia Makkah bila ya vita mwaka wa kuftahi, na watu wakaingia katika dini ya Allah makundi kwa makundi, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akavunja masanamu yaliokuwa kingizoni mwa Kaaba naye akisoma:

﴿وَقُلْ جَآءَ ٱلْحَقُّ وَزَهَقَ ٱلْبَٰطِلُ ۚ إِنَّ ٱلْبَٰطِلَ كَانَ زَهُوقًا﴾

{Na sema: Haki imefika, na batili imetoweka. Hakika batili lazima itoweke!} [Al-Israa: 81], na dini ikaenea katika kila kingo.

Na aliyekulia ubarobaroni mwake juu ya kumtii Allah, na akaizuilia nafsi yake kutokana na ya haramu na kufuata matamanio; basi Allah atamweka katika kivuli cha chini ya arshi yake siku ambayo hakuna kivuli ila chake.

Na atakayeitwa na mwanamke aliyeharamu kwake, akamwacha kwa kumuogopa Allah ; basi Allah atamfufua chini ya kivuli cha Arshi yake pamoja na waja wa Allah bora, Qatada Allah amrehemu amesema: "Mtu hawi na uwezo wa kufanya haramu kisha akaiacha, hana chochote [kilichomfanya aiache] ila kumuogopa Allah; ila Allah atambadilishia ambalo ni heri kwake kuliko hilo hapa duniani kabla Akhera."

Na aliyekosa macho yake akasubiri; basi Allah atampa badala yake katika Akhera ambalo jicho halijaona; [Mtume] swala na salamu zimshukie amesema: «**Allah Mwenye ushindi na utukufu amesema: Nitakapomtahini mja wangu na vipenzi vyake viwili [yaani: macho yake] na akasubiri; nitampa badala yake Pepo**», imepokewa na Ahmad.

Basi aliyeyakinisha uzuri wa anayomchagulia Allah mja wake; misiba kwake yanakuwa mepesi, na mazito kwake yanakuwa sahali, na atakuwa na akiba ya ujira wa aliyotahiniwa nayo, kwa kuwa na yakini ya huruma ya Allah, ukarimu wake na uzuri wa chaguo lake.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿وَعَسَىٰٓ أَن تَكۡرَهُواْ شَيۡـٔٗا وَهُوَ خَيۡرٞ لَّكُمۡۖ وَعَسَىٰٓ أَن تُحِبُّواْ شَيۡـٔٗا وَهُوَ شَرّٞ لَّكُمۡۚ وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ وَأَنتُمۡ لَا تَعۡلَمُونَ﴾

{Na huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Allah anajua na nyinyi hamjui} [Al-Baqarah: 216].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Allah huwaandikia baadhi ya waja wake daraja za juu, ambazo amali hazifikii, basi Allah huwatahini na aina za balaa; ili wapate ujira utakaowafikisha daraja zile na vyeo vya juu, na atakaye suburi kwa yaliomfika na akasalimisha jambo lake kwa Allah; Allah atamruzuku kuridhika na kuwa na yakini, na atafanya mwisho wa jambo lake ni mzuri. Na mapenzi ya kufanya aliyoyaharamisha Allah yanapokuwa na nguvu, na nafsi ikawa na shauku ya kuyafanya, kisha mja akajizuilia nayo; basi ujira wa kuacha kwake utakuwa mkubwa, na malipo ya kushindana na nafsi ili kuyaacha [ya haramu] yatazidishwa maradufu, na atalipwa badali iliyobora zaidi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## KUSUBIRI KATIKA MISIBA[1].

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamwomba msaada, tunamwomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule atakayeongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii**:

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, kwani katika uchamngu mna kuongezeka kwa neema na kukingwa na adhabu.

**Enyi Waislamu:**

Hakika Allah amekadiria makadirio ya viumbe na muda wao [wa kuishi], akasajili athari zao na matendo yao, akagawanya baina yao maisha ~~yao~~ na mali yao, na akaumba mauti na uhai ili awatahini nani kati yao atakuwa mzuri wa amali. Na kuamini hukumu ya Allah na kadari yake ni nguzo miongoni mwa nguzo za Imani. Hamna katika ardhi harakati yoyote wala utulivu isipokuwa kwa matakwa yake, na hamna kiumbe chochote ndani ya ulimwengu ila ni kwa makadirio ya Allah na uumbaji wake. Dunia nayo imejaa shida na mazito, imepewa maumbile ya mashaka na vitisho, na mabadiliko na mitihani ndani yake ni kama joto na baridi, mja hana budi nayo:

﴿وَلَنَبۡلُوَنَّكُم بِشَيۡءٖ مِّنَ ٱلۡخَوۡفِ وَٱلۡجُوعِ وَنَقۡصٖ مِّنَ ٱلۡأَمۡوَٰلِ وَٱلۡأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِۗ وَبَشِّرِ ٱلصَّٰبِرِينَ﴾

{Hapana shaka tutawapa mtihani wa kitu hafifu cha [hali ya] kuogopa, njaa, na upungufu wa mali, watu na matunda. Na wabashirie wanaosubiri} [Al-Baqarah: 155].

Na vizuizi vya njiani ni mitihani ambayo kwayo anabainika mkweli kutokana na mrongo:

﴿أَحَسِبَ ٱلنَّاسُ أَن يُتۡرَكُوٓاْ أَن يَقُولُوٓاْ ءَامَنَّا وَهُمۡ لَا يُفۡتَنُونَ﴾

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe tano ya mwezi wa Muharram, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na mbili hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

{Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Nao wasijaribiwe?} [Al-Ankabuut: 2].

Na nafsi haitakati ila kwa mitihani, na misiba inadhihirisha wanaume [wa kweli], ibnul Jawzy Allah amrehemu amesema: "Anayetaka salama na afya zidumu kwake bila ya kufikwa na msiba; basi hajaijua *taklifu* [jukumu la kisheria], wala hajaelewa kujisalimisha ni nini". Hapana budi kila nafsi ifikwe na machungu, sawa imeamini au imekufuru, na maisha yamepangwa juu ya kupitia mashaka na kuparaga ya hatari, wala yeyote asiwe na tamaa ya kusalimika kutokana na mitihani na uchungu.

Mtu katika zama zake anakuwa na mabadiliko ya kutoka kwenye neema na kuikabili mitihani, Adam [salamu zimshukie] alisujudiwa na Malaika, kisha baada ya muda ndiye huyo anatolewa Peponi, na hayakuwa mitihani ila ni kinyume cha malengo na matamanio [ya mtu], na bila shaka kila mmoja anameza machungu, lakini wanatofautiana baina ya uchache na wingi. Muumini hutahiniwa ila arekebishwe wala si aadhibiwe, fitina nyakati za furaha, na mitihani nyakati za madhara:

﴿وَبَلَوْنَٰهُم بِٱلْحَسَنَٰتِ وَٱلسَّيِّـَٔاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ﴾

{Na tukawajaribu kwa mema na mabaya ili wapate kurejea} [Al-A'raf: 168].

Na yenye kuchukiza huenda yakaleta yanayopendeza, na yanayopendeza huenda yakaleta yanayochukiza, basi usiaminie kutofikwa na madhara kutoka upande wa furaha, wala usikate tamaa ya kupata furaha kutoka upande wa madhara; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَعَسَىٰٓ أَن تَكْرَهُوا۟ شَيْـًٔا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰٓ أَن تُحِبُّوا۟ شَيْـًٔا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ ۗ
وَٱللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ﴾

{Na huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu, na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Allah anajua na nyinyi hamjui} [Al-Baqarah: 216].

Basi itulize nafsi yako kuhusu misiba kabla haijakushukia; ili yawe mepesi kwako [yatakapokushukia], wala usikose subira kwa ajili ya msiba; kwani mitihani ina muda wenye ukomo mbele ya Allah, wala usidhihirishe hasira kwa maneno kwani huenda neno likatamkwa na ulimu likamwangamiza binadamu.

Muumini barabara huthibiti katika mazito, wala moyo wake haugeuki, wala ulimi wake haushitaki. Jihafifishie msiba kwa [kukumbuka] ahadi ya malipo na usahali wa mambo kutoka kwa Allah; ili msiba uondoke bila

kushitakia. Na wenye akili hawaachi kudhihirisha ukakamavu wakati wa msiba; ili wasibebe [uzito wa] misiba pamoja na [uzito wa] furaha ya maadui kwa msiba wao. Na endapo msiba utadhihiri kwa adui basi atafurahi. Na kuficha misiba na maumivu ni miongoni mwa tabia za werevu, basi subiria joto kali la msiba, kwani ni haraka ilioje kuondoka kwake, na upeo wa jambo ni kusubiri siku chache, na hawajaangamia walioangamia ila kwa ajili ya kuishiwa na ukakamavu, na wanaosubiri watalipwa thawabu bora:

﴿وَلَنَجۡزِيَنَّ ٱلَّذِينَ صَبَرُوٓاْ أَجۡرَهُم بِأَحۡسَنِ مَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ﴾

{Na kwa yakini Sisi tutawapa waliosubiri ujira wao kwa ubora ya waliyokuwa wakiyatenda} [An-Nahl: 96].

Na malipo yao ni mara dufu:

﴿أُوْلَٰٓئِكَ يُؤۡتَوۡنَ أَجۡرَهُم مَّرَّتَيۡنِ بِمَا صَبَرُواْ﴾

{Basi hao watapewa ujira wao mara mbili kwa walivyosubiri} [Al-Qaswas: 54],

Bali bila ya hesabu, na Allah yupo nao, na nusra na faraja imeambatanishwa na subira yao.

Mola wako hajakunyima - ewe ulio na msiba - isipokuwa akupatie, wala hajakupa majanga ila akuafu, wala hajakutahini ila akusafishe. Anatahini kwa neema na ananeemesha kwa mtihani, basi usipoteze wakati wako kwa kubeba hamu ya jambo la riziki ambalo ushadhaminiwa, madamu muda [wa kuishi] umebakia basi riziki itakujia; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٖ فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزۡقُهَا﴾

{Na Hakuna chochote kitembeacho katika ardhi ila riziki yake iko kwa Allah} [Huud: 6].

Na pindi atakapokufungia kwa hekima yake njia katika njia za riziki; atakufungulia kwa rehema yake njia [nyingine] yenye manufaa zaidi nawe kuliko ile [aliyokufungia].

Kupitia mitihani inanyanyuliwa shani ya watu bora, na ujira wa watu wema unakuwa mkubwa; Sa'ad ibnu Abi Waqqaas Allah amridhie amesema: «Nilisema: Ewe Mtume wa Allah! Ni watu gani wenye mitihani migumu zaidi? Akasema: **Manabii, kisha watu wema, kisha wafananao nao zaidi kisha wafananao nao zaidi katika watu; mtu hutahiniwa kwa kulingana na dini yake, ikiwa dini yake ina nguvu basi huzidishiwa mtihani wake, na ikiwa dini yake ina udhaifu basi huhafifishiwa, na mtihani hauachi kuwa kwa mja hadi atembee juu ya ardhi akiwa hana dhambi**», imepokewa na Ahmad.

Njia ya mitihani ni mapito yalio magumu; alitaabika ndani yake Adam, akatupwa motoni *Al-Khaliil* [Ibrahim], Ismail naye akalazwa chini kuchinjwa, Yunus akatiwa ndani ya tumbo la samaki, Ayyuub akapambana na madhara, Yusuf akauzwa kwa thamani duni, akatiwa kisimani na jela kwa dhuluma, na Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie akapata aina tofauti za udhia.

Basi na wewe unatembea juu ya njia ya mitihani, na dunia haikuwa safi kwa yeyote hata akapata kutokana nayo atakayopata, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema: «**Yule ambaye Allah anamtakia heri basi humwonja**», imepokewa na Bukhari. Baadhi ya wenye elimu wamesema: "Yule ambaye Allah amemuumba kuingia Peponi basi machukivu hayataacha kumjia."

Msiba wa hakika ni msiba katika dini, na mengineo katika misiba ni afueni, mnao ndani yake kunyanyuliwa daraja na kufutiwa madhambi, na kila neema isiokurubisha kwa Allah basi hiyo ni msiba, na aliyesibiwa ni yule aliyenyimwa thawabu, basi usisikitikie ulioyakosa katika dunia, kwani misiba yake ni matukio, na hadithi zake ni ghamu, na matukio yake ni hamu, watu wanaadhibiwa ndani yake kwa kadri watakavyo kuwa na hamu nayo [dunia]. Kufurahi nayo ndio jambo lenye kuhuzunikiwa hasa, machungu yake yamezalika kutokana na ladha zake, na huzuni zake zimezalika kutokana na furaha zake. Abu Dardaa Allah amridhie anasema: "Katika uduni wa dunia mbele ya Allah, ni kuwa Yeye haasiwi ila ndani yake, na hayapatikani yalio kwake ila kwa kuiacha."

Basi jishughulishe na jambo la manufaa zaidi kwako kuliko kupata ulilolikosa, miongoni mwa kuondosha upungufu, au kutoa udhuru kwa teleza, au kusimama mlangoni kwa Bwana wa mabwana. Na hisi uharaka wa kuondoka kwa msiba nao utakuwa sahali, na lau si majanga ya shida basi hakungetarajiwa kipindi cha mapumziko. Na kata tamaa na yaliomo katika mikono ya watu utakuwa mkwasi zaidi kati yao, wala usikate tamaa [na yalioko kwa Allah] utakacho kuafikiwe.

Kumbuka neema za Allah juu yako, na jikinge na huzuni kwa kuridhia kadari ya lazima, kwani urefu wa usiku hata ukafikia upeo basi asubuhi itachomoza, na mwishoni wa hamu ndio mwanzo wa faraja, na maisha hayabaki katika hali moja, bali kila jambo baada yake kuna jambo lengine, na hakuna uzito wowote ila utasahilika, wala usikate tamaa hata yanapofika majanga, kwani uzito mmoja hautaghilibu uwepesi miwili, na nyenyekea kwa Allah faraja itaelekea upande wako, na hajawahi kunywa kikombe cha subira mtu aliyeshikamana na Allah ila itamjia njia ya kutokea;

Pindi Yakub [salamu zimshukie] alipomkosa mtoto na muda ukawa mrefu kwake hakukata tamaa ya faraja, na mwanawe mwengine alipochukuliwa matarajio yake kwa [Allah] Mmoja wa pekee hayakukatika; bali alisema:

﴿فَصَبۡرٞ جَمِيلٌۖ عَسَى ٱللَّهُ أَن يَأۡتِيَنِي بِهِمۡ جَمِيعًا﴾

{Subira ni njema! Huenda Allah akaniletea wote pamoja} [Yusuf: 83].

Mola wetu Mlezi peke yake ndiye anayemiliki na kustahiki himdi na kwake ndio yanapelekwa mashtaka. Basi pindi siku zitakapokuvamia, na njia zikafungwa mbele yako, basi usimtarajie katika kukuondolea msiba wako na kukukinga na balaa ila Allah. Na pindi giza la usiku litakapochanganyika, na usiku ukateremsha nguo ya sitara yake, basi geuze uso wako ndani ya giza la usiku kuelekea mbinguni, na nyanyua viganja vya unyenyekevu umuite Mkarimu akuletee faraja ya janga lako, na asahilishe amri yako. Na pindi matarajio [kwa Allah] yatakuwa na nguvu, na moyo ukakusanywa katika dua basi maombi hayatarudishwa:

﴿أَمَّن يُجِيبُ ٱلۡمُضۡطَرَّ إِذَا دَعَاهُ وَيَكۡشِفُ ٱلسُّوٓءَ﴾

{Au nani yule anayemjibu mwenye shida pale anapomwomba, na akaiondoa dhiki} [An-Naml: 62].

Mtegemee Muweza, na elekea kwake na moyo mnyenyekevu uliodhalili, utafunguliwa mlango. Al-Fudhwail ibnu Iyaadh Allah amrehemu amesema: "Lau utakata tamaa kwa waja hadi usitake kutoka kwao chochote basi Mola wako atakupatia kila unachotaka."

Ibrahim [salamu zimshukie] alimuacha [Mkewe] Hajar na mwanawe Ismail katika bonde lisilo na mimea ndani yake wala maji, mara tu amekuwa Nabii anawaamrisha watu wake swala na zaka. Wala Yunus [salamu zimshukie] hakupotea akiwa peke yake ufukoni patupu. Na atakayesalimisha jambo lake kwa Mola wake basi atapata malengo yake, na kithirisha maombi ya *Dhun-Nun*:

﴿لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

{Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe *Subhanaka* Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu} [Al-Anbiyaa: 87].

Wanazuoni wanasema: "Hajawahi kuomba nayo [maombi haya] aliyefikwa na janga ila Allah alifariji janga lake". Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Na hakika imejaribiwa kuwa atakayesema: *'Rabbi*

*innii massaniya dhurru wa anta arhamu ar-raahimiina'*, bimaana "Mola wangu Mlezi, hakika yamenipata madhara. Na Wewe ndiye unayerehemu kuliko wote wanao rehemu" mara saba; Allah atamwondolea madhara yake.

Basi weka ubavu wako mbele ya Allah, na fungamanisha matarajio yako naye, usalimishe amri yako kwa Mwenye kurehemu, umuombe faraja, na kata mafungamano na viumbe, na chagua nyakati za kujibiwa, kama vile [wakati wa] sujudu, na mwisho wa usiku. Na tahadhari kuona wakati wa msiba kuwa ni mrefu, ukachoka kuomba dua kwa wingi, kwani wewe umetahiniwa na msiba, unatakiwa kuabudu na subira na maombi, na msiba unapokuwa mrefu usikate tamaa na rehema za Allah, kwani faraja ipo karibu, na muombe Mwenye kufungua milango kwani Yeye ni Mkarimu:

﴿وَإِن يَمۡسَسۡكَ ٱللَّهُ بِضُرّٖ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ﴾

{Na Allah akikufikishia madhara, basi hapana wa kukuondolea [madhara hayo] ila Yeye} [Al-An'aam: 17],

Naye ni Mwenye kufanya alitakalo; Zakariya [salamu zimshukie] alifikia ukongwe katika uzee, kisha akaruzukiwa mwana aliye bwana, mbora wa watu na Manabii, na Ibrahim [salamu zimshukie] alibashiriwa mtoto na hali mkewe baada ya kukata tamaa ya hali yake anasema:

﴿ءَأَلِدُ وَأَنَا۠ عَجُوزٞ وَهَٰذَا بَعۡلِي شَيۡخًاۖ﴾

{Je, hivyo mimi nizae, na hali yangu ni mkongwe na huyu mume wangu ni mzee?} [Huud: 72].

Riziki inapochelewa; basi kithirisha toba na kuomba msamaha kwani teleza inawajibisha kuadhibiwa, na usipoona athari ya kuitikiwa basi peleleza amali yako; kwani huenda toba haikuwa ya kweli, basi isahihishe kisha elekea kwa dua, kwani hakuna mkarimu zaidi wala mwenye mkono mtoaji sana kuliko *Al-Jawwaad* [Allah], na watafute wanyonge [kwa sadaka yako] kwani sadaka inaondoa janga.

Pindi utaondolewa mtihani basi kithirisha kumhimidi [Allah] na kumsifu, na jua kuwa kudanganyika na salama ni katika mitihani mikubwa, kwani adhabu yake huenda ikachelewa, na mwenye akili ni yule anayeangalia mwisho wa mambo.

Basi daima yakinisha kadari ya Allah, uumbaji wake na uendeshaji wake, na subiri katika mtihani wake na hukumu yake, na jisalimishe kwa amri yake.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿قُل لَّن يُصِيبَنَآ إِلَّا مَا كَتَبَ ٱللَّهُ لَنَا هُوَ مَوۡلَىٰنَاۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَلۡيَتَوَكَّلِ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ﴾

{Sema: Halitusibu ila alilotuandikia Allah. Yeye ndiye Mola wetu Mlinzi. Na Waumini wamtegemee Allah tu!} [At-Tawbah: 51]

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu**:

Basi hali hazidumu juu ya hali moja, na mwema ni yule aliyedumu na uchamngu, akipata ukwasi, basi [uchamngu] unampamba, na akifukarika unamkinaisha, na akitahiniwa unamfanya mzuri. Kwa hivyo, dumu na uchamngu katika kila hali, kwani [kwa hilo] hutaona katika dhiki ila ukunjufu, wala katika maradhi ila afueni, wala katika ufukara ila ukwasi.

Lililojaaliwa hakuna mbinu ya kuliondoa, na ambalo halijajaaliwa hakuna mbinu ya kulileta, na *Ridhaa* [kuridhika] na *Tawakkul* zinazunguka makadirio, na Allah ndiye aliyepwekeka na uchaguzi na uendeleshaji, na uendeshaji wake [Allah] kwa mja ni bora kwake [mja] kuliko uendeshaji wa mja kwa nafsi yake, naye ni Mwenye rehema kwake kuliko yeye mwenyewe kwa nafsi yake. Daud ibnu Suleiman Allah amrehemu amesema: "Uchamngu wa muumini huthibitishwa kwa mambo matatu: Uzuri wa *Tawakkul* katika mambo ambayo hajayapata, uzuri wa kuridhika katika aliyoyapata, na uzuri wa kusubiri katika yaliokwisha pita."

Atakayeridhia uchaguzi wa Allah, basi atafikwa na kadari hali ya kuwa yeye ni mwenye kuhimidiwa, kushukuriwa na mwenye kuhurumiwa. Kinyume na hivyo kadari itamfikia hali ya kuwa ni mwenye kukashifiwa, si mwenye kuhurumiwa. Pamoja na haya hakuna kutoka nje ya uliokadiriwa.

Waliulizwa baadhi ya wenye hekima: "Ukwasi ni nini? Akasema: Ni uchache wa kutamani kwako na kuridhika kwako na yenye kukutosha". Shureih Allah amrehemu anasema: "Hajawahi mja kusibiwa na msiba wowote ila alikuwa na neema tatu ndani yake: Kuwa haukuwa katika dini yake, na kuwa msiba huo haukuwa mkubwa zaidi ya ulivyokuwa, na kuwa Allah alimruzuku subira juu yake aliposubiri."

Kisha mswalieni na msalimieni - enyi waja wa Allah - mbora wa viumbe vya Allah Muhammad ibnu Abdillah; kwani Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

## KUTHIBITI WAKATI WA MSIBA[1].

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na mchungeni [chungeni amri zake na makatazo yake] katika siri na minong'ono.

**Enyi Waislamu:**

Allah amekadiria makadirio na ajali, akaandika athari na amali, ameumba mbingu, na ardhi, na mauti na uhai kwa ajili ya kutahini; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَهُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ فِى سِتَّةِ أَيَّامٍ وَكَانَ عَرْشُهُۥ عَلَى ٱلْمَآءِ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا﴾

{Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi} [Al-Mulk: 2].

Basi dunia imeumbiwa katika maumbile ya uhatari na uzito wa kimaisha, huyu ametahiniwa kwa njaa, na mwengine kwa hofu, na yule kwa kukosa nafsi [kufiliwa], na wale wengine kwa mali.

Misiba haijui wakati wala jinsi, wala sehemu wala umri, [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَنَبْلُوكُم بِٱلشَّرِّ وَٱلْخَيْرِ فِتْنَةً ۖ وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ﴾

{Na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa} [Al-Anbiyaa: 35].

---

1) [Hotuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na sita ya mwezi wa Muharram, mwaka elfu moja mia nne na thelathini hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Kuamini kadari ya heri na ya shari ni: Nguzo miongoni mwa nguzo za Imani, na muumini ni mwenye kuthibiti katika shida na mazito, hatetemeshwi na balaa wala mitihani, anatembea na kadari itakavyokuwa, akiwa ni mwenye kuiamini, akisalimisha amri yake kwa Allah, akimtegemea.

Kutahiniwa ni mapito ya watukufu, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa: «Nilisema: Ewe Mtume wa Allah! Ni watu gani wenye mitihani migumu zaidi? Akasema: **Manabii, kisha watu wema, kisha wafananao nao zaidi kisha wafananao nao zaidi katika watu; mtu hutahiniwa kwa kulingana na dini yake, ikiwa dini yake ina nguvu basi huzidishiwa mtihani wake, na ikiwa dini yake ina udhaifu basi huhafifishiwa**.»

Kutahiniwa kwa muumini hakika si mengine ila ni kwa ajili ya kutimiziwa ujira wake na kunyanyuliwa cheo chake; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Mtihani hauachi kuwa na mja hadi atembee juu ya ardhi akiwa hana dhambi**», imepokewa na Ahmad. Ibnu Rajab Allah amrehemu amesema: "Hakika cheo [kiwango] cha msiba kinajulikana pindi pazia itakapokashifiwa siku ya Kiyama."

Mwislamu ni Mwenye iza mtukufu havunjiki moyo mbele ya misiba; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Mfano wa muumini ni kama mmea mchanga, upepo unauyumbisha mara moja na unausimamisha mara nyingine** - yaani: anatahiniwa na msiba kisha anarudi katika nguvu zake -**, na mfano wa mnafiki ni kama mwerezi hauachi [kusimama wima dhidi ya upepo] hadi ukianguka unaanguka mara moja tu** - yaani: katika mtazamo wa jicho ni wenye nguvu, lakini uhakika ni kuwa ni dhaifu, unaanguka mara moja tu wala hausimami tena-», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na mfumo wa Manabii [salamu ziwashukie] ulikuwa ni: kuwa na nguvu wakati wa misiba na kukita juu ya dini wakati wa mitihani, na ilikuwa katika dua ya Nabii swala na salamu za Allah zimshukie: «**Ewe Allah! Hakika mimi nakuomba umadhubuti katika jambo [langu], na azimio la nguvu juu ya uongofu**», imepokewa na An-Nasai.

*Al-Khaliil* Ibrahim [salamu zimshukie] alipovunja masanamu, maadui wake wakasema:

﴿فَأْتُوا۟ بِهِۦ عَلَىٰٓ أَعْيُنِ ٱلنَّاسِ﴾

{Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu} [Al-Anbiyaa: 67];

ili wapate kuona tukimwadhibu, basi hakuwaogopa na akasema:

﴿أُفّٖ لَّكُمۡ وَلِمَا تَعۡبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِۖ﴾

{Ubaya uwafikie nyinyi na hivyo mnavyoviabudu badala ya Allah!} [Al-Anbiyaa: 67].

Wakamtishia kumchoma na moto, basi hilo halikumzidisha ila matarajio kwa Allah, na akasema:

﴿رَبِّ هَبۡ لِي مِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Ewe Mola wangu Mlezi! Nitunukie aliye miongoni mwa watenda mema} [As-Swaaffaat: 100].

Allah akambashiria kupata kijana mwenye busara.

Na pindi babake alipomwambia:

﴿يَٰٓإِبۡرَٰهِيمُۖ لَئِن لَّمۡ تَنتَهِ لَأَرۡجُمَنَّكَ﴾

{Ewe Ibrahim! Usipokomeka (kuwatukana waungu wangu), basi lazima nitakupiga mawe} [Maryam: 46].

Hakudhoofika katika ulinganizi, na akasema:

﴿سَلَٰمٌ عَلَيۡكَۖ سَأَسۡتَغۡفِرُ لَكَ رَبِّيٓۖ إِنَّهُۥ كَانَ بِي حَفِيّٗا﴾

{Amani iwe juu yako! Mimi nitakuombea msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ananihurumia sana} [Maryam: 47].

Yusuf [salamu zimshukie] naye - akiwa jela - huzuni hazikumzuilia kulingania katika Tawhidi:

﴿يَٰصَٰحِبَيِ ٱلسِّجۡنِ ءَأَرۡبَابٞ مُّتَفَرِّقُونَ خَيۡرٌ أَمِ ٱللَّهُ ٱلۡوَٰحِدُ ٱلۡقَهَّارُ﴾

{Enyi wafungwa wenzangu wawili! Je, mabwana wengi wanaofarikiana wao kwa wao ni bora au Allah Mmoja Mwenye nguvu?} [Yusuf: 39].

Luut [salamu zimshukie] naye aliambiwa na kaumu yake:

﴿لَئِن لَّمۡ تَنتَهِ يَٰلُوطُ لَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡمُخۡرَجِينَ﴾

{Ewe Luut! Usipoacha [kutukataza kuwaendea wanaume], hapana shaka utakuwa miongoni mwa wanaotolewa mji!} [Ash-Shu'araa: 167].

Akawaambia kwa utukufu:

﴿إِنِّي لِعَمَلِكُم مِّنَ ٱلْقَالِينَ﴾

{Akasema: Hakika mimi ni katika wanao kichukia hiki kitendo chenu} [Ash-Shu'araa: 163].

Shueib [salamu zimshukie] naye walimtishia kumtoa mji endapo hatafuata dini yao, basi akawaambia:

﴿قَدِ ٱفْتَرَيْنَا عَلَى ٱللَّهِ كَذِبًا إِنْ عُدْنَا فِي مِلَّتِكُم بَعْدَ إِذْ نَجَّىٰنَا ٱللَّهُ مِنْهَا﴾

{Bila ya shaka itakuwa tumemzulia uongo Allah tukirudi katika mila yenu baada ya kwisha tuokoa nayo Allah} [Al-A'raf: 89].

Yunus [salamu zimshukie] naye hamu haikumwepusha kufungamana na Mola wake Mlezi na hali yupo ndani ya tumbo la samaki; bali alikuwa akimnadi Mola wake Mlezi kwa Tawhidi:

﴿لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبْحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

{Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe *Subhanaka* Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu} [Al-Anbiyaa: 87].

Firauni naye alipomtuhumu Musa na wazimu, akasema:

﴿إِنَّ رَسُولَكُمُ ٱلَّذِيٓ أُرْسِلَ إِلَيْكُمْ لَمَجْنُونٌ﴾

{Hakika huyu Mtume wenu aliyetumwa kwenu ni mwendawazimu} [Ash-Shu'araa: 27].

Basi hapo Musa hakuangalia kauli yake; bali alimlingania katika Tawhidi, na akasema: Mola wangu Mlezi ndiye:

﴿رَبُّ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَآ إِن كُنتُمْ تَعْقِلُونَ﴾

{Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi na viliomo baina yao, ikiwa nyinyi mnatia akilini} [Ash-Shu'araa: 28].

Na pindi Firauni alipokusanya wachawi wake ili kumsukasuka Musa:

﴿قَالَ مَوْعِدُكُمْ يَوْمُ ٱلزِّينَةِ﴾

{Akasema: Miadi yenu ni siku ya mapambo} [Twaahaa: 59], yaani: siku ya idi; ili watu wote watuone.

Hilo lilikuwa katika tukio la kuogopesha, Musa alisema - akiwa na

yakini ya nusra ya Allah na kushindwa kwao [makafiri]:

﴿أَلْقُواْ مَآ أَنتُم مُّلْقُونَ﴾

{Tupeni mnavyo tupa!} [Yunus: 80].

Na pindi wana wa Israili walipoacha kumnusuru Musa na wakasita kwenda kupigana na wakasema:

﴿فَٱذْهَبْ أَنتَ وَرَبُّكَ فَقَـٰتِلَآ إِنَّا هَـٰهُنَا قَـٰعِدُونَ﴾

{Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa} [Al-Maidah: 24].

Basi hakuchelewa kupitisha amri ya Mola wake Mlezi, bali [Musa] alipigana na wafuasi wake nao wakapina pamoja naye, na Allah akawanusuru.

Wakati Musa alipotoka Misri Firauni alimfuata, mara tu mbele yake kukawa ni bahari na Firauni yupo nyuma yake, basi

﴿قَالَ أَصْحَـٰبُ مُوسَىٰٓ إِنَّا لَمُدْرَكُونَ﴾

{Watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana!} [Ash-Shu'araa: 61].

[Musa] akasema kwa imani ya Allah iliyokita na yenye nguvu:

﴿كَلَّآ ۖ إِنَّ مَعِىَ رَبِّى سَيَهْدِينِ﴾

{Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa!} [Ash-Shu'araa: 61].

Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie naye alifungiwa ndani ya mojawapo wa mitaa ya Makaah miaka mitatu, wala hakukoma kufanya daawa, na walimfanyia shere wakasema: Ni mchawi, mrongo na mwandaazimu, hata hivyo [Mtume] akawapa mgongo; Vile vile wakamtoa katika mji wake Makkah:

﴿إِذْ أَخْرَجَهُ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ ثَانِىَ ٱثْنَيْنِ﴾

{Pindi makafiri walipomtoa [Makkah], naye ni wa pili kati ya wawili [yaye na Abu Bakr]} [At-Tawbah: 40].

Basi akakamilisha kufikisha ujumbe wa Mola wake katika mji mwengine.

Mtume pia katika vita vya Badr anaona wingi wa washirikina, na anasema: Hakika mimi nimeonyeshwa sehemu watakapofia hawa jamaa [washirikina], na katika vita vya Uhud Waislamu walipatwa na msiba, na alienda Khaybar kupigana, na mapote yalijumuika dhidi yake katika vita vya Khandaq, kisha akaenda Makkah kuifutahi, na baada ya vita vya Khandaq alisema: «**Sasa sisi tutawapiga vita wala wao hawatatupiga vita**», imepokewa na Bukhari, na katika vita vya Hunayn Waislamu walipatwa na msiba, kisha akawapiga vita waroma katika Tabuk.

Meno yake ya mbele yalivunjwa na kichwa chake kikajeruhiwa, na damu ikatiririka usoni mwake. Mayahudi nao walimfanyia uchawi, na alitiliwa sumu, na ali ndani ya nyumba yake [alipotuhumiwa tuhuma ya uzushi mkewe Aisha Allah amridhie na tendo chafu], pia walifariki watoto wake sita, na hakubaki katika watoto wake ila Fatima Allah amridhie; basi hayo yote hayakumzuia kuwanufaisha watu na elimu na nuru.

Allah alisifu subira ya Mitume na azimio lao kwa kauli yake:

﴿ وَجَعَلْنَا مِنْهُمْ أَئِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا لَمَّا صَبَرُوا ۖ ﴾

{Na tukawafanya maimamu wakiongoa watu kwa amri yetu} [Al-Anbiyaa: 73].

Masahaba Allah awaridhie nao walitolewa majumbani mwao, na jambo la kutoka mjini halikuwadhoofisha katika kuinusuru dini; basi Allah akajaalia kanzi za mfa funga mawe katika tumbo kutokana na shida ya njaa. Alituhimiwa

lme wa fursi [Kisraa] na mfalme wa roma [Qaiswar] kuwa chini ya mikono yao, na katika vita vya Khandaq: wanapata baridi na njaa, na hali nyoyo zipo kooni kutokana na hofu; na wakasubiri juu ya hilo kwa ajili ya kufikisha dini ya Allah.

Masahaba pia walifikwa na msiba mkubwa; nao ni kufa kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie; basi huzuni yao ya kufa kwake [Nabii] haikuwa kizingiti cha kulemaza kuendelea kwao katika kulingania kwa Allah na kupigana jihadi katika njia yake, basi wakatembea juu ya mwenendo wa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie katika maisha yake. Abu Bakr Allah amridhie alituma Jeshi la Usama [lilioandaliwa na Mtume], na akawapiga vita walioritadi, akawapiga vita waliozuilia zaka, Allah akaunusuru Uislamu na akaudhihirisha juu ya dini zeto.

**Na baadha ya haya, enyi Waislamu:**

Basi dini ya Allah ni yenye nguvu, na Allah ni Mwenye kuwanusuru wafuasi wake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿كَتَبَ ٱللَّهُ لَأَغۡلِبَنَّ أَنَا۠ وَرُسُلِيٓۚ﴾

{Allah ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume wangu tutashinda} [Al-Mujaadilah: 21].

Na iwapo Waislamu watadhoofika katika zama, basi Allah ni Mwenye kuwanusuru endapo watarudi kwake:

﴿إِن تَنصُرُواْ ٱللَّهَ يَنصُرۡكُمۡ﴾

{Mkimnusuru Allah naye atakunusuruni} [Muhammad: 7].

Na iwapo Waislamu watavunjika katika sehemu, basi wao ndio wenye kushinda [mwishoni] hata wakishindwa [mwanzoni], na mtihani wa muumini ni hafifu wenye kukatika, na mtihani wa kafiri ni mzito wenye kufululiza, [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَلَا تَهِنُواْ وَلَا تَحۡزَنُواْ وَأَنتُمُ ٱلۡأَعۡلَوۡنَ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ﴾

{Wala msilegee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini} [Aalu Imraan: 39].

Furaha ya makafiri ya ushindi juu ya madhaifu ndio udhalilifu kwao; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يُحَآدُّونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥٓ أُوْلَٰٓئِكَ فِي ٱلۡأَذَلِّينَ﴾

{Hakika wanaompinga Allah na Mtume wake, hao ndio miongoni mwa madhalili wa mwisho} [Al-Mujaadilah: 20].

Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Anayoyapata kafiri katika ushindi na nusra ni duni ya anayoyapata muumini kwa kiwango kikubwa; bali ndani ya hilo ni udhalilifu, kuvunjika na utwevu, hata ikiwa dhahiri ni kinyume chake", na Allah kuiacha dhuluma ya makafiri [waendelee kudhulumu]; ni kwa ajili wazidi kupata madhambi na adhabu.

**'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'**

﴿وَلَا يَحۡسَبَنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ أَنَّمَا نُمۡلِي لَهُمۡ خَيۡرٞ لِّأَنفُسِهِمۡۚ إِنَّمَا نُمۡلِي لَهُمۡ لِيَزۡدَادُوٓاْ إِثۡمٗاۖ وَلَهُمۡ عَذَابٞ مُّهِينٞ﴾

{Wala wasidhani wale wanaokufuru kwamba huu muhula tunaowapa ni kheri yao. Hakika tunawapa muhula wazidi madhambi. Na yao wao ni adhabu ya kuwadhalilisha} [Aalu Imraan: 178].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote astahili Allah kwa wema wake [kwetu], na shukrani zote astahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Mnao katika kutahiniwa na maadui; kuisafisha imani, kunyanyuliwa malipo, kufutiwa madhambi, kupatikana mashahidi, kunusuriwa dini, kurudi [kutubia] Waislamu kwa Allah na kudhihiri vitimbi vya maadui wa dini.

Na misiba inayowafika Waislamu; hakika si mengine ni kuwaamsha, na msukumo wa kuwafanya wajihasibu nafsi zao, na kutubia kwa Allah, na kusimama na maamrisho yake, na kutupilia mbali sababu za udhaifu na hitilafu, na kuomba kunusuriwa kutoka kwa Allah.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...


# JEDWALI LA YALIOMO

UTANGULIZI ........ 5
KUMWAMINI ALLAH ........ 6
MJA KUMTAMBUA MOLA MLEZI ........ 7
HOTUBA YA PILI ........ 16
KUWA NA HOFU YA ALLAH. ........ 17
HOTUBA YA PILI ........ 26
KUAMINI MALAIKA ........ 27
KUAMINI MALAIKA ........ 28
HOTUBA YA PILI ........ 33
KUAMINI VITABU ........ 35
QUR-ANI TUKUFU ........ 36
HOTUBA YA PILI ........ 40
UTUKUFU WA QUR-ANI ........ 42
HOTUBA YA PILI ........ 54
KUAMINI MITUME ........ 56
MANABII NA MITUME ........ 57
HOTUBA YA PILI ........ 63
HAKI ZA NABII SWALA NA SALAMU ZA ALLAH ZIMSHUKIE ........ 65
HOTUBA YA PILI ........ 73
KUMUITIKIA ALLAH NA MTUME SWALA NA SALAMU ZA ALLAH ZIMSHUKIE. ........ 74
KUAMINI SIKU YA MWISHO ........ 84
ALAMA ZA KIYAMA ........ 85
HOTUBA YA PILI ........ 92
MASIHI DAJJALI ........ 95
HOTUBA YA PILI ........ 102

SIKU YA MWISHO: SIKU YA MALIPO. ........................................................ 103
HOTUBA YA PILI ........................................................................................ 108
VITISHO VYA SIKU YA KIYAMA. ............................................................... 110
HOTUBA YA PILI ........................................................................................ 116
KUAMINI KADHAA NA QADAR.................................................................... 117
TAWAKKUL (KUMTEGEMEA ALLAH)........................................................... 118
HOTUBA YA PILI ........................................................................................ 128
KUWA NA DHANA NJEMA KWA ALLAH....................................................... 130
HOTUBA YA PILI ........................................................................................ 141
KHERI IPO NDANI YA ALIYOYAJAALIA ALLAH. ............................................ 142
HOTUBA YA PILI ........................................................................................ 150
KUSUBIRI KATIKA MISIBA.......................................................................... 151
HOTUBA YA PILI ........................................................................................ 158
HOTUBA YA PILI ........................................................................................ 166
JEDWALI LA YALIOMO ............................................................................... 167

**TAASISI YA TWALIBUL ILM YA KUNUSHURU NA KUGAWA**

**00966506090448**





## NI KATIKA MATOLEO YETU


### SILSILA ZA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI





Nguzo Za Uisilamu




Tawhidi




Tabia



Nabii swala na salamu za Allah
zimshukie na Masahaba zake
Allah awaridhie